ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.

24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.

36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
47.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.

51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.

72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 29 Juni, 2010

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kwa mwaka 2010/2011 naomba kuwasilisha. Ahsante.

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Asaa Othman Hamad (Waziri Kivuli wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 50

Mikopo ya *ZSSF*

Mhe. Ali Denge Makame – Aliuliza:-

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) umeanazishwa kwa ajili ya kuwasaidia wafanyakazi kwa shida zao mbali mbali pamoja na kuwapatia mafao ya uzeeni. Kuwepo kwa Mfuko huo kwa kiasi kikubwa kunategemea michango ya wafanyakazi. Mfuko huo hukopesha taasisi za umma kwa lengo la kuzisaidia na kujipatia faida kidogo.

Mhe. Waziri, kwa nini mfuko huo usitoe mikopo kwa wanachama wake ambao ndio wanaochangia, ili wafaidike zaidi na mfuko huo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kumradhi kidogo, kama ulivyosema zana tuliziacha njiani. Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 50 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, lengo kubwa la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) ni kuwalipa wanachama wake mafao ya uzeeni. Maana ya uzee kwa mujibu wa tafsiri ya Hifadhi ya Jamii ama ni kufikia umri wa kustaafu ambao wa hiari ni miaka 55 na wa lazima ni miaka 60. Sababu nyengine ni kupata ulemavu wa kudumu utakao mnyima mfanyakazi kuendelea na kazi katika soko la ajira na kwa hali hii; mfanyakazi hupata mafao sawa na yule aliyekifia umri wa kustaafu na akastaafu kazi;

(b) Fursa ya mikopo hupatikana katika mabenki. Iwapo *ZSSF* itaanzisha utaratibu wa kukopesha wanachama wake kwa sasa, kuna uwezekano mkubwa na Mfuko kushindwa kuwa endelevu, kulipa kwa wakati mafao ya wastaafu wanapofikia uzee na hivyo kushindwa kutimiza lengo la asili la kuanzishwa kwake. Yaani kuhifadhi jamii hali ya uzee haitaruhusu kutafuta kipato kwa kufanya kazi za ajira; na

(c) Msimamo huu unaendana na ushauri uliotolewa na Washirika wetu wakubwa wa Maendeleo katika fani hii ya Hifadhi ya Jamii. Nao ni Shirika la Kazi Duniani (*ILO*). Kufuatia tafiti zilizofanyika miaka ya 2002 na 2006 juu ya hali ya fedha ya mfuko. Mara zote mbili *ZSSF* imeshauriwa kutotumika kwa ajili ya utoaji wa mikopo kwa wanachama.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri anakiri kwamba Mfuko huu huwa unawekeza kwa ajili ya kuwekea watu kiinua mgongo chao. Lakini Mfuko wakati wanapopokea pesa za wateja wake huwa wanazifanyia biashara kwa kujenga majengo mbali mbali kama vile mabenki au *guest house*. Je, katika faida hiyo wateja wake anawapa chochote?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, nakubaliana na yeye kwamba ni kweli Mfuko unawekeza mapesa yake haya katika miradi mbali mbali ya maendeleo.

Hili ndio lengo hasa la Mfuko kuufanya endelevu basi wametakiwa kwa taratibu zao za Hifadhi ya Jamii wawekeze tena kwa kiwango fulani tu, wakizidi kuwa nacho fulani kwenye hizo *investment* basi wanaambiwa uzeeni. Tunao mfano huo katika majumba yale ya Chukwani, basi tathmini ilipofanyika ikaonekana Mfuko una asset nyingi kuliko pesa za mkononi. Sasa ni hatari watu wanapokuja kudai haki zao itakuwa hawana mfuko. Kwa hivyo, wana *threshold*, yaani mahala tena wakishafika hapo wasiendelee zaidi ya hapo. Kuhusu suala lake kwamba faida kuwapa wanachama. Kwa sasa utaratibu huo haupo, lakini hiyo ni rai tunaweza kuizingatia tukaifikiria.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Nakushukuru sana Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi ya kuuliza swali kwa Mhe. Waziri. Mhe. Spika, kwa kuwa sheria za kazi zinaruhusu kuacha kazi kwa hiari ikiwemo na kutoa *notice* ya masaa 24 ikiambatana na kuacha mshahara mmoja.

Je, *ZSSF* walilizingatia hili kwa sababu limo katika sheria. Kama hawakulizingatia ni kwa nini hawaoni kuwa ni matatizo kuwa mtu unamnyima haki yake. Pengine ameacha hii *notice* labda ana miaka 25, lakini kukaa kusubiri mpaka wakati wa kustaafu haoni kama huko ni kumnyima haki yake.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, naomba kusisitiza tena kama nilivyosema kwenye jibu langu mama. Mfuko huu madhumuni makubwa kabisa ya kuuanzisha ni kuwasaidia wanachama wake mafao ya uzeeni. Na nikajitahidi kuelezea huo uzee ukoje. Kama alivyosema Mhe. Zakiya Omar kwa hiari kuanzia miaka 55 na kwa lazima miaka 60. sasa lengo ni kuwasaidia ukishafika uzeeni, hiyo ndio lengo.

Huko nyuma nafikiri tulikuwa na matatizo ya kupata mafao na watu kama hawa kuwasaidia, sasa serikali ndio ikaona ianzidhe utaratibu huu wakati wewe kijana una uwezo basi ujichumie ili uweke utu uzimani, usije tena kidogo ukawa mzigo. Lakini hicho ulichokichuma ujanani kwako kikusaidie *essence* kwamba ni uzeeni. Sasa hii *point* aliyosema kama mtu kaamua. kuacha kazi kama ni kijana umeacha kazi basi ile hakiba yako pale katafute kazi kwengine ukipata kazi njoo unaendelea kwenye Mfuko mpaka unafikia mzee unapewa haki yako.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, tatizo ambalo linawagusa wafanyakazi wetu wengi wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wanapokatishwa mikataba yao ya kazi.

Suala hili ni kero na tena nategemea kwamba Mkurugenzi anapata shida kubwa sana juu ya matatizo mbali mbali yanayomgusa. Kwa kuzingatia hayo, Mhe.

Spika, pamoja na sheria hii kupita umri wa miaka 55 na 60 ndio watu walipwe mafao yao. Lakini je, sheria hii kwa kuwa sheria si msahafu, yaani katiba na sheria si msahafu, wizara ina mpango gani kwa wale watu wanaokatishwa mikataba yao ya kazi wapate haki yao hata kama hawajafikia umri wa miaka 55 na 60.

Mhe. Spika: Kabla sijamwambia Mhe. Waziri ajibu unajua hapa tunapovunja kanuni kuhusu masuala ya simu halafu ukaipeleka kwa nyuma hii haitofautiani na ile *pick pocket* ya vijana wetu. Kwa hivyo, bora tujihadhari mapema isije ikawa ufundi wa *pick pocket* ndio unaanzia humu. *(Kicheko)*

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, naomba radhi sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, nakiri kwamba alivyosema Mhe. Ali Suleiman kuwa kweli kumekuwa na kesi hizi nyingi sana na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko amekuwa akipata kesi hizi mara kwa mara. Pia nikiri kwamba waheshimiwa mara nyingi wamekuwa wakilisisitiza suala hili hasa ilivyokuwa ni Wawakilishi wa Wananchi linatoka kwa wananchi wetu ambao tunao majimboni kwetu.

Mhe. Spika, labda niseme kwamba hili suala hivi sasa Mfuko uko katika mapitio makubwa sana, tunajaribu kuifumua yote na kuipitia na hatimaye huo Mfuko katika sura mpya itakuja Barazani. Sasa wakati tunazingatia haya, na hili Mhe. Spika, naahidi tutalizingatia na namna gani tunaweza tukalitizama.

Lakini ninachoomba sana Mhe. Spika, nasisitiza tena, kwamba suala la msingi Mfuko huu umekusudia kuwasaidia wakati wa uzee. Kama kutakuwa na kesi kamahizo basi kweli hizo zitakuwa ni mfano wa matokeo yasiotarajiwa tunaweza kutayazingatia. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naahidi kwamba tutalizingatia katika mapitio yetu. Ahsante.

Nam. 43
Ujenzi wa Afisi ya Wizara ya Fedha – Pemba

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Ujenzi wa Afisi ya Wizara ya Fedha Pemba ulianza tarehe 15 Mei, 2009 na ulitegemewa kumalizika mwezi April, 2010 kwa mujibu wa mkataba. Kwa bahati mbaya hadi sasa jengo hilo halijamalizika kutokana na kujitokeza matatizo ya kiufundi yakiwemo eneo la nyuma ya jengo kudidimia na sehemu kubwa kufanya nyufa na kulifanya jengo lipoteze ubora wake. Kwa matokeo hayo, mshauri wa ujenzi (*Consultant*) alizuia ujenzi huo usiendelee.

(a) Je, Mhe. Waziri serikali imechukua hatua gani kwa mjenzi baada ya kazi ya ujenzi kusimamishwa?

(b) Je, ujenzi huo utaendelea lini na nani atalipa gharama za kulifanyia jengo hilo marekebisho kutokana na hitilafu zilizotokea?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 43 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, naomba niungane na Mhe. Mjumbe kwamba ujenzi wa Afisi ya Wizara ya Fedha na Uchumi Pemba ulitarajiwa kukamilika mwezi wa April, 2010 kwa mujibu wa Mkataba. Hata hivyo, kumejitokeza athari ya jengo hilo kutitia. Wizara imepokea taarifa ya awali ya msimamizi wa ujenzi yenye kuonesha chanzo cha tatizo na hatua zinazohitajika za kufanya marekebisho. Mshauri pia alielekeza kusitisha ujenzi kwanza ili kuweza kurekebisha kasoro zilizojitokeza, ili kupata maoni ya kitaalamu yanayojitegemea. Wizara pia kwa upande wake imeona ni busara kutafuta kampuni nyengine kuweza kutathmani athari hio na kutoa mapendekezo ya marekebisho. Maamuzi ya wizara yatazingatia ushauri kutokana na ripoti zote hizo mbili nilizozitaja; na

(b) Mhe. Spika, mustakbali wa ujenzi huo utajulikana baada ya kupatikana ripoti ya mshauri aliyeteuliwa. Kwa hivi sasa ripoti hizo hazijakamilika na hivyo hatuwezi kusema hasa *the way forward.* Ahsante.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, athari iliyotokea katika jengo lile sote ilituumiza na ni hasara kwetu. Katika kufuatilia tulipata taarifa kuwa, kabla wizara haijajenga ilikuwa na mashauri ya karibu kabisa na wahusika wa ujenzi kutoka Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Wao walitoa ushauri wao kutokana na ile hali ya pale mahala palivyo.

Lakini nasikia kuwa wizara haikutaka kufuata ushauri huo na badala yake ndio tukapata hasara kama ile. Sijui suala hili ni kweli? Ikiwa ni kweli kwa nini wizara ikapuuza mashauri ya wale waliowataka kuwapa ushauri kwa ujenzi wa jengo lile.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, hiyo sio kweli kabisa. Kiwanja kile tumepewa na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na wao tuliwaonesha ramani yetu na mipango yetu tukakaa pamoja. Kwa hivyo, kwamba labda tumekitafuta wenyewe tukafanya ukaidi hiyo sio kweli.

Mhe. Spika, ukweli kabisa tumeshauriana vizuri ile niseme ni ajali tu imetokezea bahati mbaya na kwa kweli hilo hutekezea kama zinavyotokea ajali nyengine. Lakini kwamba sisi tumefanya ukaidi watu wa fedha ujenzi wapi na wapi? Lakini tumetafuta wataalamu wenyewe na tumefuata taratibu zote. Hiyo kama ninavyosema kwamba imetokea ajali sasa tuone kutokana na ripoti hizo za wataalamu wetu wanatushauri nini.

Tatizo kubwa pale mahala panatitia maji na ujenzi wa pahala penye maji panataka utaalamu mkubwa sana. wameelekezwa vyote wamefanya, lakini bado hatukufanikiwa.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na *consultant* kuzuia ujenzi huo kutokana na athari iliyojitokeza na kushauri kufanyika marekebisho, lakini baadae *consultant* huyo aliruhusu ujenzi kuendelea. Kwa kuwa baada ya *consultant* huyo kuruhusu ujenzi kuendelea, lakini hatimaye kulitokea athari nyengine ya kuanguka kwa jengo hilo wakati wa ujenzi.

Je, Mhe. Waziri, utakubaliana nami kwamba waliopewa dhamana ya ujenzi ule hawana uwezo wa kulijenga jengo lile.

Lakini pili, utakubaliana nami kwamba iko haja sasa jengo lile livunjwe lote lianze upya ili apatikane mkandarasi ambaye anaweza kujenga jengo la uhakika.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kama nilivyosema sisi kwa upande wetu kama wizara tumetafuta *consultant* na kwa kweli *consultant* huyu anatambulika kwa hapa nchini kwetu, anaitwa *KMN Ach Plans Tanzania LTD.*

Tume *flow tender* na tukampata huyo *consultant*. Yeye sasa ndiye anayesimamia huo ujenzi wote, na nafikiri Mhe. Salmin ni mzoefu kidogo anasimamia ujenzi unakwenda hatua kwa hatua. Unapomaliza hatua moja *consultant* anapasisha kweli hatua hii imepasi tunakwenda hatua nyengine. Sasa baada ya kutokea tatizo lile na baada ya ule ujenzi wa kutokea tatizo la kumong'onyoka kwa sababu haukuanguka kwa kweli, lakini ulianza kumong'onyoka kidogo tukapata

hiyo habari. Kwa hivyo, tukamuona huyu bwana na akasema tusimamishe tuone hali ikoje? Sasa kwa kweli na yeye kidogo alizidiwa maarifa, akasema kweli kama ulivyosema hebu tuendelee, kuanza kuendelea mmong'onyoko ukaanguka juu zaidi. Sasa hapo ndio wizara ikaona tusiendelee zaidi bora tusimamishe. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba kwa hivi sasa ujenzi umesimamishwa kabisa tunatafakari kupitia hawa wataalamu, huyu *Independent Consultant* na huyu *Internal Consultant* wetu watupe ripoti kamili halafu tuweze ku-*determine* tuendelee vipi.

Kuhusu mjenzi hana uwezo. Hilo siwezi kulisema Mhe. Spika, kwa sababu tumerusha *tender* na huyu ndiye aliye *build* na kamati ile ndio iliyompitisha na vigezo vyote pamoja na taratibu vimefuatwa. Unaweza kweli ukapanga mwenyewe vizuri ukaendeleza kazi zako, lakini ikitokea ajali ndio ajali imetokezea tusiseme kwamba hana uwezo. Mimi ninaamini kabisa anauwezo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa sababu jengo karibuni lilikatika *canopy* ya juu na ilionekana wazi wazi inaning'inia na kifusi kiko chini na sio mmong'onyoko mdogo kama alivyosema Mhe. Waziri. Je, Mhe. Waziri atakubaliana kwamba, ili kuzuia hasara zaidi ni afadhali kulisamehe lile jengo likapigwa buldoza na tukaanza jengine jipya na *consultant* akawajibika katika gharama ile.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, Mhe. Rashid Seif angekuwa *engineer by profession*, ningekukubalia. Lakini wewe ni mwalimu, mimi mtaalamu wa kilimo na sisi Wizara ya Fedha ni wataalamu wa fedha. Tuwaachie ma-*engineer* wenyewe, sisi tushasema tunawapa kazi wataalamu wetu, hebu tuwaamini kipindi kidogo tu na kazi haiendelei. Wao watatuambia tulivunje, tutie buldoza, tuamue. Sasa hivi kama ninavyosema Mhe. Rashid wewe ni mwalimu sio *engineer*, tuwape uwanja hao wataalamu watatuambia wao nini cha kufanya. Mhe. Spika, ahsante.

Nam. 82

Maendeleo ya Chelezo cha Malindi

Mhe. Ali Denge Makame – Aliuliza:-

Serikali imekiimarisha Chelezo cha Malindi kwa lengo la kibiashara na kupunguza gharama kwa kuvipandisha vyombo vinavyotumiwa na Shirika la Bandari. Chelezo hicho kina uwezo mkubwa kwani kimefikia hatua ya kutengeneza *tug pull* ambayo inatumiwa na Shirika la Bandari kuongozea meli kubwa ziingiazo bandarini hapo.

(a) Je, Mhe. Waziri, serikali ina mpango gani wa kukiimarisha chelezo hicho ili kiweze kufanya kazi zaidi za biashara na kutengeneza vyombo vitakavyohitajika kwa matumizi ya serikali na kibinafsi?

(b) Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, chelezo hicho kinakabiliwa na changamoto zipi na wizara yako inachukua hatua gani kukabiliana nazo?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria Kikao cha Baraza ili kutekeleza Majukumu tuliyopangiwa.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 82 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Wizara yangu kupitia Shirika la Bandari ina mpango wa muda mrefu wa kukiimarisha Chelezo cha Malindi awamu kwa awamu, ikiwa ni pamoja na kurekebisha njia za reli za Chelezo hicho hadi kufikia urefu wa mita 140 ili kuweza kupata kina kikubwa cha maji ambacho kitapelekea vyombo vyenye "*Draft*" kubwa kupandishwa katika Chelezo hicho. Aidha, tayari wataalamu wamechukua vipimo mbali mbali vikiwemo vya utafiti wa udongo (*Soil Investigation*) mbele ya Chelezo kwa lengo la kujua njia gani itatumika ya kurefusha reli hizo za chelezo kwa upande wa baharini; na

b) Chelezo cha Shirika kiliopo Malindi kinakabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo ukosefu wa wataalamu waliobobea, kina kidogo cha maji, upungufu wa baadhi ya vifaa pamoja na mazingira machafu yanayosababishwa na kuwepo kwa Diko la eneo hilo. Aidha, hatua za kukabiliana na changamoto hizo, tayari zimeshaanza kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kurefushwa zaidi chelezo chenyewe, pamoja na kuwepo mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi wake na kuimarisha matumizi ya eneo hilo ili kuzuia msongamano mkubwa wa watu.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wafanyakazi wa kizalendo waliopo kwenye chelezo hiki wamefikia hatua ya kutengeneza *tug* ambayo imeitwa *pull* kwa kubebea mizigo na kuweka sawa matishali. Je, anawahamasisha vipi watendaji hao wa kizalendo ambao wamefika kubuni kutengeneza tagi hiyo. Na ana mpango gani wa kuwapeleka masomoni au keshapeleka wangapi ili kuongeza

zaidi bidii ya ujuzi wa kufanya utaalamu wa kutengeneza vifaa kama hivyo. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwanza nichukue pongezi zake Mhe. Mwakilishi kwa kuwapongeza wafanyakazi wetu kwa kufanya kazi nzuri. Lakini vile vile kwa upande wetu kama wizara kwa kushirikiana na Shirika la Meli huwa tunatoa motisha kwa wale ambao wanafanya kazi vizuri.

Suala la kuwapeleka masomoni kama nilivyojibu katika jibu katika jibu la msingi kwamba tayari tunachukua juhudi za kuwapeleka masomoni ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na wataalam wenye uwezo zaidi kufanya kazi kwa ufanisi.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, nimechanganyikiwa baada ya kuwa muuliza hoja alikisifu chelezo na shughuli zake. Lakini Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri alipokuwa anajibu alisema chelezo hiki kimekumbwa na matatizo, yaani changamoto ikiwemo wataalam. Je, Mhe. Naibu Waziri mwanzo wa kuunda chelezo hiki walikurupuka tu hawakufanya uchunguzi. Kwa sababu kama walifanya uchunguzi kwa nini jibu liwe kwamba wanakabiliana na changamoto ya wataalam na mambo mengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, ni kweli kama nilivyojibu swali la msingi kwamba tuna changamoto hizo za wataalam. Mhe. Spika, wataalam tuliona ni wale tu ambao walikuwa na uzoefu wa kufanya kazi siku nyingi, lakini hasa hawana ujuzi wa kutosha katika kuona kwamba tunafikia lile lengo tulilokusudia. Ndio pale tuliposema kwamba tutawapeleka masomoni ili kujifunza zaidi masuala mengine. Mhe. Spika, kimsingi kwamba wataalam tulionao wana uwezo kiasi lakini hawafikii ile rekodi ambayo tunakusudia kuwa wafikie.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri kaeleza changamoto mbali mbali zinazokabili chelezo. Kwa kuwa katika kueleza jinsi gani wanavyokabiliana nazo anasema kuna wafanyakazi aliowapeleka masomoni.

Naomba kujua Mhe. Spika, wafanyakazi aliowapeleka masomoni wanachukua fani gani katika masomo yao na katika ngazi gani ya elimu ili wakirudi waje waweze kufanya kazi vizuri. Lakini (b) pia kaelezea changamoto ya vifaa na akasema vifaa hivyo wamo katika kupambana na changamoto hilo. Ni vifaa gani mpaka sasa vya chelezo hiyo vilivyoagiziwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kama Mhe. Mwakilishi atakuwa amefuatilia kwa makini katika jibu langu la msingi nilichozungumza kwamba tunakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo ukosefu wa wataalam wenye uwezo. Kwa misingi hiyo kwamba tunapanga ili kuwapeleka masomoni hatujawapeleka hivi sasa, kwa hivyo hatuwezi kukwambia tumewapeleka wanachukua fani gani. Lakini pia vifaa hatujaagiza tumo tu katika harakati za kuona kwamba mwaka wetu wa fedha ndio tayari umeshafika Januari kama nilivyojibu katika swali la msingi, kwa hivyo tunajipanga tuhakikishe kwamba haya masuala yote tunayatekeleza kwa wakati ambao utafikiwa.

Nam. 95

Hali ya Nyumba za Shirika la Utalii

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza**:-**

Shirika la Utalii ni moja ya Mashirika ya Serikali ambalo hujiendesha kibiashara na kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali kupitia vianzio vyake vya mapato, kama vile Nyumba za Mapumziko za Ukanda wa Mashariki ya Unguja ambazo ziko Bwejuu, Jambiani na Makunduchi. Nyumba hizi hivi sasa ziko katika hali mbaya sana na muda wowote zitaanguka.

(a) Je, Mhe. Waziri suala hili unalifahamu?

(b) Kwa kuwa mwekezaji mzalendo aliyekodishwa ameshindwa kuziendeleza. Je, Wizara ina mpango gani wa kuzihami nyumba hizo?

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha alizokodishwa na kwa muda gani?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 95 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika,

(a) Suala la uchakavu unaozikabili nyumba zinazomilikiwa na Shirika la Utalii linafahamika;

(b) Kuna wawekezaji wawili wamekodishwa nyumba za shirika, ambapo mmoja amekodishwa nyumba Bwejuu na mwengine nyumba za Jambiani na Makunduchi.

Aidha, nyumba ambazo zipo katika hali mbaya ni za Jambiani na Makunduchi. Kufuatia mwekezaji mzalendo kushindwa kuziendeleza nyumba hizo, Wizara imechukua hatua ya kufanya mazungumzo na mwekezaji huyo ili kuzirudisha nyumba hizo mikononi mwa shirika. Nyumba ya Jambiani tayari tumeshamalizana nae na iko mikononi kwa shirika na tunaendelea na mazungumzo ili kukamilisha kurudi kwa nyumba ya Makunduchi.

(c) Nyumba ya Bwejuu ilikodishwa kwa miaka mitano mwaka 2003 na baadae imeongezwa miaka mitano mingine mwaka 2008 baada ya mkataba wa mwanzo kumalizika. Gharama za ukodishwaji ni USD 600 kwa mwezi.

Aidha, nyumba za Jambiani na Makundichi zilikodishwa kwa muda wa miaka kumi na tano kwa gharama ya USD 100 kwa mwezi, ili kumpa mwekezaji nafuu ya kufanyia matengenezo nyumba hizo. Kama nilivyosema mwanzo mkataba wa mwekezaji wa nyumba ya Jambiani na Makunduchi umekatishwa na kuna maombi mapya ya wawekezaji ambao wako tayari kuingia ubia na shirika kuziendeleza nyumba hizo.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika jibu mama Mhe. Waziri amekiri kwamba nyumba hizo hali yake hivi sasa si nzuri ni mbovu. Kwa kuwa wawekezaji walipopewa ilikuwa nyumba ni nzima na sasa hivi nyumba zimeharibika mikononi mwao.

(a) Je, nani atalipa gharama ya matengenezo hayo?

(b) Kuna nyumba ya Chwaka pia ina matatizo kama hayo. Je, hii nayo imekodishwa ama bado iko mikononi mwa serikali?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwezekaji: Mhe. Spika, kwa kweli nyumba hizi walipopewa wawekezaji hasa ya Jambiani na Makunduchi zilikuwa katika hali iliyo sasa hivi na mkataba wetu ulikuwa ni kwamba mwekezaji azifanyie matengenezo.

Kwa bahati mbaya mwekezaji alipata mtihani wa maradhi na kushindwa kuendelea na kazi hiyo. Kwa hiyo, ni kweli kwamba kuna maharibiko kidogo yametokea wakati iko mikononi mwake, lakini ni maharibiko ya kimazingira,

maharibiko yaliyosababishwa na mawimbi ya bahari na hasa kwa nyumba ya Bwejuu.

Mhe. Spika, nyumba ya Chwaka iko mikononi mwa Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja na yeye ndio ambaye anaipangia matumizi ya nyumba hiyo.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mbali ya nyumba zile za ukanda wa mashariki ya Unguja, lakini pia Shirika la Utalii nakumbuka pia lilikuwa linamiliki hoteli ya Wete, Mkoani na Chake-Chake. Lakini ile hoteli ya Wete je, mkodishwaji wake ni nani na inatumika vipi. Je, shughuli zile ambazo zinatumika pale za uuzaji wa baadhi ya vilevi imo katika mikataba ambayo Mhe. Waziri amekubaliana na yule ambaye amemkodisha pale.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, hoteli za Pemba zote tatu ya Wete, Chake-Chake na Mkoani zimekodishwa kwa Shirika la *National Marketing* la hapa Zanzibar. Wakati wa ukodishwaji mikataba yetu ni kuwa shirika kuendesha hoteli zile, lakini hatukuingia kwa undani shughuli za kutendeka wakati huo.

Hata hivyo, katika kipindi cha bajeti kilichopita Waheshimiwa Wawakilishi walilalamikia kuhusu hoteli ya Wete na mauzo yanayotendeka pale na yanayotendeka mle ndani. Lakini Mhe. Spika, wizara ilichukua hatua ya kukaa na mkodishwaji na kumueleza *concern* za Waheshimiwa Wawakilishi na kuahidi kwamba angerekebisha hali hiyo.

Nam. 81

Uwekezaji katika Eneo la Fumba

Mhe. Ali Denge Makame – Aliuliza**:-**

Serikali imelitangaza eneo la Fumba kwa uwekezaji kwa zaidi ya miaka 10 sasa lakini uwekezaji uliofanywa ni mdogo mno kulinganisha na ukubwa wa eneo hili na malengo yaliyowekwa.

Je, Mhe. Waziri kwa nini malengo ya kulitumia eneo la Fumba kwa uwekezaji yamekwama.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 81 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, lengo la Serikali kutangaza Maeneo Huru ya Uchumi ya Fumba ni kukaribisha uwekezaji katika sekta ya uzalishaji hasa viwanda kwa lengo la kusafirisha nje ya nchi. Uwekezaji huo ulitarajiwa kufanywa na wawekezaji binafsi ambao nao wanatarajia kukuta eneo hilo likiwa tayari na miundo mbinu inayotakiwa kuwezesha uzalishaji huo kwa gharama nafuu.

Mhe. Spika, pamoja na juhudi zilizochukuliwa na Serikali bado haijafanikiwa kuweka miundo mbinu. Kama nilivyojibu katika swali Nam. 45 tarehe 17 Juni, 2010 kwamba serikali inafanya mazungumzo na Taasisi ya *Jabel Al Free Zone* ya Dubai, lakini pia na wawekezaji wa China ili kwa pamoja kwa mashirikiano na serikali tuweze kuendeleza maeneo hayo kimiundo mbinu na hatimaye yawekezwe.

Mhe. Ali Denge Makame: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa haya maeneo ya uwekezaji baadhi ya wawekezaji wamepewa kwa muda mrefu hawajayatumia kwa kufanya shughuli yoyote na maeneo mengine ambayo yamehifadhiwa na serikali kwa madhumuni ya uwekezaji.. Je, kwa kuwa yale maeneo yamekaa muda mrefu hayajawekezwa, anawaambia nini wananchi waliokuwa karibu na maeneo yale kwa kupanda vipando vidogo vidogo vya kujisaidia kimaisha?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, kwanza naomba nifanye marekebisho kwamba maeneo huru ya Fumba na Micheweni bado hayajapewa wawekezaji. Kwa hiyo, hakuna mwekezaji ambaye amepewa na kwa muda mrefu hayawekeza, bali yamo katika hatua za kutaka kuendelezwa.

Mhe. Spika, kukaa bure kwa maeneo yale hayajakaa bure kwamba hayatumiki, ila wananchi wa Fumba wanatumia maeneo yale kwa kilimo wakijua kwamba serikali itakapokuwa tayari watatakiwa kutoka. Lakini kwa upande wa Micheweni wananchi kama nilivyosema tarehe 17 Juni, 2010 wakati najibu swali Nam. 45 wanatumia maeneo yale kwa kukata matofali. Tunachotaka wafuate maelekezo ya Idara ya Mazingira wakate kwa namna gani. Kwa hiyo, maeneo yale yanatumika kwa shughuli za kiuchumi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika jibu lake amesema kwamba yale maeneo yametolewa kwa ajili ya kuwekeza viwanda. Je, hivi viwanda vilivyotegemewa kuwa wawekezaji wakipatikana wawekeze, ni viwanda vidogo vidogo au ni viwanda vikubwa. Kama ni hivyo, kwa nini serikali isijitutumue ikaweka japo kiwanda kimoja kidogo wananchi wakaanza kuacha kukata yale matofali.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, ni kweli kwamba katika maeneo yale kuna maeneo yamekatwa kwa shughuli za viwanda. Sera ya Viwanda ya Zanzibar inazungumzia viwanda vidogo vidogo na vya kati kama viwanda vya usindikaji samaki, mazao ya baharini, viungo na mazao mengine ya kilimo, pamoja na viwanda vidogo vidogo vya *hi-tech* hivi vya kutengeneza betri, labda simu vitu kama hivyo.

Mhe. Spika, kuhusu serikali kuweka kiwanda, nasikitika kusema kwamba serikali imejitoa katika kufanya biashara. Kwa hiyo, tunachofanya ni kuwahimiza wawekezaji na hasa wafanyabiashara wa ndani wajitahidi kuwekeza katika viwanda na watoke kule walikozoea kununua na kuuza bidhaa nyepesi nyepesi. *(Makofi)*

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa mradi wa serikali miaka kumi ni mingi sana. Dhamira ya serikali ni kuweka maeneo huru ili kuongeza vianzio vya uchumi nchini na kupunguza kuwakamua wale wenye vianzio vile vile ambavyo siku zote vinatozwa kodi. Je, ndani ya miaka kumi katika mpango mkuu wa serikali imeweka mkazo gani ili kukamilisha dhamira ya serikali ya kuweka miundombinu ya kuwavutia wawekezaji.

Lakini (b) kama kweli serikali ina nia hiyo katika kutathmini ndani ya miundombinu. Ni gharama ya kiasi gani inahitajika ili Baraza pamoja na vyombo vyengine vianze kutangaza na kuondoa tatizo la visingizio vya miundombinu. Mhe. Spika, miundombinu inayohitajika kule ni aina tatu. Je, upi umekwaza zaidi yaani ikiwemo barabara, umeme na maji.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, swali (a) Mhe. Mwakilishi alitaka kujua ndani ya miaka kumi je, serikali inaweka mkazo gani. Mhe. Spika, kama alitaka kujua ndani ya miaka kumi iliyopita mkazo ni kukuza sekta zote za kiuchumi na kupunguza umaskini ikiwemo maeneo huru na viwanda. Kama ni miaka kumi ijayo kwa sababu hakunambia iliyopita au ijayo, msimamo wa serikali unabakia ule ule kupunguza umaskini kwa kukuza vianzio vya mapato, lakini pia kukuza ajira katika maeneo huru haya ambayo tunayakusudia.

Mhe. Spika, gharama za miundombinu. Mhe. Spika, kwanza Mhe. Mwakilishi alitaka kujua ni miundombinu gani hasa unaotakiwa kwa haraka. Labda niseme yote kuanzia umeme, barabara, maji na mambo kama hayo. Kwa bahati nzuri haya yote yalikwishafikishwa mpaka kijiji cha Micheweni, kazi iliyobaki ni kuvuta na kufikisha pale kwenye maeneo huru kwenyewe Micheweni Maziwang'ombe. Lakini kwa gharama ya haraka haraka ambayo tuliifanya mwaka 2006 ya kupeleka miundombinu hii kufikia eneo huru la Micheweni,

ZIPA ilitarajia kupewa si chini ya shilingi milioni 900 na zaidi ili miundombinu hii kutoa Micheweni kijijini kufikisha katika maeneo huru na kwa wakati ule serikali haikuweza kufanya hivyo.

Hoja za Serikali

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2010/2011 – Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwa Baraza lako Tukufu, likae kama Kamati ili kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (SW) kutujaalia uzima wa afya na kwa kuibariki nchi yetu kuwa na amani na utulivu. Hali hii ya amani na utulivu ni matunda ya uongozi makini wenye uadilifu mkubwa wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Amani Abeid Karume ambao umezingatia zaidi kukuza uchumi, kuweka misingi ya utawala bora na kuimarisha miundo mbinu.

Kwa niaba ya wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira napenda kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa hekima na busara zake katika kuiongoza nchi yetu na hivyo kutekeleza ilani ya uchaguzi ya CCM kwa mwaka 2005/2010 kwa vitendo.

Mhe. Spika, naomba kumpongeza Waziri Kiongozi, Mhe. Shamsi Vuai Nahodha na Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mhe. Ali Juma Shamuhuna kwa michango na maelekezo yao mazuri wanayotupa katika kuimarisha sekta ya kilimo nchini**.**

Mhe. Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa juhudi zako unazozichukua katika kuliendesha vizuri Baraza lako tukufu ukisaidiana na Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyekiti, Katibu wa Baraza na Maofisa mbali mbali wa Baraza la Wawakilishi.

Aidha, nawashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Baraza kwa michango yao, ushauri, maelekezo na mashirikiano yao mazuri na wizara yetu. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi kwa kuteuliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi. Tunamtakia kila la kheri na mafanikio mema katika utekelezaji wa majukumu mapya ya kazi.

Mhe. Spika, naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa viongozi, wanachama na wapenzi wa CCM wa Jimbo la Kikwajuni kwa umoja na mashirikiano yao mazuri katika kufanikisha vizuri maendeleo ya jimbo na uandikishaji mzuri wa daftari la kudumu la wapiga kura.

Mhe. Spika, tunatoa mkono wa pole kwa wafiwa wa Marehemu Mzee Rashid Mfaume Kawawa aliyefariki dunia tarehe 31/12/2009. Mwenyezi Mungu amlaze pahala pema peponi. Amin. Mhe. Spika, kwa vile nchi yetu inakabiliwa na uchaguzi mkuu katika mwaka huu, nachukua fursa hii ya kumuomba Mwenyezi Mungu atujaalie uchaguzi wa salama na amani ili utulivu uendelee na uwe wa kudumu katika nchi yetu. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kuupongeza uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kusimamia na kutekeleza kwa umakini Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005-2010. Aidha, napenda kukipongeza Chama Cha Mapinduzi kwa kuwa na mikakati imara ambayo imeelekezwa moja kwa moja katika kukuza uchumi wa nchi na kuimarisha mshikamano, amani na utulivu.

Mhe. Spika, utekelezaji makini wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005-2010 umeleta mafanikio makubwa katika sekta ya kilimo. Miongoni mwa mafanikio hayo ni kuongezeka kwa bajeti ya sekta ya kilimo kutoka asilimia 4 ya bajeti ya serikali mwaka 2005 hadi asilimia 7 kwa mwaka 2009. Ongezeko hili linaifanya Zanzibar kuwa ni miongoni mwa nchi zinazotekeleza azimio la *SADC* la Maputo la mwaka 2003 ambalo linaagiza sekta ya kilimo kupewa kipaumbele katika harakati za bara la Afrika za kuwa na uhakika wa chakula na kujikomboa kiuchumi. Mhe. Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana ikiwa ni matokeo ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005-2010 ni pamoja na:

- Utayarishaji wa sera, sheria, mikakati na programu mbali mbali ambazo zimelenga katika kuongeza ufanisi katika sekta ya kilimo. Sera hizi ni sera ya ushirika, sera ya mazingira, sera ya maendeleo ya mifugo na sera ya uhakika wa chakula na lishe;
- Kuongezeka kwa zana za kisasa za kilimo, hivi sasa Wizara ina jumla ya matrekta 45 mazima mengi yao mapya, ikiwa ni sawa na asilimia 83 ya mahitaji ya zana hizo kwa hapa visiwani;
- Uvumbuzi wa mbegu bora za kisasa 3 za mpunga na 4 za muhogo ambazo zina sifa ya kuhimili maradhi, ukame na uzalishaji mkubwa;
- Kuzalisha jumla ya tani 86 za mbegu bora ya mpunga kwa kushirikisha wakulima wenyewe pamoja na kukarabati maghala ya kuhifadhia mbegu na kutengeneza mtambo wa kutayarishia mbegu uliopo hapo Bambi. Mtambo huo ulikuwa umesimama kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 15;
- Kuimarika kwa miundo mbinu ya kuongeza uzalishaji ikiwa ni pamoja na ujenzi wa maabara ya kisasa ya usarifu wa mazao, ujenzi wa visima 6 vipya kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji maji na ukarabati mkubwa wa maabara za utafiti wa kilimo na mifugo;
- Ununuzi wa mtambo wa *liquid nitrogen* kwa ajili ya kuendeleza uzalishaji wa mbegu bora za ng'ombe wa maziwa; na
- Kuongezeka kwa matumizi ya zana za kisasa za uvuvi, ambapo jumla ya vifaa vya uvuvi vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.8 vimetolewa kwa kamati mbali mbali za uvuvi hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa ujumla mafanikio haya yameleta ufumbuzi katika kukabiliana na changamoto zinazokwamisha maendeleo ya sekta ya kilimo hapa Zanzibar.

HALI YA KILIMO NA UZALISHAJI NCHINI

Sekta ya Kilimo na Uchumi

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009 sekta ya kilimo imechangia asilimia 31 ya Pato la Taifa. Hali hii inathibitisha umuhimu wa sekta hii kiuchumi na ni dhahiri kwamba inahitaji kuendelea kupewa kipaumbele katika mipango wa maendeleo ya taifa.

Hali ya Uzalishaji

Mhe. Spika, uzalishaji wa mazao mbali mbali ya chakula kwa mwaka 2009 umeongezeka. Uzalishaji wa zao la mpunga umeongezeka kutoka tani 20,569 mwaka 2008 hadi tani 26,962.50 mwaka 2009. Uzalishaji kwa zao la muhogo pia umeongezeka kutoka tani 149,192.4 mwaka 2008 hadi kufikia 195,546.72 mwaka 2009.

Kwa upande wa viazi vikuu uzalishaji umeongezeka kutoka tani 3,413.25 mwaka 2008 hadi kufikia tani 11,372.5 mwaka 2009. Viazi vitamu pia vimeongezeka toka tani 50,267.5 mwaka 2008 hadi tani 53,587.5 mwaka 2009. Aidha, uzalishaji wa zao la mahindi nao umeongezeka kutoka tani 1,627.5 mwaka 2008 hadi tani 2011.75 mwaka 2009 *(Kiambatisho Nam. 1).*

Mhe. Spika, uzalishaji wa maziwa unatarajiwa kuendelea kuimarika kutokana na jitahada zinazochukuliwa na wizara yangu za kuwapatia wafugaji mitamba bora ya ng'ombe na mbuzi wa maziwa, pamoja na kuimarisha huduma za upandishaji ng'ombe kwa sindano. Aidha, jitihada zinazochukuliwa za kuimarisha jumuiya za wafugaji na ushiriki wa sekta binafsi katika kutoa huduma mbali mbali za mifugo na kuwekeza katika miundombinu ya uzalishaji na masoko zitatoa msukumo mkubwa katika maendeleo ya sekta hii.

Mhe. Spika, uvuaji wa samaki kwa mwaka 2009 umeripotiwa kuwa ni tani 25,396 mbazo zina thamani ya Sh. 47,714,069,526 ukilinganisha na mwaka 2008 tani 24,803 ambazo zina thamani ya Sh. 36,895,537. Kwa upande wa mwani, uzalishaji wa mwani kwa mwaka 2009 ulikuwa ni tani 10,248 ambazo zina thamani ya Sh. 1,665,542,469, ukilinganisha na mwaka 2008 tani 10,792 ambao ulikuwa na thamani ya Sh. 1,672,269,610.

ATHARI ZA UKOSEFU WA UMEME KWA SEKTA YA KILIMO

Mhe. Spika, kukosekana kwa huduma za umeme kuanzia mwezi wa Disemba, 2009 hadi Machi, 2010 kuliathiri sekta ya kilimo, hasa kilimo cha umwagiliaji maji katika mashamba ya mpunga, pamoja na uhifadhi wa mazao, ikiwemo maziwa, nyama, samaki. Aidha, ukosefu huo wa umeme pia uliathiri utotoaji wa vifaranga vya kuku hapa nchini pamoja na kuharibika kwa kemikali na kutokufanyika kwa tafiti mbali mbali katika maabara zote ziliopo Kituo cha Utafiti Kizimbani.

Mhe. Spika, tathmini iliyofanyika katika mabonde matatu ya kilimo cha mpunga wa umwagiliaji maji ya Kibokwa, Bumbwisudi na Cheju imeonesha kwamba maharibiko yalifikia asilimia 50 kwa ujumla. Ukosefu wa maji uliosababishwa na ukosefu wa umeme wa kuendeshea pampu katika visima vya maji ulisababisha

kukosekana kwa tani 200.4 za mpunga zilizotarajiwa kuvunwa katika maeneo hayo.

Aidha, inakisiwa kuwa wakulima 501 katika mabonde hayo walipata hasara ya jumla shilingi 100,000,000. Athari nyengine zilizojitokeza ni pamoja na upungufu wa chakula kwa wakulima hao na kuathiri maisha ya wananchi wapatao 3,006.

Mhe. Spika, tunaipongeza kwa dhati Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi kubwa ilizozichukua katika kurudisha umeme hapa Unguja. Wizara inawashukuru wananchi wote hasa wakulima na wafugaji kwa ustahamilivu wao wakati wote wa ukosefu wa huduma hii muhimu ya umeme na kwa kushirikiana na Serikali yao kwa hali na mali wakati wa kipindi hicho kigumu kwetu sote.

Aidha, naomba kuchukua nafasi hii kuipongeza sana serikali yetu chini ya uongozi wa hekima na busara wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mafanikio makubwa ya kukipatia kisiwa cha Pemba umeme wa uhakika ambao utakuwa kichocheo cha kuimarisha maendeleo ya kiuchumi katika nchi yetu.

MKAKATI WA MAGEUZI YA SEKTA YA KILIMO

Mhe. Spika, kufuatia mabadiliko makubwa ya kiuchumi hapa Zanzibar ikiwa ni pamoja na kukua kwa sekta ya utalii na huduma, kukua kwa soko la ndani na kuimarika kwa miundombinu ya barabara imeonekana ipo haja ya kufanya mageuzi ya kilimo. Mageuzi haya yakiwa na madhumuni ya kuifanya sekta hii ikuwe sambamba na matarajio ya ukuwaji wa uchumi na iweze kufaidika na fursa ziliopo katika soko la ndani na kuchangia kikamilifu katika harakati za kupunguza umasikini**.**

Mhe. Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Baraza la Biashara la Taifa (*ZBC*) na wadau wengine wa sekta, hivi karibuni ilizindua Mkakati wa Mageuzi ya Kilimo kwa azma ya kufikia maendeleo ya kiuchumi na kufanya kilimo chetu kuwa cha kibiashara na chenye tija na kupunguza utegemezi wa chakula kutoka nje ya nchi.

Mhe. Spika, mkakati wa mageuzi ya sekta ya kilito, unalenga kuongeza uwekezaji wa serikali na sekta binafsi katika kuendeleza huduma za kilimo na miundombinu ya umwagiliaji, kushajiisha mfumo wa kilimo cha kibiashara, kuongeza usarifu na thamani ya bidhaa za kilimo na kuunganisha wazalishaji na masoko ya ndani na nje ya nchi. Aidha, mkakati huu unatilia mkazo ushiriki wa nguvu kazi ya vijana katika kilimo na utunzaji wa mazingira.

Mhe. Spika, mkakati huu utatekelezwa sambamba na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA II). Aidha, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira inaendelea kufanya majadiliano na washirika wa maendeleo kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa mkakati huo.

TAARIFA YA UTEKELEZAJI MWAKA 2009/2010 NA MALENGO YA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, utekelezaji katika Sekta ya Kilimo kwa mwaka 2009/2010 ulilenga katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo na samaki yenye ubora na tija, kuongeza ufanisi katika uzalishaji na kudhibiti uchafuzi wa mazingira kama ilivyoelekezwa na sera na mikakati ya kitaifa pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Utekelezaji wa kazi za Wizara ya Kilimo kupitia taasisi zake kwa mwaka 2009/2010 pamoja na malengo ya mwaka 2010/2011 ni kama ifuatavyo:-

IDARA YA SERA NA MIPANGO

Mhe. Spika, Idara hii ndio kiungo kikuu cha Wizara ikiwa na majukumu ya kusimamia na kuratibu taasisi za ndani na nje ya Wizara, kukuza mashirikiano na taasisi za Serikali ya Muungano, Jumuiya za Kikanda, Sekta Binafsi, jumuiya na asasi zisisizo za kiserikali pamoja na Washirika wa Maendeleo.

Idara pia inasimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi, utayarishaji na uratibu wa sera, sheria, mikakati na programu za maendeleo, utumishi na mafunzo kwa wafanyakazi.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2009/2010

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/2010 Idara ilikusanya mapato ya jumla ya shilingi 469,578,270 hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2010. Kiwango hiki cha mapato ni sawa na asilimia 33 ya lengo lililowekwa.

Sambamba na kazi hii, Idara pia ilisimamia utayarishaji wa Mswada wa Sheria ya Uhakika wa Chakula na ilifanya mapitio Sera ya Mazingira na Sera ya Maendeleo ya Ushirika. Rasimu hizi zipo katika hatua za mwisho za kuwasilishwa serikalini. Mhe. Spika, jumla ya wafanyakazi 230 wa Idara mbalimbali ziliopo chini ya Wizara wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi katika fani mbali mbali (Kiambatisho 2). Idadi hii ni ongezeko la asilimia 12 ya idadi ya wafanyakazi waliopatiwa fursa za masomo katika mwaka wa Fedha 2008/2009. Idara pia imeratibu mafunzo juu ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI kwa wafanyakazi na wazalishaji.

Aidha, Idara imetoa mafunzo maalumu juu ya udhibiti wa maradhi ya mafua ya ndege kwa wafanyakazi 46.

Mhe. Spika, katika kuendelea kueneza taaluma za kilimo Wizara imeweza kuanzisha jarida la kilimo ambalo linatoa taaluma kwa wakulima na wadau wa sekta ya kilimo. Jumla ya nakala 500 zimetolewa na kusambazwa kwa wadau wa sekta hiyo

Mhe. Spika, Idara inaendela kusimamia utekelezaji wa programu tano za maendeleo, taarifa za utekelezaji kwa mwaka 2009/2010 na malengo ya mwaka 2009/2010 yanaoneshwa katika viambatisho vilivyoainishwa kama ifuatavyo:-

- Programu ya Kuimarisha Huduma za Kilimo–ASSP, **(**Kiambatisho 3**)**;
- Programu ya Kuimarisha Huduma za Mifugo -ASDP-**L (**Kiambatisho 4**)**;
- Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe – FSNP **(**Kiambatisho 5**)**;
- Mradi wa Usarifu wa Mazao ya Kilimo- *Agro-processing*,**(**Kiambatisho 6**)**; na
- Programu ndogo ya kuhamasisha na kutoa mafunzo ya UKIMWI

MALENGO YA MWAKA 2010/11

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 Idara itatekeleza malengo yafuatayo:-

- Kukusanya mapato ya TSh. 1,293,774,000 kutoka vyanzo mbali mbali vya Wizara;

- Kusimamia na kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara na maliasili;
- Kukamilisha taratibu za uwasilishaji sera na sheria mbalimbali za Wizara na kusimamia utekelezaji wake;
- Kuendeleza kazi za tathmini na ufuatiliaji kwa kuandaa ripoti ya tathmini ya hali ya chakula nchini (*Food Balance Sheet*);
- Kusimamia utayarishaji wa Mpango Mkuu wa Utafiti na Elimu kwa Wakulima wa Wizara (*Research and Extension Master Plan*);
- Kuendelea kusimamia programu na miradi ya Wizara;
- Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Wizara (*Strategic Plan*);
- Kuendelea kutoa mafunzo kwa wafanyakazi kwa mujibu wa mahitaji ya taasisi zilizo chini ya Wizara;
- Kuendelea kufanya mapitio ya kazi za wizara (*Functional review*) kwa lengo la kushauri mundo bora wa kitaasisi wa wizara utakaoleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa majukumu ya wizara;
- Kuratibu mashirikiano na taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa na utayarishaji wa miradi;
- Kutayarisha na kutoa jumla ya nakala 2,000 za Jarida la Mkulima na kusambaza kwa wadau wa sekta ya kilimo; na
- Kufuatilia upatikanaji wa Hati Miliki kwa Shamba la Makurunge. Hati hiyo ni kwa ajili ya kupatiwa shamba hilo Chuo cha Kilimo cha Kizimbani.

Mhe. Spika, Hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2010 Idara imepatiwa jumla ya Sh 592,464,639 sawa na asilimia 89.21 ya makadirio ya mwaka 2009/2010. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011 idara inaombewa jumla ya Sh. 936,965,000 kutoka Serikalini.

KAMISHENI YA KILIMO, UTAFITI NA ELIMU KWA WAKULIMA

Mhe. Spika, Kamisheni ina majukumu ya kutoa huduma za elimu kwa wakulima, kuendeleza shughuli za utafiti katika sekta ya kilimo na kuhakikisha upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo pamoja na udhibiti wa maradhi na wadudu waharibifu wa mazao**.**

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2009/2010
HUDUMA ZA PEMBEJEO NA ZANA ZA KILIMO

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 mnamo mwezi wa Januari wakulima wetu walikabiliwa na maafa ya kuvamiwa na viwavi jeshi, wizara imeweza kudhibiti uvamizi na uharibifu uliotokea katika mabonde ya mpunga ambao ulisababishwa na viwavi hivyo.

Jumla ya ekari 960.25 ziliathiriwa katika mabonde ya Cheju, Kilombero, Uzini, Koani, Mtende, Donge, Kibokwa, Mchangani na Tunduni. Wizara ilichukua juhudi za kuwapatia mbegu wakulima walioathirika pamoja na kuwaburugia ili kuwawezesha kupanda upya. Jumla ya tani 14.5 za mbegu ya mpunga na dawa za kuulia wadudu hao aina ya Actellic lita 30, Roggo lita 90, Calchet supa lita 9.5 na Thionex lita 154 zilisambazwa kwa wakulima katika kipindi hicho.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/2010 kazi za utoaji wa huduma za pembejeo na zana za kilimo kwa Unguja na Pemba ni kama ifuatavyo:-

- Jumla ya tani 88.62 za mbegu bora ya mpunga (sawa na asilimia 88.6 ya lengo) zilizalishwa na kusambazwa kwa wakulima wa Unguja na Pemba. Kati ya hizo tani 12.6 zilitolewa bure kwa wakulima ambao walipata athari ya viwavi jeshi. Mbegu iliyosalia iliuzwa kwa bei ya ruzuku ya Sh. 500 kwa kilo moja;
- Jumla ya tani 10 za mbegu ya mahindi zilizalishwa na kusambazwa katika vituo vyote vya Unguja na Pemba;
- Jumla ya matrekta 10 yamenunuliwa (Unguja 6 na Pemba 4) kupitia mradi wa *PADEP* na kugaiwa katika shehia zinazotekeleza mradi huu, pia hivi karibuni tunategemea kupokea matrekta 11 mapya ambayo yamenunuliwa na serikali kupitia fedha za msamaha wa madeni. Aidha matrekta madogo (*power tiller*) 20 nayo yamenunuliwa;
- Jumla ya madereva 52 wamepatiwa mafunzo ya udereva na ufundi kutoka karakana ya Matrekta;
- Jumla ya tani 389.55 za mbolea zimenunuliwa na kusambazwa katika vituo vya kilimo Unguja na Pemba;
- Dawa ya magugu aina ya Satunil lita 20,000 imenunuliwa na kusambazwa katika vituo mbalimbali vya kilimo cha mpunga Unguja na Pemba; na
- Jumla ya ekari 27,027 za mpunga wa kutegemea mvua zililimwa Unguja na Pemba. Huu ni utekelezaji wa asilimia 108 ya lengo.

MALENGO YA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, malengo ya kitengo cha mpunga na pembejeo ni kama ifuatavyo:-

- Kusimamia ukulima wa mpunga ekari 30,000;
- Kuzalisha na kusambaza mbegu bora ya mpunga tani 100, na tani 8 za mbegu za mahindi na mtama;
- Kutengeneza matrekta makongwe 12 pamoja na zana zake kwa Unguja na Pemba; na

- Kununua na kusambaza mbolea tani 2,600 (1,300 TSP na 1,300 Urea)

HUDUMA ZA ELIMU KWA WAKULIMA

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kitengo cha elimu kwa wakulima kilitekeleza yafuatayo:

- Jumla ya vipindi 53 vya redio na TV vilitayarishwa na kurushwa hewani;
- Vipeperushi 1,000 vya kuhamasisha wakulima juu ya uzalishaji bora wa mpunga wa kutegemea mvua, udhibiti wa maradhi na wadudu wa embe pamoja na uzalishaji bora wa mbegu za nafaka vimetayarishwa na kutumika katika mafunzo ya wakulima wa wilaya zote za Unguja na Pemba;
- Wakulima 1,500 wamepatiwa mafunzo juu ya mbinu bora za uzalishaji wa mazao na uhifadhi wa mazingira;
- Jumla ya mabwana shamba na mabibi shamba 92 wa Wilaya za Unguja wamepatiwa mafunzo mbali mbali; na
- Wakulima 25 kutoka Unguja walipatiwa mafunzo juu ya matumizi ya jembe la kukokotwa na ng'ombe.

MALENGO YA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011, kitengo kinalenga kutekeleza yafuatayo**:**

- Kutayarisha na kurusha vipindi 40 vya redio na 30 vya TV;
- Kutayarisha vipeperushi 400 na kutoa makala 30 za Kilimo;
- kutoa mafunzo kwa wakulima 30 juu ya matumizi ya jembe la kukokotwa na ng'ombe;
- Kutoa mafunzo kwa mabwana na mabibishamba 150 juu ya mbinu bora za kilimo; na
- Kufundisha wakulima 400 juu ya ukulima bora wa mpunga wa umwagiliaji maji.

UTAFITI WA MAZAO YA KILIMO

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/2010 kazi zilizotekelezwa na Kitengo cha Utafiti wa mazao ya kilimo ni kama ifuatavyo:-

- Utafiti wa kilimo cha maweni ulifanyika micheweni (Kijiji cha millenia) kwa lengo la kupata mbegu zinazostawi katika maeneo ya ukanda wa maweni;
- Jumla ya miche ya matunda 6,225 na miche 9,760 ya minazi ya asili imezalishwa na kusambazwa kwa wakulima;
- Jumla ya ekari 21 za mbegu mpya za muhogo zimezalishwa na kusambazwa kwa wakulima;
- Mbegu mpya ya mahindi ya Masaya kutoka Morogoro, bado ipo katika hatua za uzalishwaji katika mashamba ya kuzalishia mbegu;
- Mafunzo juu ya matumizi bora ya udongo na hifadhi ya mazingira yalitolewa kwa wakulima na wanafunzi wa ngazi mbalimbali; na
- Baada ya utafiti wa muda wa miaka 3, uliyoshirikisha mbegu zipatazo 18 za mpunga wa ukanda wa juu (*NERICA Varieties*) mbegu tatu zimethibitshwa kuwa na sifa za uzalishaji zinazokubalika na wakulima hapa Zanzibar. Mbegu hizo zimo katika hatua ya kuzalishwa na kusambazwa kwa wakulima.

MALENGO YA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 kitengo kinalenga kutekeleza yafuatayo:-

- Kuendelea kuzalisha mbegu ya muhogo na viazi vikuu na kuzisambaza kwa wakulima;
- Kuendeleza utunzaji wa mbegu asili na za kigeni za muhogo, viazi vidogo na viazi vikuu (*germplasm collection*) pamoja na kuendeleza vishamba vya maonyesho ya kilimo bora cha muhogo katika wilaya mbalimbali;
- Kuzalisha miche 24,290 ya matunda, misitu na viungo na miche 10,000 ya minazi;
- Kuendelea na kutoa mafunzo ya uhifadhi na matumizi bora ya udongo kwa vijana wa maskuli, vyuo na wakulima katika ngazi tofauti; na
- Kuzalisha mbegu ya mpunga wa ukanda wa juu (*NERICA* 1, 10 na 11) kwa kushikiana na wakulima.

HUDUMA ZA UTIBABU WA MIMEA

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/2010 kazi zilizotekelezwa na Kitengo cha Huduma za Utibabu wa Mimea ni kama ifuatavyo:-

- Jumla mitego 16,800 ya nzi wa matunda “fruit flies imewekwa katika maeneo ya Muyuni, Mtende, Mjini Unguja na Makunduchi; na
- Utafiti wa wadudu waharibifu wa mazao ya mboga mboga na muhogo (*Spiral white flies*) kwa kutumia madawa ya asili unaendelea. Baadhi ya wakulima tayari wameanza kupewa mafunzo ya utengenezaji wa dawa hizo.

MALENGO YA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 kitengo kinalenga kutekeleza yafuatayo:-

- Kusambaza mitego 30,000 ya kunasia nzi dume kwa Wilaya za Wete na Mkoani na Wilaya za Kaskazini Unguja pamoja na kuwapatia mafunzo wakulima na mabwanashamba juu ya udhibiti wa nzi hao. Aidha, kitengo kinategemea kupata msaada kutoka kwa wahisani wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (*IAEA*) ambao utaongeza ufanisi zaidi wa udhibiti wa wadudu hao;
- Kutoa ushauri wa kitaalamu na mafunzo kwa wakulima juu ya udhibiti wa wadudu waharibifu na maradhi ya mimea;
- Kuendeleza utafiti katika mashamba ya mahindi/mtama na kuona ni kwa kiasi gani wadudu wenye manufaa (*Cotesia flavipe*) wameenea tokea kupelekwa katika mashamba ya wakulima;
- Kuendeleza kazi za karantini, ukaguzi wa mazao na mimea; na
- Kuendeleza utafiti wa wadudu waharibifu “Spiral white flies” kwa kutumia madawa ya mitishamba na mbolea ya vimelea vyenye manufaa.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Kamisheni ya Kilimo, Utafiti na Elimu kwa Wakulima ilisimamia utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (*PADEP*). Maelezo ya mradi huu yanapatikana katika (Kiambatanisho namba 7)

Mhe. Spika, Hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2010 Kamisheni imepatiwa jumla ya Sh.1,896,715,955 sawa na asilimia 83.8 ya makadirio ya mwaka 2009/2010. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Kamisheni inaombewa jumla ya Sh. 2,448,319,000 kutoka Serikalini.

CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI

Mhe. Spika, Chuo cha kilimo Kizimbani ni taasisi pekee inayotoa mafunzo ya fani ya kilimo hapa Zanzibar. Chuo kinatoa mafunzo kwa vijana waliomaliza elimu ya sekondari na wafanyakazi kutoka idara na taasisi mbalimbali za serikali na binafsi. Hadi hivi sasa chuo kinatoa mafunzo ya ngazi ya cheti. Idadi ya

wanafunzi waliopo chuoni hadi kufikia Mei, 2010 ni 161 (wanawake 107 na wanaume 54).

MALENGO YA MWAKA 2009/2010

Mhe. Spika, utekelezaji wa malengo ya taasisi kwa mwaka 2009/2010 ni kama ifuatavyo:

- Uzinduzi wa Baraza la Chuo umefanyika baada ya kukamilika uteuzi wa wajumbe wa Baraza hilo;
- Vifaa mbalimbali vya mafunzo ya sayansi na tiba za mifugo vimenunuliwa. Aidha, chuo kimepokea nakala 120 za vitabu vya fani mbalimbali ya masomo ya kilimo kutoka maktaba kuu ya Taifa ya Zanzibar;
- Chuo kwa kushirikiana na Mradi wa *PADEP* kimenunua wanyama mbalimbali wanaotumika kwa mafuzo hapo chuoni, wakiwemo ng'ombe wa maziwa 22, mbuzi wa maziwa 16 na wanyama wengine wadogo wadogo; na
- Jumla ya ekari 11 za shamba la chuo zimelimwa (5 muhogo, 4 viazi vikuu, 2 migomba).

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Chuo kinalenga kutekeleza yafuatayo-:

- Kuongeza wigo na ubora wa masomo:-
- Kusajili wanafunzi 35 wa ngazi ya cheti na wanafunzi wa Stashahada 15;
- Kutayarisha mitaala miwili ngazi ya cheti na Diploma na kuiweka katika kiwango cha Baraza la Vyuo vya Taifa vya Taaluma (*NACTE*) pamoja na Kupokea walimu wapya watano (5) na wataalam wa maabara wawili (2);
- Kununua vifaa vya kufundishia ili kukidhi matakwa ya viwango vya Baraza la Vyuo vya Taifa vya Taaluma (*NACTE*);
- Kwa kushirikiana na Programu za ASSP Chuo kitajenga bweni moja (1) jipya, kukarabati maabara, madarasa na mabweni yaliopo;
- Kuandaa na kutekeleza mpango wa kuongeza mapato kwa kutafuta wahisani na kuongeza miradi ili kukifanya chuo kiweze kujiendesha;
- Kuandaa na kutekeleza mpango maalum wa kuwaendeleza walimu na wafanyakazi;
- Kukitangaza chuo katika ngazi ya kitaifa na kimataifa; na

- Kwa kushirikiana na idara ya Umwagiliaji Maji na mradi wa *TANRICE* kuendelea kutoa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga katika mabonde ya umwagiliaji maji.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Chuo kinatarajia kupatiwa ruzuku ya Sh. 271,560,000 kutoka Serikalini.

IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI

Mhe. Spika, Idara ina jukumu la kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji kama ilivyoainishwa katika Mpango Mkuu wa Umwagiliaji Maji (*Zanzibar Irrigation Masterplan*) kwa lengo la kuongeza uzalishaji, tija na kuimarisha uhakika wa chakula.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2009/2010

Mhe. Spika, Kwa mwaka 2009/2010 Idara ilitekeleza yafuatayo:-

- Jumla ya ekari 250, zimeingizwa katika uzalishaji baada ya kujengewa miundo mbinu ya Umwagiliaji kama vile mitaro ya saruji, vigingi, visima na kufungwa pampu (Bumbwi sudi ekari 100, Kibokwa ekari 70, Cheju 35 na Saninga Pemba ekari 45). Hivyo, kufanya eneo lote linalolimwa mpunga wa umwagiliaji maji kufikia ekari 1,825 (sawa na hekta 730);
- Kazi ya uungaji wa umeme (High tension) katika mabonde ya Bumbwisudi na Cheju inaendelea, kazi ambayo imegharimu jumla ya Shilingi 136,000,000;
- Mashamba ya mfano yenye ukubwa wa ekari 5 kwa kumwagilia kwa matone yameanzishwa kupitia vikundi vya wakulima katika vijiji vya Jendele, Kijini na Bumbwini Misufini; na
- Mradi wa Umwagiliaji maji wa Masingini Pemba ambao unafadhiliwa na Japani umeanza kutekelezwa.

MALENGO YA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Idara inalenga kutekeleza yafuatayo:

- Kuendeleza ekari 618 kwa kuziwekea miundombinu ya umwagiliaji maji;
- Kutoa taaluma kwa jumuiya za wakulima wa mpunga na mboga mboga wa Umwagiliaji maji juu ya mbinu bora za kutumia maji kwa ufanisi pamoja na matunzo ya mashamba yao;

- Kwa kushirikiana na *TASAF* (kupitia Programu ya Uhakika wa Chakula) na Mradi wa *MACEMP*, jumla ya ekari 249 zitajengewa miundombinu ya umwagiliaji maji. Maeneo yatakayohusika ni Shehia za Machangani na Tunduni (ekari 40), Bumbwisudi (ekari 45), Kianga (ekari 35), Jendele (ekari 45) na Shehia ya Cheju (ekari 34) kwa Unguja. Kwa upande wa Pemba maeneo yatakayohusika ni mabonde ya Mlemele (ekari 30) na Machigini Mkoani Pemba (ekari 20);
- Kuendeleza teknolojia ya umwagiliaji wa matone (*Drip Irrigation*) katika shehia 12 za Unguja na Pemba;
- Kupitia Mradi wa uendelezaji mpunga Tanzania (*TANRICE*) unaodhaminiwa na Serikali ya Japani, Idara itatoa mafunzo maalum ya uzalishaji mpunga wa umwagiliaji maji Unguja na Pemba;
- Kwa kushirikiana na *PADEP*, Idara inalenga kujenga bwawa na mitaro ya saruji ya kumwagilia huko Kinyakuzi; na
- Kwa kushirikiana na KOICA Idara inalenga kufanya utafiti wa maji (*Hydrological Survey*) kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/2010, Idara imetekeleza miradi miwili ya Umwagiliaji maji ambayo ni mradi wa Mpango Mkuu wa Umwagiliaji maji wenye lengo la kuhakikisha eneo lote lililoibuliwa kuwa linaweza kulimwa kilimo cha Umwagiliaji maji linaendelezwa kwa kilimo hicho. Aidha, Idara inasimamia utekelezaji wa mradi wa Mpango wa Kilimo cha kisasa. Mradi huu unalenga kukarabati na kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji maji iliopo hivi sasa katika hali inayotakiwa

Mhe. Spika, Hadi kufikia April, 2010 Idara imepatiwa jumla ya Sh 282,493,905 sawa na asilimia 86.0 ya makadirio ya mwaka 2009/2010. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011 idara inaombewa jumla ya Sh. 369,006,000 kutoka Serikalini.

IDARA YA MAENDELEO YA MIFUGO

Mhe. Spika, Idara hii ina jukumu la kusimamia maendeleo ya mifugo hapa Zanzibar ikiwa pamoja na kupanga, kuratibu na kutekeleza mikakati na programu za maendeleo ya sekta hii. Pia Idara ina jukumu la kutoa taaluma ya ufugaji bora na teknolojia mpya ya mifugo.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2009/2010

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010 Idara ilitekeleza yafuatayo:-

- Mtambo wa kuzalisha "*Liquid Nitrogen*" umenunuliwa na jengo la kuhifadhia mtambo huo limekarabatiwa kama ilivyoelekezwa na wataalamu wa kampuni iliyotuuzia mtambo huo. Mtambo huo umegharimu jumla ya Dola za Kimarekani 410,000;

- Jumla ya mifugo 122,189 (ng'ombe 14,012, mbuzi na kondoo 2,968, wanyama-kazi 3,500, mbwa 14,528 na kuku 87,181) wametibiwa Unguja na Pemba. Aidha, mifugo 452,539 imepatiwa chanjo dhidi ya maradhi mbali mbali;
- Jumla ya wafugaji 5,840 kwa Unguja na 4,229 Pemba wamepatiwa taaluma juu ya ufugaji bora wa kuku wa kisasa na wa kienyeji, ufugaji bora wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa;
- Jumla ya wananchi 130 (89 Unguja na 41 Pemba), waliteuliwa kutoka vijijini na kupewa mafunzo ya miezi 2 juu ya utibabu mifugo. Wananchi hawa hivi sasa wanatoa huduma hizi kwa wafugaji katika shehia zao;
- Mashamba-darasa 180 yameanzishwa katika kila wilaya Unguja na Pemba ambapo wadau wamepatiwa mafunzo juu ya uzalishaji bora wa mifugo yao;
- Jumla ya wananchi 2,500 (kati ya hao 1,757 ni wanafunzi) wamepatiwa mafunzo juu ya tahadhari ya kujilinda na maradhi ya kuambukiza ya Mafua makali ya ndege na nguruwe pamoja na kichaa cha mbwa; na
- Wataalamu wanne wa Idara walipatiwa mafunzo juu ya namna ya kubaini vimelea vya mafua makali ya ndege katika maabara.

Mhe. Spika, kazi nyengine zilizofanywa na Idara hii ni majaribio ya kuzalisha nishati (*biogas*) kwa kutumia samadi ya mifugo. Zoezi hili limetekelezwa kwa kushirikiana na NGO ya *DANTAN* ya Denmark na *ZALWEDA* ya Zanzibar. Hadi sasa wafugaji sita wa vijijini wameshafaidika na mitambo hii na Wizara yangu inaendelea kushajiisha wafugaji wengi zaidi kutumia teknolojia hii ambayo imeonekana kuwa na mafanikio mazuri.

MALENGO KWA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 Idara inalenga kutekeleza yafuatayo:

- Kushajiisha wafugaji kuzalisha gesi ya kupikia kwa kutumia mbolea ya samadi inayotokana na mifugo yao;
- Kuendelea kutoa huduma za kinga, tiba na ushauri wa kitaalamu kwa wafugaji;
- Kuimarisha upatikanaji wa huduma za upandishaji ng'ombe kwa sindano kwa kutumia mbegu bora za ngo'mbe na mbuzi wa maziwa;
- Kuendelea kuimarisha karantini na ukaguzi wa mifugo na mazao yake kwa lengo la kuikinga mifugo na binadamu dhidi ya maradhi yanayoweza kuletwa na mifugo au bidhaa zake kutoka nje ya nchi;
- Kuziimarisha maabara za uchunguzi wa maradhi kwa kuzipatia zana na nyenzo za kufanyia uchunguzi wa maradhi hayo;

- Kuimarisha majengo yaliyopo katika Jinjio Kuu la Kisakasaka pamoja na uwekaji wa umeme katika kituo hicho na uwekaji wa uzio katika eneo la Karantini; na
- Kuanzisha eneo la karantini ya wanyama huko Pemba.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Idara itaendesha miradi mitatu ambayo ni mradi wa Kudhibiti Kichaa cha Mbwa (Kiambatisho na. 9) Mradi wa Upandishaji wa Ng'ombe kwa Sindano unaotekelezwa na Serikali na Mradi wa Kudhibiti Mafua Makali ya Ndege na Nguruwe (Kiambatisho na 10).

Mhe. Spika, Hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2010 Idara imepatiwa jumla ya Sh 576,510,962 sawa na asilimia 85.5 ya makadirio ya mwaka 2009/2010. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011 idara inaombewa jumla ya Sh. 848,636,000 kutoka Serikalini.

IDARA YA MAZAO YA BIASHARA, MATUNDA NA MISITU

Mhe. Spika, Idara hii ina majukumu ya kushirikiana na taasisi nyengine pamoja na wananchi kuendeleza rasilimali za misitu ya nchi kavu na misitu ya mikoko, kusimamia wanyama pori na kuhamasisha kilimo cha mazao ya biashara.

UTEKELEZAJI WA MALENGO MWAKA 2009/2010

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/2010 Idara ilitekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

- Mpango wa Usimamizi wa Rasilimali za Misitu za shehia nane zinazozunguka Msitu wa Hakiba wa Hifadhi Kiwengwa - Pongwe umekamilika na rasimu zake zimepelekwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kukamilisha taratibu;
- Rasimu ya Mpango wa Muda Mrefu wa Usimamizi wa Msitu 2009 hadi 2020 imekamilika na imepelekwa Serikalini kwa kukamilisha taratibu zilizosalia;
- Mapitio ya Mpango wa Usimamizi wa Rasilimali za Misitu, kwa shehia 10 za Hifadhi ya Maumbile Ngezi – Vumawimbi na Hifadhi ya Taifa ya Jozani, yameanza kwa kufanya mikutano na shehia zinazozunguka hifadhi hizo;
- Mafunzo ya Sheria ya Usimamizi wa Raslimali za Misitu namba 10 ya mwaka 1996 yametolewa kwa wanajamii wa Wilaya zote za Unguja na Pemba;
- Jumla ya miche 930,000 ya miti ya aina mbalimbali iliyozalishwa na vitalu vya Serikali na 610,000 ya vitalu binafsi imepandwa;
- Mpango wa Usimamizi wa Mikoko umekamilika;

- Matayarisho ya mapitio ya Sera ya Misitu ya mwaka 1996 yameanza. Kazi hii itafadhiliwa Mradi wa Usimamizi wa Ardhi na Mazingira (SMOLE);
- Elimu ya ufugaji nyuki na usarifu wa asali umetolewa kwa vikundi 33 vya wananchi (Wilaya Kusini 6, Micheweni 20, Wete 3, Chake chake 1, Mkoani 3); na
- Kaya 1,103 katika Wilaya ya Mjini, Unguja zimeanza kutumia gesi asilia, baada ya kuhamasishwa kutumia nishati hii mbadala ili kupunguza matumizi ya kuni na makaa.

MALENGO KWA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, kabla ya kusoma malengo ya mwaka 2010/2011 napenda kutoa tamko rasmi kuhusiana na suala zima la ukataji wa miti ovyo "Tunawaomba Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Masheha, Vikosi vya ulinzi pamoja na wananchi wote kwa ujumla kukemea vitendo hivi vya ukataji wa miti ovyo" na tabia hii isionekane kama ni jukumu la Wizara ya Kilimo tu, bali ichukuliwe kama ni janga la kitaifa na athari yake ni kwa nchi nzima.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 malengo ni kama yafuatayo:-

- Kutoa elimu ya kilimo cha kisasa kwa mazao ya biashara, uzalishaji bora wa mazao ya misitu, uhifadhi wa maliasili pamoja na taratibu bora za matumizi yake;
- Kuzalisha miche 1,500,000 ya matunda, viungo, mapambo na misitu;
- Kupanda miti ya misitu katika eneo la hekta 60 na kuvuna eneo la mita za ujazo (*Cubic meter*) 2,500 kwenye mashamba ya serikali.
- Kutekeleza Mpango wa Usimamizi wa Misitu ya Mikoko;
- Kufanya semina na wilaya, vyombo vya sheria na ulinzi kuzungumzia usimamizi na sheria za uhifadhi wa miti na misitu.
- Kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Misitu ya Zanzibar ya mwaka 1996;
- Kuendelea kushajiisha matumizi ya nishati mbadala (gesi ya asili);
- Kuimarisha ulinzi wa rasilimali ya misitu na madini;
- Kuimarisha huduma za utalii wa kimaumbile katika Msitu wa Hifadhi wa Kiwengwa; na
- Kuwajengea uwezo wafugaji nyuki Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kabla ya kusoma malengo ya mwaka 2010/2011 napenda kutoa tamko rasmi kuhusiana na suala zima la ukataji wa miti ovyo 'Tunawaomba Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Masheha, Vikosi vya ulinzi pamoja na wananchi wote

kwa ujumla kukemea vitendo hivi vya ukataji wa miti ovyo' na tabia hii isionekane kama ni jukumu la Wizara ya Kilimo tu, bali ichukuliwe kama ni janga la kitaifa na athari yake ni kwa nchi nzima.

Mhe. Spika kwa mwaka 2010/2011 malengo ni kama yafuatayo: -

- Kutoa Elimu ya Kilimo cha Kisasa kwa mazao ya biashara, uzalishaji bora wa mazao ya misitu, uhifadhi wa maliasili pamoja na taratibu bora za matumizi yake;
- Kuzalisha miche 1,500,000 ya matunda, viungo, mapambo na misitu;
- Kupanda miti ya misitu katika eneo la hekta 60 na kuvuna eneo la mita za ujazo *(Cubic meter)* 2,500 kwenye mashamba ya serikali;
- Kutekeleza Mpango wa Usimamizi wa Misitu ya Mikoko;
- Kufanya semina na wilaya, vyombo vya sheria na ulinzi kuzungumzia usimamizi na sheria za uhifadhi wa miti na misitu,
- Kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Misitu ya Zanzibar ya mwaka 1996;
- Kuendelea kushajiisha matumizi ya nishati mbadala (gesi ya asili),
- Kuimarisha ulinzi wa rasilimali ya misitu na madini;
- Kuimarisha huduma za utalii wa kimaumbile katika Msitu wa Hifadhi wa Kiwengwa; na
- Kuwajengea uwezo wafugaji nyuki Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 idara itasimamia miradi mikuu mitatu ambayo ni hii ifuatayo:-

- Mradi wa Uimarishaji Mikarafuu (Kiambatisho namba 11);
- Mradi wa Hifadhi Misitu ya Asili *(HIMA);* na
- Mradi wa Uhifadhi wa Misitu ya Ukanda wa Pwani.

Mhe. Spika, Mradi wa Hifadhi Misitu ya Asili (HIMA) ni mradi wa miaka minne (2010 – 2013) wenye lengo la kupunguza hewa mkaa kutokana na ukataji wa miti ovyo na uharibifu wa misitu na kuongeza kipato kwa jamii, ambacho kitatokana na kutunza misitu ya asili. Mradi huu utagharimu jumla ya Dola za Kimarekani 5,539,175 ambazo zitatolewa na Serikali ya Norway.

Mradi huu una malengo yafuatayo:-

- Kutayarisha muongozo utakaotoa mwelekeo wa utayarishaji wa mipango ya usimamizi wa rasilimali za misitu;
- Kufanya mapitio ya mikataba 17 ya usimamizi wa rasilimali za misitu Unguja na Pemba;
- Kutayarisha mikataba 12 mipya ya rasilimali za misitu kwa kuzingatia ushiriki wa wanajamii Unguja na Pemba;

- Kuhamasisha jamii kutumia nishati ya gesi kwa kupikia ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa; na
- Kusaidia jamii kuanzisha vitalu na kuendeleza mashamba ya miti.

Mhe. Spika, Mradi wa Uhifadhi wa Misitu ya Ukanda wa Pwani ni wa miaka minne (2010 – 2013) wenye lengo la kuyalinda na kuyatambua maeneo ya misitu yaliyo chini ya usimamizi wa serikali na yale yaliyo chini ya usimamizi wa mamlaka za Wilayani (vijijini/shehia).

Mradi pia utayatambua na kuyaimarisha maeneo mapya yatakayoingizwa katika mpango huu. Mradi huu una jumla ya Dola za Kimarekani 900,500 kutoka *Global Environment Fund - GEF*. Mradi huu una malengo yafuatayo:-

- Kuwawezesha wanavijiji kupanga mipango shirikishi na endelevu ya matumizi ya misitu inayowazunguka kwa maendeleo endelevu ya misitu husika; na
- Usimamizi na uimarishaji wa maeneo ya Misitu ya Hifadhi ya Taifa, Jozani-Ghuba ya Chwaka, Hifadhi ya Masingini-Dole, Hifadhi ya Msitu wa Kiwengwa- Pongwe kwa Unguja na Hifadhi ya Msitu wa Ngezi, Ras Kiuyu na Msitu Mkuu kwa Pemba.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2010 idara imepatiwa jumla ya shilingi 694,808,853/- sawa na asilimia 86.1 ya makadirio ya mwaka 2009/2010. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011 idara inaombewa jumla ya shilingi 919,177,000/- kutoka serikalini.

IDARA YA UVUVI NA MAZAO YA BAHARINI

Mhe. Spika, Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini ina jukumu la kusimamia na kuhudumia wananchi juu ya matumizi bora ya rasilimali ya baharini pamoja na kuendeleza kilimo cha mwani.

UTEKELEZAJI MALENGO YA MWAKA 2009/2010

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/2010 idara ilitekeleza malengo iliyojipangia kama ifuatavyo:-

- Kwa kushirikiana na jamii, idara iliendelea kuimarisha kazi ya ulinzi wa hifadhi ya rasilimali za baharini *(MIMCA, MENAI na PECCA).* Pia idara imeendelea na kufanya doria za kawaida na doria maalum kwa kushirikiana na vikosi maalum vya ulinzi

- Kamati za Doria zitakazoshiriki kukabiliana na uvuvi haramu na shughuli za kitalii zimeundwa;

- Juhudi za kuwahamasisha wavuvi wadogo wadogo kujishughulisha na ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini kwa kuanzisha mabwawa ya ufugaji wa samaki zinaendelea katika maeneo ya Makombeni, Chambani, Kiwani na Mtangani (Pemba) na Muanda na Bumbwini (Unguja);

- Uanzishaji wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu *(DSFA)* umeanza ikiwa pamoja na kuchaguliwa wafanyakazi watakaosimamia utaratibu wa mpito *(interim arrangement)*, wakati ikisubiriwa kuridhiwa kwa sheria ya Mamlaka hiyo na Baraza la Wawakilishi;

- Hatua za kuanzisha Sheria mpya ya Uvuvi ya mwaka 2010 zimekamilika na tayari sheria hiyo imeshapitishwa na Baraza lako tukufu;

- Tafiti za kilimo cha mwani mnene *(cottonii)* utakaoweza kutoa tija zaidi kwa wakulima zimeendelea kufanyika katika maeneo ya Kisiwa cha Fundo katika maji ya kina kirefu; na

- Hatua za kuweka maeneo mapya ya hifadhi katika bahari ya Tumbatu na eneo la bahari ya Mji Mkongwe pamoja na kuyatangaza maeneo hayo kisheria zimeendelea.

MALENGO YA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, kwa mwaka wa 2010/2011 malengo ya Idara ya Uvuvi ni kama yafuatayo:-

- Kuendelea kuishirikisha jamii katika uhifadhi wa rasilimali za baharini na mazingira yake na pia kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira ya bahari kwa jamii ya ukanda wa pwani;

- Kuhamasisha uwekezaji katika fani ya ufugaji wa samaki;

- Kuwashajiisha wavuvi vijana kuacha kuvua katika maeneo ya hifadhi na badala yake kwenda kuvua katika maeneo ya kina kirefu; na

- Kudhibiti matumizi ya nyavu zenye macho madogo kwa kushirikisha jamii katika maeneo ya hifadhi na kupiga marufuku matumizi ya nyavu hizo, pamoja na kuendeleza kazi za doria katika maeneo ya hifadhi.

Mhe. Spika, Idara ya Uvuvi na Mazao Baharini kwa mwaka 2010/2011 iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mradi wa *MACEMP* unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Maelezo ya utekelezaji wa mradi huu yameelezwa katika ***(Kiambatisho 8).***

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2010 idara imepatiwa jumla ya shilingi 200,925,127/- sawa na asilimia 79.4 ya makadirio ya mwaka 2009/2010. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011 idara inaombewa jumla ya shilingi 267,666,000/- kutoka serikalini.

IDARA YA MAZINGIRA

Mhe. Spika, Idara ya Mazingira ina jukumu la kusimamia na kuendeleza mpango wa hifadhi ya mazingira katika maeneo ya ardhi, angani na majini, kushajiisha jamii juu ya uhifadhi na kutoa elimu ya mazingira pamoja na kuratibu tathmini za kimazingira.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2009/2010

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010 utekelezaji wa malengo ya idara ulikuwa kama ifuatavyo:-

- Jumla ya vikundi 25 vya mazingira (Unguja 16, Pemba 9) vimepatiwa elimu ya uhifadhi wa mazingira ya ukanda wa pwani;

- Idara imeshirikiana na asasi za kiraia katika kuandaa rasimu ya mtaala wa somo la uhifadhi wa mazingira;

- Jumla ya miradi 270 ya utalii inayoendelea (Unguja 241, Pemba 29) na miradi 19 mipya (Unguja 17, Pemba 2) ilifanyiwa ukaguzi na kupatiwa maelekezo ya kimazingira;

- Tathmini za awali *(Scooping)* kwa miradi ya uwekezaji *(Sea Rock* – Kama, Mnara wa Tigo – Uroa, Kizimkazi, Ras Shungi – Makunduchi na Underwater – Pemba) imefanyika;

- Rasimu za mwanzo za miongozo ya tathmini ya Mazingira *(EIA Guidelines)* imekamilishwa;

- Rasimu ya mwanzo ya viwango vya kimazingira imekamilika kwa ushirikiano na Baraza la Taifa la Mazingira *(NEMC);*

- Jumla ya miradi 45 ya maenedeleo (Unguja 30, Pemba 15) imefanyiwa ufuatiliaji;

- Kazi ya utafiti na ufuatiliaji wa kasa imeanza katika Wilaya ya Kusini kwa kuzipitia Kamati za Uhifadhi wa Kasa;

- Zoezi la kusimamia agizo la serikali juu ya upigwaji marufuku mifuko ya plastiki linaendelea Unguja na Pemba. Tathmini iliyofanywa inaonesha kwamba bado mifuko hiyo inatumika kwa kiwango kidogo isipokuwa kasi inaongezeka;

- Rasimu ya mwanzo ya miongozo ya tathmini za athari za kimazingira imeshakamilika na kuwasilishwa kwa wadau, kwa ajili ya kutoa maoni yao;

- Kazi ya utayarishaji wa mikakati ya mpango wa uwiano wa ukanda wa pwani imekamilika;

- Tathmini ya maeneo yanayoingia maji ya bahari imefanyika kwa kisiwa chote cha Pemba na kazi hiyo inaendelea kwa kisiwa cha Unguja. Aidha, maeneo manne (4) ya Nungwi na Jambiani Unguja na Kisiwa Panza na Fundo kwa Pemba yameshaandaliwa maandiko ya mradi tayari kwa kuwasilishwa kwa wafadhili; na

- Kazi za kuwaangamiza kunguru kwa kuwanasa katika mitego imeanza na mitego 20 imesambazwa katika Mkoa wa Mjini Magharibi na hadi sasa kunguru 4,500 wameangamizwa katika kipindi cha miezi mitatu. Aidha, kuwepo kwa mitego hiyo kumeonesha kupungua kwa kunguru na hata kurudi kwa baadhi ya ndege, ambao hapo nyuma walianza kutoweka.

MALENGO KWA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Idara ya Mazingira inalenga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuendeleza kazi za utoaji wa elimu ya mazingira kwa jamii na wawekezaji;

- Kufanya mapitio ya miradi 180 pamoja na kuratibu tathmini za kimazingira kwa miradi 20 ya maendeleo;

- Kukamilisha utengenezaji wa viwango vya kimazingira kwa bidhaa za mitumba;

- Kuendeleza kazi za ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na kuifanyia tathmini ya kimazingira;

- Kukamilisha kazi za uhifadhi wa kasa pamoja na kufanya utafiti juu ya mazingira ya maisha ya wanyama hao;

- Kuendelea kusimamia upigaji marufuku uingizwaji na matumizi ya mifuko ya plastiki;

- Kuandaa Mpango Mkakati wa utekelezaji wa Sera mpya ya Mazingira;

- Kutekeleza kazi za mpango wenye uwiano wa maeneo ya pwani; na

- Kuendeleza kazi za kupunguza idadi ya kunguru kwa kutumia sumu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, idara ilitekeleza miradi miwili na programu moja.

Mradi wa Matumizi Endelevu ya Ardhi na Mazingira (*SMOLE*)

Mhe. Spika, Mradi wa Matumizi Endelevu ya Ardhi na Mazingira unatekelezwa kwa pamoja na idara nne, ambazo ni Idara ya Mazingira, Idara ya Upimaji na Mipango Miji; Idara ya Ardhi na Usajili na Idara ya Utawala wa Ardhi. Mradi huu unaendeshwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Finland. Mhe. Spika, madhumuni ya mradi huu ni kuandaa mpango wa muda mrefu wa kusimamia matumizi endelevu ya ardhi na mazingira na kujenga uwezo wa idara hizo katika kusimamia masuala ya ardhi na mazingira, ili kuleta maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.

Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani (*MACEMP*)

Mhe. Spika, Idara ya Mazingira inatekeleza baadhi ya vipengele vya Mradi wa *MACEMP* unaoratibiwa na Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini. Vipengele hivyo ni pamoja na Tathmini za Athari za Kimazingira (*EIA*) na Jamii na kuendeleza Mpango wa Uwiano wa Usimamizi wa Rasilimali za Pwani (*ICM*). Aidha, idara inakusudia kukamilisha kazi ya kutengeneza Mkakati wa *ICM* pamoja na kutekeleza kazi zilizoainishwa katika mkakati huo.

Programu ya Usimamizi wa Mazingira

Mhe. Spika, programu hii ina jumla ya miradi midogo midogo mitatu ambayo ni:

- Mradi wa Kudhibiti maji machafu Msingini Chakechake Pemba;
- Mradi wa Changamoto za Millenia Tanzania (MCA-T); na
- Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani kwa Nchi za Magharibi ya Bahari ya Hindi (*ReCoMap*).

Mradi wa Kudhibiti Maji Machafu Msingini Chake-Chake Pemba
Mhe. Spika, Mradi wa Kudhibiti Maji Machafu Msingini Chake-Chake Pemba unatekelezwa na Shehia ya Msingini – Mtoni, Wilaya ya Chake-Chake Pemba wenye lengo la kurekebisha mfumo wa maji machafu katika shehia hiyo. Mradi huu upo katika hatua za mwisho za kuunganisha mabomba kutoka katika majumba hadi katika mtaro mkuu.

Mhe. Spika, mradi huu ulitengewa jumla ya Dola za Kimarekani 150,000 kutoka *UNEP*, shilingi 60,000,000/- kutoka *TASAF* (Shehia za Kichungwani na Msingini) na shilingi 15,0000,000/- kutoka serikalini.

Hadi kufikia mwezi wa Aprili 2010, jumla ya Dola za Kimarekani 150,000 (100%) kutoka *UNEP*, shilingi 60,000,000/- kutoka *TASAF* (100%) na shilingi 3,000,000/- (20%) kutoka serikalini zilitumika. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, mradi huu unategemewa kupata jumla ya Dola za Kimarekani 88,000 kutoka *UNEP* na shilingi 20,000,000/- kutoka serikalini.

Mradi wa Changamoto za Millenia Tanzania (*MCA-T*)
Mhe. Spika, idara inashiriki katika kutekeleza mradi wa Changamoto za Millenia Tanzania kwa upande wa tathmini za kimazingira. Mradi huu unahusika na kuweka njia mpya ya umeme kutoka Ubungo (Tanzania Bara) hadi Mtoni (Unguja) kupitia chini ya bahari kwa kutokea Ras Kiromoni hadi Fumba. Jukumu la idara ni kuhakikisha kuwa mradi unatekelezwa bila ya kuathiri mazingira ya baharini na nchi kavu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, mradi huu ulitengewa jumla ya Dola za Kimarekani 96,350 kutoka *MCA-T* na shilingi 15,0000,000/- kutoka serikalini na hadi kufikia mwezi wa Aprili 2010, jumla ya Dola za Kimarekani 44,000 (45.7%) kutoka *MCA-T* na shilingi 3,000,000/- (20%) kutoka serikalini zilitumika. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, mradi huu unategemewa kupata jumla ya Dola za Kimarekani 52,350 kutoka *MCA-T* na shilingi 20,000,000/- kutoka serikalini.

Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani kwa Nchi za Magharibi ya Bahari ya Hindi (*ReCoMap*)

Mhe. Spika, mradi huu una lengo la kutoa elimu kwa jamii ya ukanda wa pwani juu ya kuhifadhi rasilimali za ukanda huo. Miongoni mwa kazi zinazotekelezwa na mradi huu ni pamoja na upandaji wa mikoko, ufugaji wa samaki, kaa, kombe na nyuki, usafi wa mazingira ya fukwe, kuhamasisha wanafunzi na wakulima wa mwani na utunzaji wa mazingira.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, mradi huu ulitengewa jumla ya Euro 20,000 kutoka EU na shilingi 10,000,000/- kutoka serikalini na hadi kufikia mwezi wa Aprili 2010, jumla ya Euro 20,000 (asilimia 100) kutoka EU na shilingi 3,000,000/- (asilimia 30) kutoka serikalini zilitumika. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, mradi huu unategemewa kupata Euro 25,000 kutoka EU na shilingi 10,000,000/- kutoka serikalini.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2010 idara imepatiwa jumla ya shilingi 101,527,490/- sawa na asilimia 73.4 ya makadirio ya mwaka 2009/2010. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011 idara inaombewa jumla ya shilingi 199,803,000/- kutoka serikalini.

IDARA YA VYAMA VYA USHIRIKA

Mhe. Spika, idara hii ina jukumu la kuendeleza Vyama vya Ushirika kwa kuvisajili, kutoa elimu na kutoa huduma za ukaguzi wa mahesabu pamoja na kusaidia kutatua migogoro inayotokea katika vyama hivyo**.**

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2009/2010

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

- Idara kwa kushirikiana na miradi ya wizara (*MACEMP*, *PADEP*, *ASSP*) imesajili jumla ya vyama vipya vya ushirika 366 (Unguja 226 na Pemba 140). **Kiambatisho Na. 14;**
- Rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Ushirika imekamilika na tayari imewasilishwa kwa washirika mbali mbali kwa maoni na ushauri;

- Jumla ya vyama 242 vimepatiwa mafunzo juu ya uanzishaji na uendeshaji wa Vyama vya Akiba na Mikopo na vyama vyengine vya Uzalishaji. Mafunzo hayo yaliwashirikisha wanaushirika 19,725, (Unguja 12,525 na Pemba 7,200); na

- Vyama vya ushirika 93 vilifanyiwa ukaguzi (Unguja 63 na Pemba 30), kati ya vyama hivyo, 29 vimechunguzwa hesabu zao

na 64 vimefanyiwa ukaguzi wa kawaida na kupewa ushauri wa kitaalamu.

MALENGO YA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 idara inalenga kutekeleza yafuatayo:-

- Kusajili vyama vya ushirika 150 vya miradi mbali mbali ya kiuchumi, mkazo zaidi ukiwekwa katika uanzishaji na uimarishaji wa *SACCOS*;

- Kukagua vyama vya ushirika 2,000 vilivyo hai na kuvipatia ushauri wa kitaalamu Unguja na Pemba,
- Kufanya uchunguzi wa vyama vyote vya ushirika vilivyokufa na kuvifuta rasmi;

- Kutoa mafunzo kwa vyama 375 vilivyosajiliwa kwa Unguja na Pemba;

- Kuimarisha uwezo wa utendaji wa idara kwa kuipatia nyenzo na vitendea kazi; na

- Kuanza matayarisho ya kuanzisha taasisi ya ukaguzi itakayojitegemea baada ya kukamilika marekebisho ya Sheria mpya ya Vyama vya Ushirika.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2010 idara imepatiwa jumla ya shilingi 122,870,764/- sawa na asilimia 73.3 ya makadirio ya mwaka 2009/2010. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011 idara inaombewa jumla ya shilingi 171,840,000/- kutoka serikalini.

KARAKANA YA MATREKTA

Mhe. Spika, Karakana ya Matrekta inatoa huduma mbali mbali za kiufundi ikiwa pamoja na kutengeneza matrekta, gari pamoja na kufanya kazi za uchongaji na uchomaji.

UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2009/2010

Mhe. Spika, katika kipindi kilichomalizikia Aprili 2010, Karakana ya Matrekta imetekeleza malengo yafuatayo: -

- Imeyafanyia matengenezo makubwa na madogo matrekta ya Kamisheni ya Kilimo;

- Ilitoa huduma za uchongaji wa vifaa na vipuri mbali mbali kwa makampuni ya watu binafsi na taasisi za serikali pamoja na kazi za uchomaji wa *welding* na *gas;*

- Huduma za matengenezo ya gari za serikali na za watu binafsi ziliendelea kutolewa kibiashara;

- Mafunzo ya Amali (*Vocational Training*) yaliendelea kutolewa kwa vijana kutoka taasisi za serikali na watu binafsi. Pia wanafunzi wapya 25 waliandikishwa; na
- Karakana ilikusanya jumla ya shilingi 38,679,005.00/- sawa na asilimia 77 ya lengo na kutumia jumla ya shilingi 33,635,917.00/- sawa na asilimia 70.67 ya lengo.

MALENGO YA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, karakana inalenga kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Kuyafanyia matengenezo makubwa na madogo matrekta ya Kamisheni ya Kilimo pamoja na kutoa huduma kwa matrekta ya taasisi za watu binafsi;

- Kutoa huduma za uchongaji wa vifaa na vipuri mbali mbali kwa makampuni ya watu binafsi na taasisi za serikali, pamoja na kufanya kazi za *welding* na *gas* na kutengeneza vifaa;

- Kuendelea kutoa huduma za matengenezo ya gari za serikali na za watu binafsi;

- Kuendelea kutoa mafunzo ya amali (*Vocational Training*) kwa vijana kutoka taasisi za serikali na watu binafsi;

- Kutoa huduma za ukulima kwa matreta kibiashara; na

- Kukusanya jumla ya shilingi 48,670,000.00/- na kutumia jumla ya shilingi 45,650,800.00/-.

AFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika, Afisi Kuu Pemba ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa kazi zote za wizara kwa upande wa Pemba kwa kushirikiana na idara tofauti

ziliomo katika wizara hii. Kwa mwaka 2009/2010, kazi zilizotekelezwa na Afisi Kuu Pemba ni miongoni mwa kazi zilizokwishwa elezwa chini ya idara zote ziliomo katika wizara hii.

Mhe. Spika, kwa kutekeleza hayo kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Afisi Kuu Pemba ilipangiwa kutumia jumla ya shilingi 1,425,506,000/- na hadi kufikia mwezi Aprili, 2010, jumla ya shilingi 1,255,182,646/- zilikwishatolewa na serikali, sawa na asilimia 88.05 ya lengo. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Afisi Kuu Pemba imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 1,593,588,000/-.

MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2009/2010

Makusanyo ya Mapato 2009/2010

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, wizara ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,429,900,000/- kutoka vyanzo mbali mbali vya mapato. Hadi kufikia Aprili, 2010 wizara imekusanya jumla ya shilingi 469,578,270/- sawa na asilimia 32.84 ya makadirio. Hadi kufikia Juni, 2010 wizara inakadiria kukusanya jumla ya shilingi 566,981,670/- na kufanya makusanyo yote kwa ujumla kufikia shilingi 1,036,559,940/-. Hii ni sawa na asilimia 72 ya lengo (***Kiambatisho 12).***

Matumizi ya Fedha 2009/2010

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara ya Kilimo Mifugo na Mazingira iliidhinishiwa jumla ya shilingi 26,559,663,000/- ambapo shilingi 6,803,300,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, na shilingi 19,756,363,000/- kwa kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, shilingi 1,650,000,000/- zilikuwa mchango wa serikali na shilingi 18,106,363,000/- zilikuwa mchango wa wahisani.

Mhe. Spika, kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo hadi kufikia Aprili, 2010 jumla ya shilingi 1,281,253,000/- ikiwa ni sawa na asilimia 77.65 ya fedha zilizoombwa ikiwa ni mchango wa serikali ***(Kiambatisho 13)***. Kwa upande wa mchango wa wahisani hadi kufikia Aprili, 2010 wizara imepokea jumla ya shilingi 14,032,849,483/- ambazo ni sawa na ailimia 77.5.

Kuanzia Julai 2009 hadi Aprili, 2010, kwa kazi za kawaida wizara imepata shilingi 5,769,963,341/- ambayo ni sawa na asilimia 84.81 ya fedha zilizoombwa. (***Kiambatisho 14).***

MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA 2010/2011

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira inakadiriwa kukusanya mapato ya shilingi 1,293,774,000/-. Aidha, wizara kwa mwaka wa 2010/2011 inakadiriwa kutumia shilingi27,374,817,000/-. Shilingi 19,619,817,000/- ni kwa ajili ya kutekeleza miradi 17 ya maendeleo. Kati ya hizo shilingi 2,110,000,000/- ni mchango wa serikali na shilingi 17,509,817,000/- ni fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kazi za kawaida, wizara inatarajia kutumia shilingi 7,755,000,000.00/-

SHUKRANI

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuzishukuru serikali za nchi zifuatazo:- Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Egypt, China, Jamhuri ya Korea, Japan, Iran, Israel, Finland, Norway, Uholanzi, Austria, USA, UK. Aidha, napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo wakiwemo *FAO*, Benki ya Dunia, *IFAD*, *ADB*, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *KOICA*, *JICA*, *USAID*, *UNDP*, *WSPA*, *WFP*, *IAEA*, *WCS*, *GEF*, *ACTION AID*, *GLOBAL FUND*, *IDA*, *UNICEF*, *DANIDA*, Pia tunazishukuru Jumuia za *EAC*, *EU*, *SADC* pamoja na Wizara za SMZ na taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali zinazosaidia kuleta maendeleo ya Sekta ya Kilimo.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii, kuwashukuru sana wataalamu na wafanyakazi wote wa Wizara Unguja na Pemba kwa kazi zao nzuri na zenye ufanisi wa hali ya juu. Vile vile, nawapongeza Wakuu wa Mikoa, wakulima, wafugaji, wavuvi, wakulima wa mwani, wanamazingira na wanaushirika wote kwa kazi zao nzuri za kuleta maendeleo katika Sekta ya Kilimo. Aidha, navipongeza vyombo vyote vya habari kwa utoaji wa habari za Sekta ya Kilimo.

HITIMISHO

Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waipokee na kuijadili bajeti ya wizara yangu na watupe ushauri na maoni yao juu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo kwa manufaa ya wakulima na taifa kwa ujumla. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 27,374,817,000/- kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kwa mwaka 2010/2011. Kati ya fedha hizo, shilingi 7,755,000,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 19,619,817,000/- ni kwa ajili ya matumizi kwa kazi za miradi ya maendeleo. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mazao/ Mwaka	**2005**	**2006**	**2007**	**2008**	**2009**	**JUMLA**
Mahindi	1,419	3,927	1,931	1,920	2,011.75	11,208.75
Mtama	459	409	794	610	453.2	2,725.2
Mpunga	15,935	24,730	20,038	20,857	26,962.5	108,522.5

					0	
Muhogo	102,886	190,266	187,213	153,050	195,546.72	828,961.7
Ndizi	22,984	88,438	93,641	100,873	90,420.85	305,936
Viazi Vitamu	13,211	63,949	45,620	55,294	53,587.50	178,074
Viazi Vikuu	2,394	5,100	8,192	3,516	11,372.50	19,202
Njugu Nyasa	302	1,800	76	465	320.43	2,643

KIAMBATISHO Na. 1. TAKWIMU ZA UZALISHAJI WA MAZAO KWA TANI MWAKA 2008/2009

	2005	**2006**	**2007**	**2008**	**2009**	**JUMLA**
	1,419	3,927	1,931	1,920	2,011.75	11,208.75
	459	409	794	610	453.2	2,725.2
	15,935	24,730	20,038	20,857	26,962.50	108,522.5
	102,886	190,266	187,213	153,050	195,546.72	828,961.7
	22,984	88,438	93,641	100,873	90,420.85	305,936
	13,211	63,949	45,620	55,294		178,074

					53,587.50	
	2,394	5,100	8,192	3,516	11,372.50	19,202
	302	1,800	76	465	320.43	2,643

KIAMBATISHO NA. 2 MAFUNZO KWA WAFANYAKAZI

		JINSIA		
Nam	**AINA YA MAFUNZO**	**MUME**	**MKE**	**JUMLA**
1	Shahada ya Pili (MSc)	9	4	13
2	Shahada ya Kwanza (Bsc)	18	15	33
3	Stashahada (PGd)	3	1	4
4	Astashahada (Diploma)	18	30	48
5	Cheti	11	18	29
	JUMLA	**59**	**68**	**127**

N.B. Jumla ya wafanyakazi 103 wamepatiwa nafasi za masomo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi

KIAMBATISHO NA. 3. PROGRAMU YA KUENDELEZA HUDUMA ZA KILIMO (ASSP)

Gharama: USD 5.9 millioni
Wachangiaji: SMZ 22%, IFAD 77.1 %, Walengwa 0.7%
Lengo Kuu: Kuinua hali ya maisha ya wakulima kwa kuongeza uzalishaji wenye tija, kuongeza kipato,uhakika wa chakula na kupunguza umaskini

Vipengele vya Programu
(1)Kuwawezesha wakulima (2) Kutoa huduma za kilimo (3) Uratibu na Uendeshaji wa Programu

Bajeti ya mwaka 2009/2010
Jumla ya Tshs. 1,591,502,195, SMZ Tshs. 360,000,000: IFAD Tshs. 1,220,361,680, na Walengwa Tshs. 11,140,515.

Utekelezaji wa Malengo 2009/2010
Vikundi 216 vya skuli za wakulima viliendelea kupewa taaluma ya uzalishaji, pamoja na vikundi 10 vilivyoibuka nje ya skuli za wakulima
Ziara za kimafunzo zilifanyika Pemba ambapo skuli ya wakulima wa muhugo kutoka Kilombero (Kaskazini B) walitembelea wenzao huko Pemba ili kujifunza na kubadilishana mawazo juu ya ukulima wa muhogo.

Programu zimeendelea kusaidia shughuli za utafiti katika: kudhibiti nzi wa embe kwa kutumia dawa ya kivutio iliotengezwa na wakulima wenyewe. Aidha wakulima hao wameweza kugundua sumu inayoweza kuwauwa nzi baada kukamatwa ambayo inaendelea kufanyiwa majaribio kwa msaada wa programu; kuhifadhi mbegu za muhogo na kutilia mkazo kwenye viazi vikuu na viazi vidogo.

Jumla ya wakulima 20 walipelekwa Dodoma katika maonesho ya nane nane kwa madhumuni ya kujifunza na kubadilishana mawazo na wakulima wenzao wa Tanzania Bara.

Bajeti ya mwaka 2010/2011: Programu inatarajia kupata kutoka kwa IFAD US Dola 664,845.48, TSh. 200,000,000 kutoka SMZ na Tshs. 8,985,516 kutoka kwa Walengwa.

Malengo ya Mwaka 2010/2011
Kuendelea kuvipatia elimu vikundi vya skuli za wakulima
Kuviendeleza vikundi ambavyo vimeibuka nje ya skuli za wakulima
Kuandaa ziara za kimafunzo ndani ya Zanzibar na Tanzania Bara
Kuimarisha shughuli za utafiti na elimu kwa wakulima
Kujenga bweni la wanafunzi katika Chuo Cha Kilimo Kizimbani
Kuendeleza uzalishaji mbegu bora za mpunga kupitia skuli za wakulima kwa mashirikiano na Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe.

KIAMBATISHO NA. 4 PROGRAMU YA KUENDELEZA SEKTA YA MIFUGO (ASDP-L)
Gharama za mradi: USD 3.76 millioni

Wachangiaji: SMZ (6.1%), IFAD (93 %,) WALENGWA (0.9%)
Lengo Kuu: Kupunguza umasikini, kuongeza uhakika wa chakula, kuongeza kipato cha watu masikini wanaotegemea mifugo katika maisha yao.

Vipengele vya Programu
Kuwawezesha wafugaji (2) kusaidia maendeleo ya sekta ya mifugo, (3) Mijadala ya Sera na marekebisho ya Sheria, (4) Uratibu wa Programu
Bajeti ya mwaka 2009/2010
Jumla Tshs., 1,613,970,657 (IFAD Tshs. 1,499,444,939, SMS Tshs. 100,000,000, walengwa Tshs. 14,525,736)

Utekelezaji 2009/2010
Vikundi 144 vya skuli za wafugaji viliendelea kupewa taaluma ya ufugaji, pamoja na vikundi 10 vilivyoibuka nje ya skuli za wafugaji.

Kutambua huduma zinazohitajika ili kuwawezesha wafugaji kuongeza uzalishaji na kuzalisha kibiashara na utafiti wa mfumo wa uzalishaji wa mifugo umekamilika.

Ukarabati wa vituo na maabara za mifugo umo katika taratibu za manunuzi.
Wafugaji wa ng'ombe wa maziwa kutoka vikundi viwili Unguja na kimoja Pemba walipata fursa kutembelea wafugaji wenzao wa Dar-es-Salaam na Tanga ili kuangalia jinsi gani wafugaji wenzao wanakabiliana na tatizo la uhifadhi wa maziwa na uwezekano wa kununua mashine za kuhifadhia na kusindika maziwa na hatimae kupata soko.

Wafugaji 20 walipatiwa ziara katika maonesho ya wakulima yaliyofanyika Dodoma.

Bajeti ya mwaka 2010/2011: Jumla Programu inatarajia kupata kutoka kwa IFAD US Dola 725,777.67, TSh. 95,000,000 kutoka SMZ na Tshs. 13,072,540 kutoka kwa Walengwa.
Malengo ya mwaka 2010/2011
Kuendelea kutoa taaluma kwa vikundi vya skuli za wafugaji pamoja na zilizoibuka zenyewe.
Kutambua huduma zinazohitajika ili kuwawezesha wafugaji kuongeza uzalishaji na kuzalisha kibiashara
Kununua chanjo ya mahepe na kutoa chanjo katika Shehia zote Unguja na Pemba.
Kuwapa wafugaji ziara za kimafunzo
Kununua mitambo 4 ya kusindika maziwa
Kuaanda warsha zinazohusiana na taaluma ya masoko katika wilaya 9.

Kuviwezesha vituo vya mafunzo (learning sites) za kuku, mbuzi na Ng'ombe.
Kuandaa mpango mkakati wa sekta ndogo ya maendeleo ya mifugo na warsha mbali mbali za wadau.

KIAMBATISHO Na. 5. PROGRAMU YA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE

Gharama: USD 15 million katika awamu ya miaka mitano ya mwanzo
Wachangiaji: SMZ, *FAO, UNDP*, Serikali ya Ujerumani na Washirika wengine wa Maendeleo
Lengo Kuu:

Lengo kuu la Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe ni kuchangia katika hatua za kitaifa za kupunguza umasikini wa chakula na kipato, kukabiliana na hali ya kutokuwa na uhakika wa chakula na lishe katika ngazi za taifa, jamii na kaya na kushajiisha ushiriki wa jamii katika hatua za kujiongezea kipato, kuondoa njaa na kufikia hali ya kila mtu kuwa na haki ya kula na kishiba.

Gharama mwaka 2009/2010
Programu iliombewa Sh. 160,000,000 kutoka SMZ na ilitarajia kupata USD 146,000 kutoka UN-JP5. Hadi kufikia April, 2010 fedha zilizopatikana ni kutoka SMZ Sh. 157,208,000.00, Fedha za JP5 hazikupatikana hadi mwishoni mwa Aprili 2010.

Utekelezaji 2009/2010
Taratibu za uanzishaji wa ofisi ndogo ya programu Pemba zimekamilika na ofisi itafunguliwa sambamba na uzinduzi wa Mradi wa kujenga uwezo wa Wilaya kutayarisha mipango ya Maendeleo unaofadhiliwa na Serikali ya Ujerumani.

Hatua zimechukuliwa kuweka muundo wa usimamizi wa kazi za programu katika ngazi mbali mbali za utekelezaji. Kamati ya Uongozi ngazi ya Taifa imezinduliwa rasmi na tayari imeanza kazi kwa kusimamia utayarishaji wa Sera ya Masoko ya Bidhaa za Kilimo na Mswada wa Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe.

Rasimu ya Mswada wa Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe imekamilika na hivi sasa inasubiri kuwasilishwa rasmi serikalini kwa ajili ya kupitishwa na kuwa sheria kamili.

Kazi za kujenga uwezo wa Wilaya kuandaa mipango ya maendeleo

(District development plans) imeanza kwa kuteuwa timu ya wakufunzi ya maofisa kutoka Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira, Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala bora na Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ. Aidha mafunzo ya awali kwa watendaji wa Wilaya mbili teule yamefanyika kwa watendaji 20 kwa kila wilaya za Chake Chake Pemba na Kusini Unguja.

Kazi za kuandaa na kuchapisha ripoti ya kila mwaka ya mfumo wa upatikanaji na matumizi ya chakula (Food Balance Sheet Report) imekamilika; ripoti ya kwanza ya Food Balance Sheet ya Zanzibar kwa mwaka 2007 imekamilika na imezinduliwa rasmi. Aidha, ripoti ya mwaka 2008 imo katika hatua za mwisho za utayarishaji. Sambamba na ripoti hizi, programu imekamilisha maandilizi ya utoaji wa dondoo za kisera (Policy briefs) ambazo zitaelekeza hatua za kuchukuliwa na Serikali na wadau wengine katika kukabiliana na hali tete ya uhakika wa chakula nchini. Dondoo ya mwanzo za kisera imezinduliwa rasmi mwezi mei 2010.
Rasimu ya Sera ya Masoko ya Bidhaa ya Kilimo imekamilika na hivi sasa timu ya uandaaji iko katika hatua za mwisho za kukamisha mpango wa utekelezaji wa sera hiyo.

Kazi za kuhamasisha uelewa wa Sera na Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe zimeendelezwa kwa kuchapisha vitabu vya Sera na programu pamoja na vipeperushi na kuvisambaza katika taasisi zote za Serikali katika ngazi za Taifa, Mikoa na Wilaya

Ripoti ya kwanza ya mfumo wa upatikanaji na matumizi ya chakula *(Food balance Sheet)* ya Z Zanzibar kwa mwaka 2007 imekamilika na ilizinduliwa rasmi; na ripoti ya mwaka 2008 imo katika hatua za mwisho za utayarishaji.

Gharama mwaka 2010/2011

Programu inatarajia kupata Sh. 200,000,000 kutoka SMZ, US$ 50,000 kutoka Serikali ya Ujerumani na US$ 102,000 kutoka JP5

Malengo ya mwaka 2010/2011

Kuendeleza kazi za uhakika wa chakula na lishe kwa kuimarisha utendaji na kusimamia uundwaji wa mfumo wa uratibu katika ngazi za kitaifa na Wilaya kwa mujibu wa sheria.
Kuendeleza uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora ikiwa ni mkakati wa kuongeza uzalishaji wa ndani na tija kwa wakulima. Malengo yafuatayo yamepangwa kwa mwaka 2010/2011:-

Kuendelea kujenga uwezo wa uzalishaji mbegu bora kupitia skuli za wakulima na mashamba ya mfano;
Kuhamasisha wakulima juu ya utumiaji wa mbegu bora;
Kuendeleza utafiti wa mbegu bora mama kwa zao la mpunga;
Kuendeleza ukuzaji wa mbegu mama kwa ajili ya kusambaza katika vikundi vya uzalishaji mbegu;
Kujenga uwezo na kuandaa mipango ya maendeleo ya wilaya teule inayozingatia utekelezaji wa sera ya uhakika wa chakula na lishe na haki ya kila mtu kupata chakula. Aidha, kuunda kamati za kuratibu masuala ya uhakika wa chakula na lishe katika ngazi za shehia.; na
Kuendeleza kampeni za utoaji wa elimu ya lishe katika ngazi za taifa, wilaya na kaya,

KIAMBATISHO Na. 6 MRADI WA USARIFU WA MAZAO YA KILIMO

Muda wa Mradi: Miaka mitatu, (Julai 2009/Juni 2012**)**
Gharama/Wachangiaji.: KOICA: US $ 2,300 milioni 2. SMZ US $ 0.400 milioni

Lengo kuu: Kujenga uwezo wa wakulima juu ya usarifu wa mazao na ujasiriamali pamoja na kutoa huduma za udhibiti wa ubora kwa bidhaa zinazozalishwa kwa lengo la kuongeza ajira na kipato kwa wazalishaji.

Gharama kwa mwaka 2009/2010: Shs. 170,000,000 SMZ

Utekelezaji 2009/2010:-

- Matengenezo ya kisima ambacho kinachopeleka maji katika kituo yamekamilika na uchunguzi wa maji yanayotarajiwa kutumika kituoni yamefanyika;
- Maandalizi ya uanzishwaji wa mradi yamekamilika ikiwa ni pamoja na : kusafisha eneo la ujenzi wa kituo;
- Tayari ununuzi wa baadhi ya vifaa vya usarifu wa mazao pamoja na vifaa vya maabara umefanyika;
- Tayari michoro/ramani ya majengo na kituo cha usarifu wa mazao pamoja na maabara ya uchunguzi wa vyakula imekamilika;
- Wakulima 60 tayari wamepata mafunzo ya usarifu wa mazao na ujasiri amali;
- Ujenzi wa kituo cha usarifu wa mazao tayari umekwishaanza; na
- Miundombinu ya maji katika eneo la ujenzi tayari imeshakamilika

Gharama kwa mwaka 2010/2011: US$ 1 milioni – KOICA na SMZ Sh. 190,000,000

Malengo ya mwaka 2010/2011

- Ununuzi na ufungaji wa transforma mpya;
- Kutoa mafunzo kwa wadau 100 (wajasiriamali) pamoja na kuandaa ziara za kimafunzo kwa maafisa wa mradi na wazalishaji;
- Kufunga vifaa vya usarifu wa mazao pamoja na vifaa vya maabara;
- Kutoa huduma za udhibiti wa ubora kwa mazao yaliyosarifiwa; na
- Kuandaa miradi mipya itakayosaidia kutanua wigo (scope) wa mradi uliopo sasa.

KIAMBATISHO Na. 7 MRADI SHIRIKISHI WA MAENDELEO YA KILIMO NA UWEZESHAJI (PADEP)

MRADI WA PADEP

Gharama: US $ 9.605 milioni
Wachangiaji: 1. IDA: US $ 7.942 milioni 2. SMZ na Walengwa: US $ 1.663 milioni

Lengo kuu: Kujengea wakulima uwezo wa kitaaluma ili waweze kutambua matatizo yao na kuibua miradi yao kwa lengo la kuongeza uzalishaji na tija na kushajiisha sekta binafsi kushiriki katika kutoa huduma za kilimo.

Gharama kwa mwaka 2009/2010: : Sh. 3,746,458,000 (Benki ya Dunia Sh. 3,646,458,000 na SMZ Sh. 100,000,000).

Utekelezaji 2009/2010

- Jumla ya Sh. 3.3 bilioni zimepelekwa kwa wanajamii kwa ajili ya kutekeleza miradi yao ya jamii na vikundi vya wakulima sawa na asilimia 143 ya lengo;
- Sh. 334.7 milioni sawa na asilimia 126 ya lengo zimepelekwa Wilayani kwa kutekeleza kazi za kujenga uwezo kwenye Wilaya mpya na kwa ajili ya kazi za ushauri na ufuatilaji kwa zile Wilaya za mwanzoni;
- Kabrasha lenye kujumuisha kumbukumbu za uzoefu, changamoto na mafunzo yaliopatikana katika utekelezaji wa Mradi wa PADEP kwa matumizi ya baadae ya kusaidia maendeleo ya Sekta ya Kilimo limetayarishwa;
- Mradi umeendelea kusaidia mafunzo ya Maafisa Ugani katika Chuo cha Kilimo, Kizimbani;

- Ziara za mafunzo zimefanyika kwa wakulima 152 wa Unguja na Pemba kutembeleana, kujifunza na kubadilishana uzoefu. Aidha, wakulima 20 na Mabwanashamba 12 na Maafisa watano walihudhuria Maonyesho ya Kilimo Kitaifa (Nane Nane) huko Dodoma. Pia wakulima 20 wa Unguja na Pemba pamoja na maafisa watano wametembelea Bagamoyo kujifunza usarifu wa muhogo. Wakulima 24 wa Unguja na Pemba na Maafisa watatu wametembelea Arusha kujifunza usarifu wa maziwa na jinsi ya kuendesha kilimo cha mboga mboga kibiashara;
- Rasimu ya Ripoti ya Mwisho ya Utekelezaji wa Mradi (Implementation Completion Report) imetayarishwa; na
- Mafunzo ya kilimo biashara yametolewa kwa wanajamii 46, pia wanajamii 634 wa Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali na usarifu wa mazao ya kilimo na mifugo.

Gharama kwa mwaka 2010/2011: Sh. 166,000, 000 kutoka SMZ

Malengo ya mwaka 2010/2011

- Kuratibu na kusimamia Shughuli za Mradi; na
- Kuendelea kufuatilia maendeleo ya miradi ya wanajamii.

KIAMBATISHO NA. 8. MRADI WA MACEMP
JINA LA MRADI
MRADI WA USIMAMIZI WA MAZINGIRA YA BAHARI NA UKANDA WA PWANI

MUDA WA MRADI MIAKA SITA (2005 – 2011)

JUMLA YA GHARAMA
Shilingi bilioni 31.34 – Benki ya Dunia bilioni 25.194; Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani (GEF) bilioni 5.187 na Shirika la Maendeleo la Japan (JSDF) ni shilingi milioni 959

Lengo Kuu la Mradi wa MACEMP
Kupunguza Umasikini kwa wananchi waishio katika Ukanda wa Pwani na Taifa kwa Ujumla; na kuhifadhi Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani.

Maeneo ya Mradi

Wilaya zote 10 za Unguja na Pemba na Maeneo ya Bahari Tanzania.

Jumla USD 8,107,001.00 zimepangwa kutumika katika mwaka 2009/2010

Utekelezaji 2009/10

- Katika utaratibu wa kuongeza kasi ya kutoa miradi kwa jamii kwa Unguja na Pemba katika kipindi cha 2009/10 jumla ya miradi arubaini na nane (48) yenye thamani ya Tshs. 779,691,870.00 imepatiwa fedha kupitia utaratibu wa MACEMP/TASAF, miradi 22 yenye thamani ya Tshs. 410,022,640.00 ni ya Unguja na miradi 26 yenye thamani ya Tshs. 369,669,230.00 ni ya Pemba, jumla ya miradi 251 tayari imeshapatiwa fedha na kutekelezwa katika kipindi cha Mei, 2006 – Aprili, 2010, kati ya hiyo jumla ya miradi 137 ni kwa Pemba na 114 ni kwa Unguja .
- Mafunzo na vifaa mbali mbali kwa wakulima wa mwani wapatao 4,000 na vikundi 17 vya wavuvi yametolewa.

Jumla U$D 9,500,000.00 zimepangwa kutumika katika mwaka 2010/2011

Malengo ya Mwaka 2010/2011:

- Kuendelea na ziara za ufuatiliaji na tathmini miradi ya jamii kwa Unguja na Pemba, ambapo jumla ya miradi 251 imepatiwa fedha na kutekelezwa kwa utaratibu wa MACEMP/TASAF.
- Kuendelea kutoa taaluma kwa wakulima wa zao la mwani Unguja na Pemba na wavuvi wa ukanda wa Pwani kwa Unguja na Pemba katika kutekeleza Uvuvi na Ukulima wa Mwani Bora wenye faida kubwa na kukamilisha utafiti wa ukulima wa mwani wa Cotonii katika maji marefu.
- Kuanza kwa ujenzi wa afisi za Mamlaka ya Uvuvi wa bahari kuu Tanzania zitakazojengwa Fumba – Zanzibar.
- Kusimamia ujenzi wa majengo ya idara ya uvuvi hapo Maruhubi (Unguja) na Limbani (Pemba)
- Kuendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu yanayohusu mamlaka ya Uvuvi wa Bahari kuu Tanzania.

KIAMBATANISHO NA.9 PROGRAMU YA UDHIBITI WA KICHAA CHA MBWA

Maelezo Mafupi ya Mradi:
Programu hii imeanza Agosti 2005 ikiwa na madhumuni ya kuchanja mbwa na paka na kutoa huduma ya matibabu na kuwafunga uzazi. Wanyama kazi (punda na ng'ombe) kupatiwa matibabu dhidi ya maradhi mbali mbali.

Lengo Kuu:

- Kudhibiti na hatimaye kutokomeza Kichaa cha Mbwa katika mbwa kwa lengo la kutokomeza pia maambukizi ya kichaa cha mbwa kwa binadamu.
- Kutoa ushauri kwa wafugaji juu ya haki za wanyama na kudhibiti ukatili dhidi yao.

Bajeti ya mwaka 2009/2010: WSPA USD 92,82O, SMZ Tshs 25,000,000

Utekelezaji 2009/2010:

- Jumla ya Mbwa 741 na Paka 589 walifungwa uzazi na mbwa 9,983 walipatiwa dawa za minyoo.
- Jumla ya mbwa 13,230 waliogeshwa kwa kuwakinga na maradhi
- yanayotokana na Kupe.
- Jumla ya Ng'ombe 516 wa gari na Punda 555 walitibiwa kutokana
- na maradhi ya aina
  mbali mbali
- Jumla ya Mbwa 6,989 asilimia 34.94% walipata chanjo dhidi ya kichaa
- cha mbwa
- Jumla ya wafugaji 330 walipatiwa mafunzo ya umuhimu wa chanjo dhidi
- ya kichaa

cha mbwa na utunzaji bora wa mbwa na haki zake.

Bajeti ya mwaka 2010/2011:WSPA USD 97,461 na SMZ Tshs 65,000,000

Malengo ya mwaka 2010/2011:

- Kudhibiti maradhi ya kichaa cha mbwa na kuimarisha afya za mbwa 10,000 na paka 5,000 kwa kuwapatia huduma na matibabu ya kinga dhidi ya maradhi mbali mbali.
- Kutoa huduma za matibabu kwa wanyama kazi (Ng'ombe 650 na Punda 650).
- Kuchanja mbwa 10,000 dhidi ya maradhi ya kichaa cha mbwa.
- Kufunga uzazi kwa mbwa 1,000 na paka 700.
- Kutoa elimu kwa wafugaji mbwa 360 na wasiokuwa wafugaji mbwa 360 katika Wilaya zote za Unguja.
- Kutoa ushauri kwa Manispaa ili kutoa leseni za magari ya ngombe na punda kwa wafugaji na upatikanaji wa takwimu sahihi za wanyama ki-Wilaya.

KIAMBATISHO NA. 10 MRADI WA KUKABILIANA NA MAFUA YA NDEGE

MAELEZO MAFUPI YA MRADI

Mradi ulianza 2006/2007 kwa lengo la kuikinga Zanzibar na homa ya mafua makali ya ndege. Aidha, mradi ulianza baada ya kutayarishwa Mpango wa Kitaifa na kupata baraka zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mpango unatekelezwa katika Wilaya zote 10 za Zanzibar.

LENGO KUU:

Kuikinga Zanzibar dhidi ya mafua ya ndege na kuitayarisha kukabiliana nayo pindi yakiingia nchini

BAJETI YA MWAKA 2009/2010:

Jumla TShs 385 million; SPINAP TSHS 300 million; UNICEF Tshs 35 million; SMZ Tshs 50 million

UTEKELEZAJI 2009/2010

- Taaluma za mafua ya ndege kwa walimu na wanafunzi katika Wilaya 2 za Magharibi- Unguja na Mkoani- Pemba kwa kupitia 'School clubs'. Jumla ya wanafunzi na waalimu 1,760 walipata taaluma
- Kusambaza vipeperushi na mbango ili kuelimisha jamii katika Wilaya zote Unguja na Pemba. Jumla ya vipeperushi 9,500 na mabango 3,000 yalisambazwa.
- Taaluma ilitolewa kwa wafanyakazi wa Mifugo na Wizara ya Afya kuhusu kushughulikia wagonjwa, uchunguzi wa maabara, usafi , sheria na taaluma ya maradhi ya mafua makali.
- Kuanzishwa na kupewa taaluma kwa vikosi viwili maalum (Rapid Response Teams) vya kushughulikia mafua ya ndege- kimoja Unguja na chengine Pemba.
- Kuanzisha na kuelimisha Kamati za Wilaya za Mafua ya ndege katika Wilaya zote 10 Unguja na Pemba.
- Uchunguzi wa maradhi ya mafua ya nguruwe kwa binaadamu ulifanyika katika hospitali ya Mnazimmoja, Kivunge na Chake chake na Micheweni na katika mashamba ya Mifugo- Mchui, Kitumba na Kizimbani.
- Mafunzo ya Maabara yalitolewa kwa wafanyakazi wanane huko Tanzania bara (4 kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na 4 kutoka Idara ya Mifugo).
- Kulifanyika vikao vya Kamati za Wataalamu (Technical Committee) na 'Task Force' za mafua ya ndege

BAJETI YA MWAKA 2010/2011

SPINAP TSHS 132 Million; UNICEF 175.8 million; SMZ TSHS 67 million

MALENGO YA MWAKA 2010/2011

- Kununua vifaa vya maabara
- Kufanya mapitio ya Mpango wa Mafua ya Ndege wa mwaka 2006
- Kutengeza Mpango wa kukabiliana na Homa ya Bonde la Ufa
- Kuendelea kutoa taaluma ya mafua makali kwa jamii na wafanyakazi

KIAMBATISHO Na. 11: MRADI WA MPANGO WA TAIFA WA UIMARISHAJI MIKARAFUU

Jina la Mradi	Mradi wa Uimarishaji Mikarafuu
Muda wa mradi Wa kuendelea	
Wachangiaji SMZ na Shirika la ZSTC	
Lengo kuu Kuongeza pato la wananchi kwa lengo la kupunguza umaskini	
Malengo maalum • Kufufua na kuendeleza mashamba ya mikarafuu kwa kupanda miche mipya katika maeneo yaliowazi. • Kufanya utafiti wa zao hilo na mazao mengine ya biashara.	
Maeneo ya Mradi Wilaya tano za Unguja na zote Pemba.	
Vipengele vya Mradi • Kuotesha miche ya mikarafuu kwa wingi ili kutosheleza mahitaji ya wakulima. • Kutoa elimu ya kilimo mchanganyiko cha karafuu na mazao ya viungo.	
Gharama kwa mwaka 2009/2010 Tshs 60,000,000/- kutoka SMZ, zilizotolewa ni 35,000,000/- sawa na asilimia 58.33%	

Malengo ya mwaka 2009/2010

- Kuzalisha 300,000 ya mikarafuu.
- Kutoa mafunzo ya kilimo mchanganyiko ya mikarafuu na mazao mengine ya viungo.
- Kuanza matayarisho ya kuhesabu mikarafuu.
- Kutoa mafunzo ya uchumaji na ukaushaji wa zao la karafuu.

Utekelezaji 2009/2010

- Miche 185,000 ya mikarafu imeoteshwa sawa na asilimia 62 ya lengo
- Mafunzo ya kilimo mchanganyiko cha mikarafuu na mazao mengine ya viungo yametolewa kwa wakulima 30 Mkoa wa kaskazini, 25 wilaya ya kati na Magharibi, Unguja na 35 Mkoa wa Kasikazini na 30 Mkoa wa Kusini, Pemba.

Gharama kwa mwaka 2010/2011 80,000.000/=

Malengo ya mwaka 2010/2011

- Kuzalisha miche 300,000 ya mikarafuu.
- Kutoa mafunzo ya kilimo bora cha mikarafuu, uvunaji na uwanikaji.
- Kufanya utafiti wa vifo vya mikarafuu midogo.
- Kuhamasisha wakulima kupanda mikarafuu na kuhudumia.
- Kuwajengea uwezo wananchi kuongeza uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na karafuu.

KIAMBATISHO Na. 13: TAARIFA ZA KAZI ZA MIRADI YA MAENDELEO JULAI HADI APRIL 2010

KASMA	MAELEZO	MAKADIRIO MWAKA 2009/2010 SMZ	FEDHA ZILIOTOLEWA JULY,09 - APR,10	SAWA NA ASILIMIA	MAKADIRIO YA 2010/2011 SMZ	MAKADIRIO 2010/2011 WAHISANI	JUMLA
61205	Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo - Mifugo	100,000,000.00	55,000,000	55.00	95,000,000	994,315,000.00	1,089,315,000
61225	Programu ya Kuimarisha Huduma Za Kilimo	360,000,000.00	195,000,000	54.17	200,000,000	914,162,000	1,114,162,000
61300	Programu ya Kuelimisha Wadau Wa Sekta ya Kilimo	30,000,000.00	20,000,000	66.67	40,000,000	-	40,000,000
61310	Mradi wa Uhakika Wa Chakula	160,000,000.00	157,208,070	98.26	200,000,000	208,240,000	408,240,000
61320	Mradi wa Kukuza Usarifu wa Mazao Ya Kilimo	170,000,000.00	167,000,000	98.24	190,000,000	1,370,000,000	1,560,000,000
61260	Mradi wa PADEP	100,000,000.00	95,000,000	95.00	166,000,000	-	166,000,0

							00
61206	Mradi wa Kichaa Cha Mbwa	25,000,000.00	15,000,000	60.00	65,000,000	123,300,000	188,300,000
61207	Maradi wa Upandishaji wa Ngo'mbe Kwa Sindano	40,000,000.00	31,500,000	78.75	147,000,000	-	147,000,000
61208	Kudhibiti Mafua ya Ndege	50,000,000.00	32,291,930	64.58	67,000,000	685,000,000	752,000,000
61240	Mradi wa Kuimarisha Mikarafuu	60,000,000.00	35,000,000	58.33	80,000,000	-	80,000,000
61252	Hifadhi ya Misitu ya Asili	-	-	-	-	2,831,835,000	2,831,835,000
61253	Uhifadhi wa Misitu ya Pwani	-	-	-	-	731,580,000	731,580,000
61270	Mradi wa Ghuba ya Minai	30,000,000.00	-	-	-	-	-
61290	Mradi wa MACEMP	100,000,000.00	75,000,000	75.00	350,000,000	9,500,000,000	9,850,000,000
61251	Programu ya Usimamizi wa Mazingira	40,000,000.00	25,000,000	62.50	50,000,000	14,385,000	64,385,000
61214	Programu ya Ushirika	25,000,000.00	18,500,000	74.00	40,000,000	-	40,000,000
61215	Mpango Mkuu wa Kilimo Cha Umwagiliaji Maji	180,000,000.00	180,000,000	100.00	200,000,000	-	200,000,000
61216	Mradi wa kilimo Cha kisasa cha Umawagiliaji Maji	180,000,000.00	179,753,000	99.86	220,000,000	137,000,000	357,000,000
	JUMLA	**1,650,000,000.00**	**1,281,253,000**	**77.65**	**2,110,000,000**	**17,509,817,000**	**19,619,817,000**

KIAMBATISHO NA. 14
MAKADIRIO YA MATUMIZI YA MWAKA 2009/2010 PAMOJA NA FEDHA ZILIZOTOLEWA JULAI, 2009 HADI APRIL, 2010 NA MAKADIRIO YA MWAKA 2010/2011
KAZI ZA KAWAIDA

KASMA	MAKADIRIO YA FEDHA MWAKA 2009/2010	FEDHA ZILIZOTOLEWA JULAI ,09 – APR, 2010	SAWA NA ASILIMIA %	MAKADIRIO YA MWAKA 2010/2011
03 PEMBA	1,425,506,000.00	1,255,182,646.00	88.05	1,593,588,000.00
04 IDARA YA MIPANGO NA SERA	664,114,000.00	592,464,639.00	89.21	936,965,000.00
05 KAMISHENI YA KILIMO, UTAFITI NA ELIMU KWA WAKULIMA	2,264,684,000.00	1,896,715,955.00	83.75	2,448,319,000.00
06 IDARA YA MAENDELEO YA MIFUGO	674,894,000.00	576,510,962.00	85.42	848,636,000.00
07 IDARA YA MAZAO YA BIASHARA NA MATUNDA/MISITU	806,444,000.00	694,808,853.00	86.16	919,177,000.00
08 IDARA YA UVUVI NA MAZAO YA BAHARINI	252,936,000.00	200,925,127.00	79.44	267,666,000.00
09 IDARA YA MAZINGIRA	138,424,000.00	101,527,490.00	73.35	199,803,000.00
10 IDARA YA VYAMA VYA USHIRIKA	167,786,000.00	122,870,764.00	73.23	171,840,000.00
11 IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI	328,512,000.00	282,493,905.00	85.99	369,006,000.00
12 CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI	80,000,000.00	46,463,000.00	58.08	
JUMLA	**6,803,300,000.00**	**5,769,963,341.00**	**84.81**	**7,755,000,000.00**

KIAMBATISHO NA. 15
VYAMA VYA USHIRIKA VYA MIRADI MBALI MBALI VILIVYOANDIKISHWA UNGUJA NA PEMBA (JULAI 09-APRIL 10)

Aina ya Mradi	Mjini	Magharibi	Kaska A	Kaska B	Kati	Kusini	Jumla Unguja	Mkoani	Chake	Wete	M/weni	Jumla Pemba	Jumla kuu
Saccos	1	4	0	0	0	0	**5**	1	1	1	3	**6**	**11**
Biashara	3	0	2	11	2	0	**18**	0	0		1	**1**	**19**
U/Mwani	0	0	0	0	0	1	**0**	1	0	1	0	**2**	**2**
Duka	0	0	1	1	1	1	**4**		0		1	**1**	**5**
Kazi za Mikono	0	1	1	0	0	2	**4**	0			0	**0**	**4**
Kilimo	0	3	14	32	3	38	**90**	30	6	7	15	**58**	**148**
Ufugaji	2	1	7	24	1	20	**55**	24	11	4	23	**62**	**117**
Uchongaji	0	0	2	3	0	0	**5**	0	0	0	0	**0**	**5**
U/Mazingira	0	0	0	0	0	0	**0**	1	0	0	3	**4**	**4**
Ushonaji	0	0	1	3	0	0	**4**	0	1	0	3	**4**	**8**
Upandaji Miti	0	0	1	0	0	4	**5**	0	0	0	1	**1**	**6**
Uvuvi	0	7	6	13	4	3	**33**	0	1	0	0	**1**	**34**
Utembezaji watalii	0	0	2	0	0	0	**2**	0	0	0	0	**0**	**2**
Jumla	**6**	**16**	**37**	**87**	**11**	**69**	**226**	**57**	**20**	**13**	**50**	**140**	**366**

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi): Mhe. Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake. Kwa kuendelea kutujaalia sisi sote kutumia neema yake ya uhai na uzima. Nitumie nafasi hii pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kabisa kutoa maoni ya kamati juu ya hoja iliyopo mbele yetu.

Mhe. Spika, naomba pia nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira kwa uwezo wake mkubwa wa kiutendaji kama ambavyo ametuwasilishia hotuba yake hii leo.

Pongezi hizi pia ziwaendee watendaji wake wote wanaoongozwa na Katibu Mkuu, Kamishna, Wakurugenzi na Wakuu wa vitengo mbali mbali vya wizara hii. Tunawapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutekeleza majukumu yao, wakati mwengine katika mazingira magumu ya upungufu wa nyezo na raslimali nyengine.

Mhe. Spika, katika shukrani zangu nisingependa hata kidogo kuwasahau wajumbe wangu wa kamati kwa kazi zao nzuri, mashirikiano waliyonipa, michango na mawazo yao kwa serikali kupitia wizara mbali mbali kamati hii ilimofanya kazi zake. Kazi na juhudi zao hizo zimetufikisha katika mafanikio makubwa hadi leo kwa wizara hii ikiwa ni kazi ya mwisho kwa awamu hii ya muda wa kamati vile vile na Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, tunaombeana kila la kheri kwa wale ambao wangependa kuendelea na kazi basi Mwenyezi Mungu awapokee dua yao hiyo, kwa wale ambao wataamua kupumzika basi Mwenyezi Mungu nao awape mapumziko yenye baraka na fanaka.

Naomba niwatambue wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Salmin Awadh Salmin	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Ali Abdalla Ali	-	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Assaa Othman Hamad	-	Mjumbe
4.	Mhe. Ashura Abeid Faraji	-	Mjumbe
5.	Mhe. Said Khelef Ali	-	Mjumbe
6.	Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	-	Mjumbe
7.	Mhe. Mwajuma Faki Mdachi	-	Mjumbe
8.	Mhe. Juma Duni Haji	-	Mjumbe
9.	Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	-	Mjumbe
10.	Mhe. Rashid Seif Suleiman	-	Mjumbe
11.	Ndg. Amour Moh'd Amour	-	Katibu
12.	Ndg. Maryam Hussein Rajab	-	Katibu

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ina majukumu makubwa ambayo yanagusa muenendo wa maisha ya wananchi wetu ya kila siku. Tunazo kauli nyingi zenye kuthibitisha umuhimu wa wizara hii. Kwa mfano, Kilimo ndio Uti wa Mgongo, Kilimo ndio Mkombozi wa Wanyonge na sasa tunayo kauli ya Kilimo Kwanza kwa wenzetu wa Tanzania Bara.

Mhe. Spika, wizara hii inajumuisha sekta nyingi na naomba nitoe maoni ya kamati kupitia sekta hizo kama ifuatavyo:-

SEKTA YA KILIMO

Mhe. Spika, tumekuwa tukisisitiza sana ukulima wa mpunga na kwa kweli mtazamo wa wananchi na serikali umekuwa ni kutumia nguvu nyingi katika aina hii ya kilimo. Yawezekena ni kwa sababu ya wananchi wetu wa visiwa hivi kupendelea sana kutumia mchele kama chakula chetu kikuu.

Serikali imepanga kuyaimarisha mabonde ya mpunga ya Bumbwisudi, Saninga, Kibokwa na Cheju, kwa ajili ya mpunga wa umwagiliaji maji na wizara imejitahidi kutengeneza miundombinu ili kufanikisha hilo.

Ni dhahiri eneo ambalo limepimwa la hekta 730 likifanyiwa kazi vizuri basi nafuu kidogo ya kupata chakula hasa cha mchele itaonekana. Tunaiomba kazi ya kuunganisha umeme kwenye mabonde ya Bumbwisudi na Cheju iendelee, ili hiyo azma tunayoidhamiria itimie.

Mhe. Spika, pamoja na aina hiyo ya kilimo cha mpunga wa umwagiliaji maji, lakini bado ipo haja kubwa ya kuimarisha kilimo cha mpunga wa kutegemea mvua. Ingawa kuna mabadiliko ya mienendo ya upatikanaji wa mvua na bado mabadiliko hayo hayajaleta tofauti kubwa kwani mvua za msimu zinapatikana, ni vyema elimu kwa wakulima ikatolewa, upatikanaji wa mbegu bora na mbolea kwa bei nafuu na vile vile kulimwa kwa matrekta tena kwa wakati.

Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Waziri ameliarifu Baraza lako tukufu kwamba wizara ina jumla ya matrekta 45 ikiwa ni sawa na asilimia 83 ya mahitaji ya zana hizo. Tunadhani matrekta hayo yakitunzwa na kutumiwa vizuri yanaweza kusaidia sana kwa matatizo ya wakulima wetu. Kwa hivyo, ni vizuri kuwa na ratiba inayokubalika ya kuanza kulima na hayo yote yafanywe kwa mashirikiano baina ya wizara na wakulima kupitia kamati zao za ukulima.

Mhe. Spika, pamoja na mapenzi yetu ya mpunga lakini ni vyema pia tukaamua kulima kwa wingi vilimo vyengine kama vile muhogo, ndizi, mbaazi, mtama na mazao mengine. Mazao haya yanaweza kupatikana kwa wingi hapa Zanzibar.

Hivi sasa Makunduchi kunazalishwa sana ndizi jambo ambalo halikuwepo siku za nyuma, ni dhahiri kwamba hata maeneo mengine kwa mazao mengine wakiamua kupitia utaalamu basi haya yanawezekana. Tunaiomba wizara kupitia kwako Mhe. Spika ifanye utafiti wa kutosha, ili tuweze kugundua ni ardhi ipi inaweza ikazalisha mazao yepi.

BIASHARA, MATUNDA NA MISITU

Mhe. Spika, sote tunaelewa faida ya kutunza rasilimali ya misitu, faida zake ni nyingi. Wizara imejitahidi kuweka maeneo ya uhifadhi wa misitu hiyo. Wao wanajukumu kubwa la kuitunza lakini kwa vyovyote vile hawatofanikiwa malengo yao bila ya mashirikiano ya kweli na wananchi na hasa wale wanaoishi karibu na maeneo hayo. Kamati inaomba wananchi wautambue umuhimu wa kuitunza rasilimali hii lakini pia wawe tayari kushirikiana na Wizara katika uhifadhi wake.

Mhe. Spika, ili tuwe na miti endelevu ikiwa ya misitu au ya matunda au ya biashara suala la uimarishaji wa vitalu vyetu ni muhimu . kwa kufanya hivyo tunaweza kuzalisha miche ya kutosha ambayo itasaidia kuendeleza mazao yetu.

Jengine ni suala la elimu kwa wakulima juu ya uoteshaji na uendelezaji wa miche hiyo. Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba karibu miche 1500,000 imetolewa kwa ajili ya kupandwa. Kwa mtazamo miche hiyo ni mingi kiasi kutolewa kwa mwaka, lakini swali linakuja je ni miche mingapi itakayohuika. hapa ndipo tunapozungumzia juu ya kuhitajika kwa elimu.

Mhe. Spika, tumezoea sana kuona kwamba karafuu ni zao pekee la biashara na ndio maana tunalikazania sana. Tunadhani umefika wakati wa kuyaangalia mazao mengine kama vile vanilla, hiliki na viungo vyenginevyo ili navyo visaidie pato la wakulima. Ni vyema Serikali ikatoa kila aina ya msaada kwa wale wakulima wanaoshajiishika na ukulima wa aina hii.

CHUO CHA KIZIMBANI

Mhe. Spika, tumekuwa tukisisitiza sana umuhimu wa elimu kwa wakulima ili kilimo chetu kiwe na tija. Chuo chetu cha Kizimbani kinaweza sana kutatua tatizo hilo. Kinahitaji kuimarishwa kwa kuwa na mitaala bora yenye kuendana na uhalisia wa mahitaji yetu. Kiendelee kupatiwa vifaa na nyenzo mbalimbali za mafunzo. Lakini pia kijenge mashirikiano na mahusiano mazuri na vyuo vyengine vya nje ya Zanzibar kama vile Sokoine *University of Agriculture* cha Morogoro na vyuo vyengine vya kilimo nje ya Tanzania.
Tunaamini kwamba suala la kubadilishana uzoefu wa kitaalamu kunaweza kusaidia sana maendeleo ya Chuo hiki.

SEKTA YA MIFUGO

Mhe. Spika, wakulima wengi hupenda kufuga, kwani wanaamini kuchanganya fani mbili hizi kuwa tija, kwani ni mambo yanayotegemeana. Pamoja na juhudi zinazooneshwa na wafugaji hao lakini mara nyingi huvunjwa moyo na uzalishaji wake, ama kwa mazao yanayotokana na mifugo hiyo au maradhi ya mara kwa mara yanayosumbua. Tunaomba Wizara kupitia miradi yake mbalimbali iweze kuwasaidia wafugaji wetu suala la uteuzi wa mbegu bora za mifugo na elimu ya kinga na maradhi yanayowasumbua mara kwa mara.

Mhe. Spika, kuwa na Karantini ni muhimu ili kuweza kuwahifadhi wanyama wapya wasiingize maradhi nchini mwetu. Kwa muda mrefu karantini ya Kisakasaka imekuwa ikitumika kwa madhumuni hayo. Eneo hilo limekuwa likivamiwa mara kwa mara na wanajamii na Serikali isipokuwa makini basi tutabaki na eneo dogo lisilotosheleza mahitaji yetu.

Tunaomba eneo hilo lipimwe, liwe na hatimiliki na lizungushiwe uzio kwa usalama wa kulihifadhi. Halikadhalika na ile Afisi iliyopo pale nayo ijengwe ionekana kweli ni Afisi ya Serikali. Kuhusu chinjio liliopo pale nalo bado halikidhi haja. Ni kongwe na utaratibu wake ni wa kizamani. Ni vyema Wizara ikaangalia tena uwezekano wa kuwa na chinjio la kileo lenye vifaa vya kisasa.

SEKTA YA UVUVI

Mhe. Spika, kwa maumbile ya visiwa vyetu ni kwamba tumezungukwa na bahari hatuna sababu tusiwe watumiaji wakubwa wa neema hii aliyetujaaliya Mwenyezi mungu katika kufaidika na rasilimali zilizokuwemo.

Mhe. Spika, Wizara kupitia mradi wa *MACEMP* imejitahidi sana kuwasaidia wananchi wetu katika uvunaji wa mazao hayo ya Baharini. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi na watendaji wake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mhe. Spika, Wavuvi wetu sasa wameelimika ni vyema waekezaji wazalendo waekeze katika sekta hii kwenye uvuvi wa Bahari kuu ili rasilimali iliyokuwepo nasi wenyewe tuweze kuivuna. Nina hakika wavuvi wetu wakiwa na nyenzo hizo wanaweza.

SEKTA YA MAZINGIRA

Mhe. Spika, neno mazingira kwa upeo wake ni neno kubwa na lenye maana pana lakini tafsiri haiendi mbali isipokuwa ni yale mambo yanayotuzunguka. Haya yanahitaji kutunzwa kwa kujenga mustakabali wa maisha yetu kwa sasa na kizazi kijacho.

Mhe. Spika, pamoja na juhudi kubwa za Serikali juu ya kuwa na miundo mbinu ya kuyalinda mazingira yetu lakini wananchi wachache wamekuwa wakirudisha nyuma juhudi hizo. Suala la ukataji miti hasa mikoko limekuwa likiendelea bila ya kufata taratibu na sheria zilizopo, magari ya ng'ombe yamekuwa yakichota mchanga katika maeneo mbalimbali na matumizi ya mifuko iliyokatazwa nayo yanaendelea tena bila ya kificho.

Mhe. Spika, bado kunahitajika nguvu za pamoja za kuweza kukabiliana na maangamizi hayo. Masheha na viongozi wengine wasaidiane sana ulinzi huu wa mazingira . lakini hili pia linamhusu kila mwananchi. Hata hivyo Wizara nayo inawajibu wa kusimamia vyema sheria zake ili wale wanaopatikana na makosa basi sheria zifate mkondo wake. Kama sheria zilizopo zinapunguza uwezo wao basi ni vyema waziwasilishe barazani kwa hatua za kufanya marekebisho zichukuliwe.

SEKTA YA VYAMA VYA USHIRIKA

Mhe. Spika, Vyama vya ushirika vimekuwa mkombozi mkubwa wa maisha ya wananchi wetu waliojikusanya pamoja kuunda hivi vyama vya ushirika. Wameshajiishika vya kutosha na hivi sasa vikundi vya ushirika ni vingi vilivyosajiliwa na vyengine vinasubiri kusajiliwa. Tatizo lililokuwepo ni uchache wa maafisa wanaoshughulikia uratibu wa vyama hivi kama vile wakaguzi wa mahesabu, maafisa elimu wa ushirika na wahudumu wa usajili wilayani. Lakini hata Afisi yenyewe haina jengo la kuridhisha. Wanafanyia kazi katika jengo bovu na la hatari kabisa.

Mhe. Spika, tunaiomba Wizara iangalie sana mahitaji hayo ili iweze kukidhi kiu ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, Baada ya maoni hayo ya Kamati, niwaombe sasa wajumbe wenzangu wa Baraza lako tukufu, wakubali na kuidhinisha makadirio ya Mapato na matumizi kwa mwaka 2010/2011, Tanzania Shilingi 7,755,000,000/= kwa matumizi ya kazi za kawaida za Wizara, Tanzania shilingi 19,619,817,000/= kwa kazi za maendeleo na kuyakubali mapendekezo ya makusanyo ya mapato ya Tanzania shilingi 1,293,774,000 ya Wizara.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Fedha na Uchumi tunaunga mkono hoja hiyo na vilevile kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni nasema pia naunga mkono hoja na nikiwataka Wajumbe wenzangu wamuunge mkono Mheshimiwa Waziri ili Wizara itekeleze majukumu yake.

Mhe. Spika, Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika, baada ya hotuba hii naomba sasa nitumie nafasi hii nikiwa kama Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Jimbo la Magomeni kuzungumzia jambo moja. Jambo ambalo ningependa kuzungumzia kwa Mhe. Waziri ni juu ya suala la uhifadhi wa wanyama kama ng'ombe sasa hivi vijana wetu wamekuwa wakiwatumia vibaya hasa wale wanaotumia ng'ombe kwa gari na kwa kazi zao za kila siku, ng'ombe ni wanyama lakini nao ni viumbe sasa kama serikali haiotowaonea huruma kwa kutumia sheria zake basi wanyama wale watakuwa katika hali ya hatari.

Mhe. Spika, sisi sote ni mashahidi tunaona jinsi wanyama wanavyoteseka wanabebeshwa mizigo mkubwa kinyume na uwezo wao na serikali inaona na inangalia, sisi wananchi kubwa kwetu ni kusononeka na kuona jinsi wanyama wale wanavyotesa. Mimi naamini sheria zipo lakini sheria ni sheria chombo hiki kimekuwa kikipisha sheria mbali mbali juu ya mambo mbali mbali lakini matokeo yake sheria zile hazitumiki au wahusiki hawazitumii.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri kwamba Wizara yake sasa ione umuhimu wa kuangalia wanyama wale, vijana wanaowatumia wanavuta bangi wamekuwa hawana huruma juu ya wanyama wale wanabebeshwa mizigo kinyume na uwezo wao, wanakula usiku usiku mchana kutwa wanabebeshwa mizigo na usiku ndio wamewekewa taimu yao ya kula.

Kwa hivyo mimi kilio changu ni juu ya wanyama na laiti kama sheria zimekuwa hazitoshelezi basi sheria zirekebishwe ili tuone na wale wanyama tunawahurumia kwa sababu sisi ni binaadamu na wale wanyama mwenyezi Mungu ametuletea sisi kwa ajili ya kitoweo, lakini na kutumia kwa ajili ya mambo mengine.

Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri suala la wanyama wanaotumikia wao wanaowatumikia waweze kuangaliwa kwa makini ili wasiendelee kuteseka.

Baada ya maelezo yangu hayo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni tunaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ahsante.

Mhe. Spika. Mhe. Mwenyekiti nakupongeza sana kwa mchango wako huo kwa sababu hili la wanyama na mimi limenigusa sana hawa wanyama wa ng'ombe na mbuzi ni hatari kabisa inanigusa mno pamoja na punda.

Mhe. Assaa Othman Hamad (Waziri Kivuli, Wizara ya Kilimo Mifugo na Mazingira): Mhe. Spika, Naomba kumshukuru Allah (S.W) muumba Mbingu na Ardhi na vilivyomo ndani yake! Kwa *REHEMA NA MAPENZI* makubwa kwetu kutujaalia uhai na uzima wa afya na kuweza kuendelea na shughuli za kuwatumikia wananchi wa Zanzibar yetu iliyojaa matumaini ya kuimarika kwa umoja, mshikamano na maelewano na hatimae kuifikia ile Zanzibar tuitakayo Inshaallah "Amina". Aidha nikushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kuniruhusu kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu maoni ya Kambi yangu ya Upinzani, halkadhalika nakushukuru kwa uongozi wako mahiri unaotuongoza sisi wajumbe wa Baraza lako tukufu kumudu vyema shughuli zetu ndani ya chombo hichi muhimu cha wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, **n**aomba pia nimshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Mhe. Abubakar Khamis Bakary kwa uwezo mkubwa wa ujasiri alionao katika kuiyoongoza Kambi yetu ya Upinzani ndani ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, mwaka huu tarehe 31/7/2010 ni upigaji wa kura ya maoni nchini ya kuamua ama Zanzibar iwe ni nchi ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa au laa, halkadhalika mwezi Oktoba, 2010 pia nchi yetu itakabiliwa na uchaguzi Mkuu wa kumpata Mhe, Rais wa awamu ya saba, waheshimiwa wabunge, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani, kwa sababu ya matukio haya mawili makubwa tumuombe mungu aipeleke nchi yetu – salama usalimini.

Mhe. Spika, niimani yangu kuwa Wazanzibar wote wenyehaki ya kupiga kura wataitumia fursa hii adhimu kuunga mkono kwa vitendo uwamuzi uliopitishwa na Baraza lako tukufu kwa KURA zote za NDIO za waheshimiwa wajumbe wa Wawakilishi wa wananchi.

Mhe. Spika, nidhahiri kuwa nchi yetu inakabiliwa na matumizi makubwa mawili mwaka huu, kufuatia chaguzi mbili (2) mfululizo hii ni changamoto ya kujipanga upya kukabiliana na hali mbaya ya Uchumi Duniani.

Mhe. Spika, bado karafuu ni zao muhimu sana kwa uchumi wa Zanzibar, na tungeishauri Serikali tena wakati umefika wa KULIBINAFSISHA zao hili, hali hiyo Serikali itaendelea kufaidika kwa Kodi zake huku wakulima wakinawirisha mashamba yao kupanda upya na kuyasafisha.

Mhe. Spika, Serikali inaonesha dhahiri kuwa zao hili linalihitaji bali haiwezi kulisimamia kwa uzalishaji wala utunzaji.

Aidha ni Serikali hii hii inayosema ! mambo ya BIASHARA sasa Serikali BASI, hivyo nikwanini kuna kigugumizi kwa Serikali yetu kutamka bayana juu ya jambo hili?

Mhe. Spika, mpango mkuu wa uwendelezaji wa mikarafuu kupewa shs. 60,000,000 ama 80,000,000 kwa mwaka hii ni dhihaka, na kamwe haistahiki kutajwa kwa zao kama hili tegemeo la uchumi wetu.

Mhe. Spika, Serikali ya CCM nisikivu, iko karibu na wananchi wake na inafanya kila linalowezekana kuhakikisha kuwa wananchi wake wanavuna mazuri kutokana na ILANI YA CHAMA – INAYONADI MAISHA BORA – kwa kila mtanzania!!, kama hivyo ndivyo! Hebu Serikali ya CCM ifanye kweli juu ya ZAO LA KARAFUU.

Mhe. Spika, Kambi yangu ya Upinzani, inaamini kwamba bado sekta ya Kilimo nimkombozi wa uchumi wa Zanzibar, aidha sekta hii inaendelea na itaendelea kuajiri idadi kubwa ya wananchi wetu hasa vijijini na kuchangia pato la Taifa kwa kupatikana fedha za kigeni, kutokana na umuhimu huu sekta ya Kilimo inamchango mkubwa katika kupunguza umasikini.

Mhe. Spika, mazao ya kilimo ni pamoja na karafuu, nazi, pilipili manga, pilipili kichaa- haya ni mazao ya biashara wakati mazao ya nafaka kama vile mpunga,mahindi, mtama, mawele hutumiwa kwa ajili ya chakula, pia kuna mazao kama muhogo, viazi vitamu, viazi vikuu, ndizi n.k. vyote vinasaidia sana katika suala zima la upatikanaji wa chakula kwa watu wa visiwa hivi na kwa hali hiyo ndipo vita dhidi ya adui njaa hushinda.

Mhe. Spika, kilimo mwaka 2009, kimechangia asilimia 31 ya pato la Taifa, ila hapa nipadogo Kambi yangu inaamini kuna asilimia kubwa zaidi bado hatujaifikia, hivyo basi nguvu za makusudi zinahitajika na kauli mbiu hai, itolewe na iyendelezwe juu ya kilimo kwa ujumla wake, aidha Dira ya Maendeleo 2020, mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini Zanzibar *(MKUZA)* na mkakati wa wa kukuza uchumi *(Zanzibar Growth Strategy)* yatabaki kuwa yanadai kufikiwa kwake.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo inamiliki matrekta 45 sawa na asilimia 83 ya mahitaji ya zana hizo hapa kwetu, pia hali ya hewa ya kuzalishia mazao nayo ilikuwa nzuri sana, bali kamwe haitoshi Wizara kutwambia kwamba kupatikanwa zana za kilimo na pembejeo kwa wakati pamoja na hali ya hewa nzuri mazao ya kilimo yaliongezeka kiidadi ya tani ama kilo!, wazanzibari walitarajia waambiwe ongezeko hilo la uzalishaji limepunguza kwa kiasigani uwagiziaji wa chakula hasa mchele nchi za nje! Na kuokoa kiasi gani cha fedha za kigeni?.

Mhe. Spika, Wizara kwa sababu mwaka 2009/2010 mkazo ulikuwa kuongeza kiwango cha uzalishaji wa mazao ya chakula ili kutekeleza mkakati wa uhakika wa chakula, sambamba na mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini, na kwa sababu hizo kambi yangu ya Upinzani na wazanzibari kwa ujumla wao wanapenda kujua je! Ni kwa kiasi gani dhana ya uhakika wa chakula mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini imefikiwa?. Mhe. Spika, Kambi yangu inapenda kujua hivi ni asilimia ngapi ya wakulima wameelewa na kutumia zana za kisasa na pembejeo BORA? Na ni asilimia ngapi bado? Na kuna sababu zipi zinazofanya wao wabakie nyuma?.

Mhe. Spika, Takwimu inaonesha bado jembe la mkono lina nafasi kubwa zaidi hasa kwenye kilimo cha mpunga wa kutegemea mvua, na hapa ndipo penye wasi wasi wa matumizi ya mbolea, dawa za kuulia magugu na zile za maradhi ama wadudu waharibifu wa mazao ya chakula , kwamba bado utumiaji halisi hauendi na upatikanwaji wa pembejeo hizo. Mhe. Spika, ili baraza lako tukufu liridhishwe nikuambiwa idadi ya ekari zilizolimwa, ngapi ziliwekwa mbolea, zikapigwa dawa ya wadudu waharibifu wa mimea, hili ingalisaidia kujua kwamba wakulima wanazitumia pembejeo vile ipasavyo au bado kunatatizo na liko wapi?.

Mhe. Spika, Tani 2,566 za mbolea zilinunuliwa na kutoka *FAO,* na kuuzwa kuruzuku ya asilimia 50, na lita 20,000 za dawa ya magugu zilizonunuliwa msimu huu na kutosheleza mahitaji, hii ni kauli ya Wizara ila tutaithibitishaje kama hatukuoneshwa idadi ya ekari zilizotumia mbolea na madawa hayo? Au kwa sababu tu dawa imebaki ndicho kigezo cha kutosheleza? Naje? Kama mbolea haikuuzwa kiruzuku wakulima wangemudu kuinunua na kuitumia mashambani?.

Mhe. Spika, bado kuna usumbufu wanaoupata wakulima huko mashambani, kuhusu huduma ya matrekta mipango zaidi ya utumiaji wa huduma huyo inahitajika kuondoa kabisa foleni ya kusubiri huduma hiyo hata kufikia wiki moja!.

Mhe. Spika, Taasisi za fedha bado hazijasaidia kilimo hapa Zanzibar, mabenki yetu yanayoingia hapa kwetu tungeona yanaenda sambamba na mafanikio ya wakulima wetu wadogo wadogo na wakati hapa nchini.

Mhe. Spika, halikadhalika Serikali ya Mapinduzi sasa iyone haja ya makusudi ya kuweka mazingira mazuri na ya uhakika yatakayowavutia waekezaji wa ndani na wa nje kuwekeza ndani ya sekta hii muhimu kwa maisha ya wananchi wa nchi hii na maendeleo yao.

Mhe. Spika, Benki ya watu wa Zanzibar, sasa umefika wakati wa kupokea hati za umiliki wa ARDHI itoshe kuwa ni KINGA ya kupatiwa mkopo tena uwe ni mkopo nafuu, kwa wakulima wazalendo wa Zanzibar pekee! Mhe, Spika, Katika kujenga Miundo mbinu ya Kilimo ni vyema pia kulitazama suala la kuwa na soko la BIDHAA zitakazozalishwa mashambani ziwasaidie wakulima kwa chakula na ziada iweze kuuzwa na kusaidia mipango mengine ya kiuchumi.

Mhe, Spika, Mabadiliko ya tabia ya nchi yanayadhofisha na kuyarejesha nyuma maendeleo ya nchi nyingi duniani, Zanzibar ni mojawapo!
Hivyo basi, ile dhana ya uvunaji wa maji ya mvua iliyokuwa ikizungumzwa ayami ya miaka sasa ifike mahali kwamba ni muda muafaka wa zoezi hili kuchukuliwa hatua zitakazo wezesha uzalishaji wa mazao ya kilimo yaende kama yalivyotarajiwa hata kama pale ukame utakapoikumba nchi yetu kwa kipindi kirefu.

Mhe, Spika, ikumbukwe kwamba Ilani ya CCM ya mwaka 2000-2005 na 2005-2010 inakubali kuwa kilimo kuwa ndio sekta pekee kwa uchumi wa Zanzibar na chanzo kikuu cha ajira kwa wananchi walio wengi hasa vijijini, aidha ili kuongeza tija na mapato ya wakulima, SMZ chini ya CCM iliahidi mambo yafuatayo:-

(i) Kusimamia sera mpya ya kilimo na kuwahamasisha na kuwawezesha wakulima kuendesha kilimo cha kisasa kitakachowezesha kutoa mazao mengi katika eneo dogo;

(ii) Kuendeleza kilimo cha matunda na viungokwa kuchanganya na mikarafuu na minazi, likizingatiwa tatizo la ufinyu wa ardhi na haja ya kuongeza aina ya mazao ya biashara;

(iii) Kuendeleza na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji kwa kuzingatia mpango mkuu wa kilimo cha umwagiliaji maji; na

(iv) Kuwahamasisha na kuwahimiza wazalishaji wa sekta ya kilimo kuazisha vyama vyao vya ushirika wa kuweka na kukopa *(SACCOS).*

Mhe, Spika, kwa sababu Bajeti kuu ya Serikali ya Mapinmduzi (SMZ) kwa mwaka wa fedha 2010/2011 imejikita kutekeleza sera za chama cha Mapinduzi na kwa sababu ndani ya ilani hiyo kulitolewa mazingatio maalum kwa Zanzibar.

Hivyo ni vyema Wizara hii kupitia kwa Mhe, Waziri mwenye dhamana atufafanulie mambo manne niliyoyataja hapo juu, ni vipi utekelezaji wake umefikiwa hadi sasa?

KILIMO CHA UMWAGILIAJI MAJI

Mhe, Spika, Kama tujuavyo mchele ni chakula maarufu kinacholiwa na wakaazi wengi wa Zanzibar pamoja na vyakula vyengine vingi vinavyopandwa nchini husaidia sana pale inapotokea upungufu wa mchele. Halkadhalika mazao ya nafaka kama vile mahindi, mtama na uwele yanakubali vyema hasa kwenye ukanda wa mawe nikote Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Ili tuweze kufikia dhana ya kuwa na uhakika wa chakula nchini hatuna budi tujikite kwenye kilimo cha umwagiliaji maji kwa mazao yetu mengi kama siyo yote ya nafaka na yale ya matunda na mboga mboga.

Mhe. Spika, Zanzibar, ina eneo la kuweza kulimwa kwa kumwagilia maji lisilopungua 8,521 ha. bali hadi sasa uwezo wa kulilima na kulimwagilia 730 ha. Na matarajio ya kulima ni chini ya 400 ha. kwa mwaka, je?

Mhe. Waziri ataliambia nini Baraza lako tukufu kwa mwendo huu tunaokwenda nili nchi yetu itaifikia ile dhana ya kuwa na uhakika wa chakula?.

Mhe. Spika, mpango mkuu wa kilimo cha umwagiliaji maji uliokua unatajwa kwenye vitabu vya bajeti vya Wizara hii tokea kuwepo kwangu ndani ya chombo hichi kitukufu cha wananchi, nadhani ipo haja ya wananchi wetu na hasa wakulima kupata maelezo ya yatulipofikia.

Mhe. Spika, uzalishaji wa mpunga wa kutegemea mvua hadi sasa ni 0.8 ton./ha. na uzalishaji wa mpunga wa umwagiliaji maji tumefikia 4 ton./ha. bado kiwango cha uzalishaji hakijafikiwa wa kuzalisha mazao mengi katika eneo dogo.

IDARA YA MIFUGO

Mhe. Spika, mifugo ni miongoni mwa sekta muhimu sana ya kusaidia hali ya watu wetu kiuchumi na ustawi wa jamii, aidha ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, mbuzi na kukuwa kisasa mbali ya kwaongezea lishe bora bali pia huongeza kipato na maendeleo yao.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni vyema nguvu zake za kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia mikopo ya mifuko mbali mbali izielekeze kwa wafugaji, wakulima wa mboga mboga na matunda.

Mhe. Spika, kwa kufanya hivyo dhana ya kua na uhakika wa chakula itaweza kufikiwa kutokana na wananchi wenyewe kupata uwezo wa kukabiliana na mahitaji ya zana pamoja na pembejeo, Mhe. Spika, pongezi maalum kwa Waziri wa Kilimo Mifungo Maliasili na Utalii kwa ununuzi wa mtambo wa kuzalisha *"Liguid Notrogen",* ni ishara njema maziwa tutasafirisha!

IDARA YA UVUVI

Mhe. Spika, Uvuvi ni miongoni mwa muhimili mkuu wa uchumi wa kipato cha mtu mmoja mmoja na kitaifa endapo Serikali itakubali kuyabadilisha mazingira duni ya uvuvi tuliyonayo sasa!

Mhe. Spika, bado haitoshi kugawa zana na vifaa vile vya ngwanda, mashine za nje na ndowana! Tukajifariji kuwa sasa wavuvi wetu watavua na kusaidia pato la Taifa kiuchumi, hatua hii siajabu kikundi kikajikuta wanagawana machofu ya banvua badala ya kipato.

Mhe. Spika, vifaa vya uvuvi vyenye thamani ya shillingi billioni 1.8 kwa vikundi vya ushirika Zanzibar vitasaidia bali bado Serikali inadeni kubwa na dhima haswa ya kuhakikisha wavuvi wetu wanavua katikati ya bahari kuu "EEZ", kwani huko ndiko kwenye uvuvi wa tija kwa mvuvi na kipato kwa taifa letu!

Mhe. Spika, juhudi zichukuliwe za kuhakikisha tunajenga mazingira bora ya kuwavutia waekezaji wa sekta hii muhimu, sekta ambayo vijana wengi na kinamama watamezwa viwandani kwenye kusanifu minofu ya samaki na vijana wengi wa kiume kutugumizwa kwenye mameli.

Mhe. Spika**,** waekezaji watalipa – KODI – mbali mbali, lakini pia ajira nchini itapatikanwa; kwa mantiki hiyo naiyomba sana Wizara hii ilione hilo kwa faida ya watu na maslahi ya Taifa letu Zanzibar mpya baada ya Oktoba, 2010 Inshaallah ! Amin!.

MISITU NA MAZINGIRA

Mhe. Spika, visiwa vyetu vimejaaliwa utajiri mkubwa wa maliasili, ambavyo ni vivutio vikubwa kwa watalii, juhudi zaidi zinahitajika kuhakikisha misitu ya asili kama vile Ngezi – Pemba pamoja na Jozani kwa Unguja, halkadhalika na msitu wa hakiba wa hifadhi Kiwengwa – Pongwe hapa Unguja.

Mhe. Spika, jumla ya miche 930,000 iliyozalishwa na vitalu vya Serikali na 610,000 ya vitalu vya binafsi vimetolewa na kupandwa, hii ni habari njema! Ila wasi wasi wangu nikuwa hii hesabu haiyendelezwi wala haisimamiwi, kwani bado akina "CHAIN –SAW" inaunguruma misituni bila siri wala kisisi! Halmashauri zipo na Masheha wapo – haya hufanyika mbele ya macho yao!.

Mhe. Spika, magari ya mchanga, uchimbwao bila ya mashimo kurejeshewa uwasilia wake tunashuhudia Halmashauri za Wilaya kupokea – ADA – toka kwa magari hayo "yumkini" kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara imekusudia kusimamia miradi mitatu (3)

(i) Mradi wa Hifadhi ya Misitu ya asili (HIMA) – Serikali ya Norway itagharimia US za Marekani 5,539,175 (Milioni Tano Laki Tano Thalathini na Tisa Elfu mia moja sabiini na tano);

(ii) Mradi wa Uhifadhi wa Misitu ya ukanda wa pwani utakaogharimiwa na GEF *(Global Envornment Fund)* US za Marekani 900,500 (Laki Tisa Mia tano tu); na

(iii) Mradi wa Uimarishaji mikarafuu uliotengewa Tshs. 80,000,000/- (Millioni Thamanini tu) zao linalotegemewa kiuchumi nchini.

Mhe. Spika**,** Wizara inakadiriwa kukusanya mapato ya shs. 1,293,774,000 (Bilioni moja mia mbili tisiini na tatu milioni, Laki saba sabiini na nne elfu) pia kwa mwaka wa 2010/2011 inakadiriwa kutumia shs. 27,374,817,000/- (Bilioni ishirini na saba mia tatu sabiini na nne Millioni laki nane kumi na saba elfu), shillingi 19,619,817,000 (Bilioni Kumi na tisa mia sita kumi na tisa Milioni laki nane kumi na saba elfu) ni kwa miradi (17) ya maendeleo, SMZ shs. 2,110,000,000/- (Bilioni mbili mia moja na kumi Millioni) na shs. 17,509,817,000/- (Bilioni kumi na saba mia tano na tisa Millioni laki nane kumi na saba elfu) kwa washirika wa maendeleo jee? miradi kumi na saba itatekelezwa vipi? Ilhali wanaotusaidia maendeleo hayo wako hoi kwa mtikisiko wa kiuchumi duniani mbona kuna kitandawili hapa?.

Mhe. Spika, bado kazi ipo, juhudi kubwa inayochukuliwa yakuzalisha miche ya misitu na matunda haijafuadafu kwa kasi ya ukataji miti ovyo kama sio ufujifu, elimu ya mazingira bado inahitajika la sivyo visiwa vinaangamia juu na baharini!!.

VYAMA VYA USHIRIKA.
Mhe. Spika, umuhimu wa ushirika kama mkombozi wa wakulima wafugaji, wavuvi na wafanyabiashara wadogo wadogo, halkadhalika ushirika wa kuweka na kukopa (*SACCOSS*) ni muhimu sana kwa kusaidia wananchi kupata chanzo cha mitaji ya maendeleo yao, hili linatambuliwa pia na Ilani ya CCM, 2000 – 2005 kif. 84. pg. 102.

HITIMISHO
Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kumshukuru sana ALLAH (S.W) kwa kuniwezesha kuisoma hotuba hii ya Kambi ya Upinzani mbele ya Baraza lako tukufu, Aidha nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa ridhaa na uvumilivu ulionipa na kuniwezesha kukamilisha kazi hiyo!.
Mhe. Spika, niruhusu niwashukuru sana! Wananchi wa Jimbo langu la Uchaguzi Wete, kwa mashirikiano na ushauri wanaonipa kila ninapohitaji, jambo linalonirahisisha itendaji wa majukumu yangu waliyonikabidhi.

Mhe. Spika**,** nawaomba wananchi wa Jimbo la Wete na Wazanzibari wote wanaoitakia kheri Zanzibar yao kwamba ifikapo tarehe 31 Julai, 2010 wakatie "NDIO" ya KURA ya Maoni kwa faida ya Wazanzibar na maslahi ya Zanzibar tuitakayo !.

MUNGU WABARIKI WAZANZIBAR, IBARIKI ZANZIBAR, IBARIKI TANZANIA IBARIKI AFRIKA "AMIN".

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa moyo wangu kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kunipa pumzi dakika hii kuweza kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Kilimo.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wakuu. Lakini pamoja na hivyo nina salamu za pekee kabisa kutoka kwa wananchi wa Shehia ya Kipandoni kumletea Mhe. Katibu mwenyewe.

Mhe. Spika, pamoja na hayo walitaka wananchi wangu wa jimbo la Kitope hasa shehia ya Kipandoni walikuwa katibu wa Kilimo hawamjui jina lake nani leo nawambia kupitia Baraza anaitwa Dokta Khalid.

Mhe. Spika, nianze katika ukurasa wa 13 katika Kamisheni ya Kilimo, Utafiti na Elimu kwa Wakulima. Nimshukuru sana Kamishna huyu pamoja na watendaji wake wakuu pamoja na kijana wake mmoja Othman kwa kutoa elimu nzuri ya wakulima na tumeona maendeleo katika majimbo yetu yaliyokua yana ukanda wa sehemu kubwa ya ulimaji. Hivi karibuni nashukuru sana umewafanyia vijana wa Kirombero kuwatoa Unguja kuwapeleka Pemba kwenda kuona jinsi gani kule Pemba maendeleo yao ya upandaji wa muhogo.

Kwa kweli wameridhika na wameona jinsi ya utaalamu au taaluma waliyoipata kupitia msaada huu ulipitia kwa Naibu Waziri Kiongozi nay eye alichangia sehemu kubwa baada ya kutembelea sehemu ya mabonde ya muhogo na akatoa ofa hiyo wamepeleka na waliporudi wamesifu sana na wametoa pongezi na sasa nafikiri wamo katika mashindano ya upandaji kati ya Pemba na Unguja muhogo basi safari hii Unguja tutakuwa nambari one.

Mhe. Spika, kwa kuendelea kuchangia naingia katika ukurasa wa 20 katika chuo cha Kizimbani. Wananchi wengi katika majimbo huwa wanauliza katika hii ni jinsi gani au njia gani. Hili namuomba Mhe. Waziri aje kutusaidia ili waweze kuingia kupata kwenda kujielimisha wafanye njia gani hao wananchi katika majimbo au kuna kipimo gani kinamfanya mtu aweze kuingia katika chuo hicho. Ningeomba Mheshimiwa anisaidie ili wananchi wetu wengi katika majimbo na wao wanataka kuwa wataalamu katika masomo ambayo fani inayosomeshwa katika Chuo hicho.

Mhe. Mwenyekiti, alisisitiza sana kusema kuwa kiwezeshwe. Kwa hivyo tunaomba Mheshimimiwa kwa kupitia mafungu yako basi ukione hiki chuo kiwezeshwe ili kende na wakati kabisa au kiwe na mashirikiano katika vyuo vyengine kati ya Bara na nchi nyengine. Kiwe na hadhi ya kimataifa.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 23 Idara ya Umwagiliaji Maji. Hapa kidogo nitachukua muda kwa sababu kila bajeti ikija katika vitabu hivi wanataja Kibopwa, Cheju. Mheshimiwa tuna lengo kubwa la kutaka kuondoa umasikini kwa kupitia umwagiliaji maji mpunga ili wananchi waondokane na umasikini.

Zanzibar kama alivyosema mwenyekiti wangu hapa asilimia kubwa tunapenda kula ubwabwa. Huu ni ukweli usiofichika, watu wa Zanzibar wanapenda kula wali na hili ni suala la ukweli na uhakika. Hili zao kama litashikwa hasa au litapewa taaluma au litawezeshwa au litapewa fungu kubwa sana naamini tutaondokana na umasikini. Vile vile hii kila siku Kibopwa, kuna maeneo mengine ambamo tayari yanarutba nzuri, yana maeneo makubwa kabisa, ningeomba kwa kupitia Katibu wake Mkuu hebu tuangalie katika ukanda wa Kirombero, Pangeni, Upenja kule kuna maeneo mazuri sana na yapo siku nyingi.

Lakini kila nikiangalia katika kitabu hatutiwi kwenye programu hizi, lakini kama zipo tetesi nimesikia sasa hivi kuna mradi ambao unakuja wa wasaidizi wa Shirika wetu wa Ummoja wa Mataifa. Naomba kwa kupitia Mhe. Waziri na Katibu wake hebu mara hii au bajeti inayokuja au kabla yakuondoka kwenye majimbo watuoneshe ile nia yetu. Sisi tunataka turithiwe sio mimi kila siku kwamba nitakuwa katika jimbo lile tu, hapana lakini naanza kujenga plan ya kuona jinsi gani wananchi wangu nawajali katika kuwaondoshea umasikini.

Mhe. Spika, umwagiliaji maji mpunga kwa kweli ni njia moja ya kuondoa umasikini. Hebu tuangalie hivi sasa hivi kwa hesabu za mtazamo ghafla tu kilimo hiki cha kutegemea maji ya mvua hebu tizama sasa hivi nenda kwenye mabonde waliokuwa hawajapata athari zile za magonjwa. Wanavuna mpunga tena mara hii ni mnene kabisa una rutba nzuri. Juzi nilimuona Mhe. Katibu wangu sehemu za Cheju anavuna. Kwa kweli sijui ile TV ilinidanganya lakini nilione ile chembe moja ya mpunga ni nene kabisa, inavyoonesha kuwa wale walilima kwa wakati, walipata mbolea, walipata dawa ya kuuwa magugu, hata matrekta yalisogea kwa muda huo. Naomba hii Idara Iwezeshwe ndio maana huku nyuma tunaambiwa **“Kilimo ni Uti wa Mgongo”.**

Siku zote Wizara hii inaonewa, Wizara hii inapewa mafungu ambayo ni madogo sana, leo trekta moja tunaambia sichini ya milioni 60. Kwa kweli hili fungu wanalopewa hawa hatutofika pahali, ukweli tuseme kwa sababu leo Mhe. Waziri wa Kivuli anasema kuna matrekta 40, katika Zanzibar nzima, wengine watakuwa katika foleni ya kusubiri na hata likifika kule tusidanganyane tunampotezea nguvu bure yule jamaa, hata akija akifika kwa wale wanaotaka kulimiwa muda ushapita na mvua zenyewe tunaziona.

Kwa hivyo tungeomba sana pamoja na ziada ya fungu alilopewa wakati sisi hatuwezi kulitengua lakini iyone serikali umuhimu zaidi yakuongeza matrekta. Huku nyuma nimeona kuna kitrekta kidogo kwenye picha, kitrekta hichi kama ni kweli yapo au ni picha tu basi ibakie picha lakini kama hapo yanatosha hapa sio lazima tununue matrekta makubwa tena haya ni mazuri katika ule ulimaji wa zile ploti za mpunga wa kumwagilia maji. Kwa sababu sehemu nyengine ukenda kwa wenzetu kama Bara huko utavikuta vile vinaingia kwenye yale mabonde yanatifua, yanachimbua halafu yanaburuga.

Mhe. Spika, ningeomba hii isiwe tumewekewa picha tu na haya yaletwe. Wenzetu kule. Bara wana *contract* na mabenki na sisi sasa hivi CRDB ipo hapa ambayo ni mkombozi wa wakulima, basi kilimo waingie nao ubiya waende kule wajikubalishe, wako tayari kuweza kukopesha wale kwa kupitia mgongo wao na wao wataangalia jinsi gani wale wakulima ambao wenye ulimaji wa kutia tija kuweza kulipa wataangalia na wao. Ningeomba kwa kupitia kwa Waziri hili suala alione kwa umuhimu zaidi ili kuweza kuwasaidia.

Mhe. Spika, naingia katika ukurasa wa 25 katika Idara ya Maendeleo ya Mifugo. Hapa mimi nasifu sana tumeona jinsi gani muhusika mkurugenzi wake wanavyojitahidi. Lakini pamoja na hayo kuna kitu kimoja kidogo hichi naomba Mhe. Waziri kupitia Katibu wake kule Pangeni atusaidie. Kule Pengeni kuna dhana ya wananchi wanasema kuna eneo lao wamelima na sasa hivi wanavuna embe lakini inavyosemekana wameingia kimakosa. Lakini kama ni makosa watatuzi nani? Serikali.

Mhe. Spika, mimi naamini Waziri ni mtu mzima, msikivu, mlezi mzuri kwa kupitia Dokta wake Khalid halikadhalika ana imani na wananchi kwa sababu uzoefu wake ni kuwatatulia wananchi sio kuonesha wizara yake inakandamiza wananchi kwa sababu hii ni moja katika kilimo. Sasa pale wamelima, wanavuna embe, minazi lakini hatimaye wanaishia polisi. Hili ni suala la kusikitisha, lakini najua wazi Mhe. Spika kwa kupitia Waziri na Katibu na watendaji wake wakuu hili suala litapewa suluhisho nzuri na wataendelea kuishangiria kabisa Wizara yao ya kilimo kwa kuipa utekelezaji wake mzuri.

Mhe. Spika, Kwa kweli mtu keshapinda mgongo miaka nenda miaka rudi leo anaambiwa hili zao si lako kwe kweli inasikitisha. Kwa hivyo naomba utusaidie twende kama tulivyokwenda kipandoni mkawasaidia na leo wanatoa pongezi za dhati kabisa kila wakikaa wanasema, Katibu lakini Mheshimiwa hatumjui jina lake.

Mhe. Spika, nipo katika ukurasa wa 29 Idara ya Mazao, Biashara, Matunda na Misitu. Msitu wa Kiwengwa tusifichane unapotea. Kama hizi sheria hazifanyi kazi au zina mapungufu tuletewe tuzirekebishe, misitu iliyobakia sasa hivi ni miwili tu msitu wa Jozani na Kiwengwa. Mheshimiwa sasa hivi tayari Ramadhani hiyo hapo, ikifika Ramadhani sisi viongozi ambao tunaoupenda ule msitu tunakuwa tumbo joto, tunatishiwa amani, tunaambiwa hatupewi kura. Mimi nasema na nisipewe kura lakini msito sitokubaliana nao ukatwe.

Msitu wa kiwengwa ni muokozi kuna vianzio vya maji vya asili na asili na ile vimeanziwa kutokana na msitu wenyewe, ingekuwa hakuna msitu basi vile vianzio Wallahi sasa hivi ingekuwa vimeshakauka vyote, lakini kutokana na ule msitu wenyewe ulivyokuwa umejishona kule na vile vianzio vilivyokuwa havipati jua vya kufyonzwa basi umekuwa unahifadhika.

Mhe. Spika, msitu wetu tusipoangalia unapotea na sisi viongozi tusiogope kutishiwa hivyo. Leo kweli mwananchi wangu nimuachie anibomolee nyumba yangu au abomoe afisi kwa kuwa ananitishia hatonipa kura. Sikubali. Msitu unakwenda zake. Tumeunda Kamati, kamati zinakuwa hazifanyi kazi zinazidiwa, Waheshimiwa wanakwenda kule watu wanachukua mashoka, mapanga kwa kweli inasikitisha.

Mhe. Spika, mimi siku moja nilijitolea na wananchi wangu walinita, si vibaya nimelala mwituni. Nilivyolala mwituni huu ukumbi wako wote ndani fanya 10x4 watu waliokuwepo kwenye msitu wa Kiwengwa, majiti mabichi kabisa Matani kwa Matani yaliyokuwepo pale yaliyokushanywa na picha tunazo. Kina mama kina baba sawa kwa sawa. Hivi kweli Mheshimiwa tutakuwa na msitu wa Kiwengwa.

Tukipeleka ripoti polisi, wale polisi wanatoa *direction* wenyewe wanaambiwa leo wapo wenyewe, anaambiwa mwenye gari usije. Mwenye gari haji lakini siku hiyo tungekuwa tushakufa, mwenye gari wallahi tumeweka kile kigari changu kidogo almanusura na yeye nimemsifu kwa upande mmoja kapata udereva vizuri, lakini alikipembua kile na tani ya kuni nyengine zikenda zake chini zikaangukia kwenye bodi ya gari. Siku hiyo ilikuwa hatari tupu anaitwa njiwa basi apenya kweli kweli. Hili ningeomba Idara husika au Wizara husika jamani sheria zipambe moto. Ramadhani inakuja msitu unakwenda zake na maji, tusipoangalia.

Mhe. Spika, niingie katika ukurasa wa 33 Idara hii sitokuwa na mengi niisifu sana tu kwa utendaji wake mzuri. Sasa hivi tumeona makabrasha hapa mazuri ya *MACEMP* imeonesha jinsi gani ilivyolinda fedha za watu za *World Bank*, wenyewe Would Bank wamesifu na sisi jamani tusifuni kwa sababu utendaji mzuri. Mzungu kama hukuonesha jinsi gani feza zake zinavyotumika basi hakubali kukuletea lakini wanaendelea kutuletea *MACEMP* itatusaidia vizuri. Isipokuwa Mheshimiwa mwenzangu alisema kuwa tuongezewe tu na kufika katika bahari ya kati kati hilo nalo Mhe. Mkurugenzi msikivu naye tunamuomba atusaidie atupe vyombo vikubwa zaidi ili tuendelee kupata matunda yake mazuri sana na yeye Mwenyezi Mungu ambariki kila la kheri kwa kulinda pesa za watu wenyewe wafadhili hawa.

Mhe. Spika, mwisho mazingira, hili limeliripoti na nitaendelea kuliripoti. Nimemwita Mkurugenzi wa Mazingira akaangalie kule ukanda wa pwani ambapo kuna hoteli imeshaharibu, sasa inatengeneza shimo la kufanya kama gati. Nayo sheria nimesema kama yake sheria haina meno basi aje tumtengenezee tumtie meno, athari inaendelea kule vigogo vimepangwa huku na mpaka leo havijang'olewa. Namuomba Mhe. Mkurugenzi, mwenzangu anisaidie hili suala linaendelea kuathiri kule, itafanya kima kile cha maji pale kwa sababu watu miya wanabeba mchanga kupeleka juu, nambie leo halifanyiki shimo? Basi hili nalo alione kabisa, leo nikiondoka hapa nikirudi vigogo vyote kwa uwezo wako mkurugenzi viondoke mara moja.

Mhe. Spika, kwa hayo naunga mkono asilimia mia kwa mia pamoja na wananchi wangu wa jimbo la Kitope kutokana na Wizara hii ya Kilimo ndio uti wa mgongona Inshallah Jimbo la Kitope litaondokana na umasikini kwa mpunga wa kumwagilia maji Kirombero, Pangeni na Upenja. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Said Khelef Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na miye kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Ardhi. Pia sina budi kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote.

Mhe. Spika, nikianza kuchangia nataka kuchangia Idara ya Mazingira kwanza nawapongeza na wao kwa kazi zao nzuri wanazozifanya lakini pia nina masikitiko, kwanza nataka nijue hii Idara ya Mazingira shughuli zake ni nini? Pili Wilaya ya Kaskazini "B" ni Wilaya imetekwa mchanga sana na mazingira yanaharibika vibaya sana. Sasa nilitaka nijue hapa kwamba je, pale wanapowaruhusu wale kuchimba mchanga huwa wanakwenda kuangalia au hawendi?

Mtu kuuza shamba lake hatukatai lakini kitu tunachoomba basi angalau pale pahala pakaangaliwe ile hali ilivyo. Katika jimbo langu palitokezea tatizo la kutaka kuchimbwa mchanga lakini wananchi wa jimbo langu wakasema mchanga hauchimbwi na kama utachimbwa basi tutamwaga damu. Kwa busara ya Mhe. Waziri Kiongozi nampongeza kwa juhudi yake na kazi yake nzuri aliyoifanya pahala pale pamezuiliwa.

Mhe. Spika, lakini humu mnamochimbwa michanga kuna minazi, miembe kuna mizao chungumzima. Minazi inateketea leo mnazi unachongwa boriti, unapasuliwa mbao, nahakikisha baada ya miaka miwili minazi itakuwa haipo. Yanachimbwa mashimo ya michanga minazi inang'olewa.

Sasa katika hiyo sehemu ninayosema Waziri Kiongozi aliifatilia ilikua ni sehemu karibu na mto, ina minazi michanga tu. Sasa mimi nilisikitika ile minazi ilikuwaje ikakatwa kabla ya kupata mfano kibali na mazingira wanajua na suala lile wanalijua kama walikuwa hawalijui kazi yao ipi. Huyo aliyetaka kuchimba mchanga alitaka kuchimba kwa ruhusa ya nani ata akakata ile minazi michanga.

Mhe. Spika, sehemu hiyo ni karibu ya mto tena wakati mwengine mto huo unachanganyika na maji ya chumvi, nina hakikisha pengichimbwa mchanga basi jimbo Bumbwini lingekuwa halipo. Sasa tunapotoa hizi ruhusa naomba basi angalau kwanza pale pahala pakaangaliwe ikiwa mazingira ndio kazi yake basi wakaangalie wasiruhusu tu watatuumiza.

Kama sio tishio la kusema kwamba watu watamwaga damu pengelichimbwa kwa sababu huyo bwana alikuwa keshajifanya yeye ndio mbabe. Lakini namshukuru Mhe. Waziri Kiongozi Mwenyezi Mungu amjaalie maisha marefu atusaidie.

Mhe. Spika, nikiacha hapo hapa natoa ombi langu naona hapa imeletwa jumla ya tani 289.55 za pembejeo ya mbolea. Mbolea hii imesambazwa katika vituo lakini vituo hivi katika jimbo langu hakuna, kwa vile wananchi wangu wanapata tabu

wakati wa kutolewa hii mbolea kuifatilia kule kwenye kituo. Namuomba Mhe. Waziri atusaidie kututafutia sehemu katika jimbo la Bumbwini ili ziwekwe hizi pembejeo ili watu wapate urahisi wa kufatilia.

Mhe. Spika, jengine mbegu zinazostahamili ukame. Hivi nafikiria zimeingia katika jimbo langu lakini wamepata watu wawili. Kwa vile wananchi wa Bumbwini sasa hivi hawana konde za kulima, kwa sababu konde walizokuwa wakilima zimechuku na Kiwanda cha Sukari, inalimwa miwa. Sasa ilivyokuwa mbegu hizi zinastahamili ukame na sehemu za juu namuomba Mhe. Waziri katika Jimbo langu uzidishe zaidi badala ya hao watu wawili basi uwaongezee zaidi.

Mhe. Spika, mimi kwa kusema kweli sina maelezo mengi lakini leo hapa ninasema kwamba mimi kipindi kinachokuja sitogombania tena nataka kupumzika kwa hali yangu. Kwa vile nawaomba wanachama wangu wa jimbo la Bumbwini maana hawana wasi wasi, leo nasema hapa mbele ya kiriri hichi wasikie kwamba nimewapa ruhusa ukifika wakati wachukue fomu wajaze na Mwenyezi Mungu atawajaalia salama na amani na wenzangu mliomo humu Mwenyezi Mungu atakujaalieni mtapata mnalolitafuta na sisi mje mtusaidie msitusahau.

Kwa hayo machache Mhe. Spika naunga mkono hotuba hii asilimi mia kwa mia ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Omar Ali Jadi: Ahsante Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tukawa tuko hai na afya njema na kufika hapa kuja kutekeleza majukumu yetu.

Pia Mhe. Spika, nikushukuru wewe na mimi kunipa nafasi ili kutoa mawazo yangu katika Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ambayo ni wizara muhimu katika nchi yetu kwani huwa inawagusa jamii yote. Nataka nimpongeze Mhe. Waziri wa Kilimo na watendaji wake kwa upeo mkubwa kabisa ambao kuwa kuna mambo yakuyaonea imani yeye kasema wacha binadamu lakini mpaka wanyama akawaangalia kwa jicho la huruma.

Mhe. Spika, kwa sababu muda ni mchache sitaki nipoteze muda wako mkubwa niendelee kwenye bajeti moja kwa moja. Mimi nataka nianze na ukurasa wa sita katika sehemu ya uvuvi. Mhe. Spika, tukielewa kwamba uvuvi ni moja katika changamoto na ukusanyaji wa maendeleo katika nchi yetu na kwa sababu sekta hii ya uvuvi umewagusa jamii kwa asilimia kama 50 ya wananchi walio katika nchi hii. Bahati nzuri Mkurugenzi kajitahidi kuwaelekeza jamii, kuwafahamisha kujua malengo yao na taratibu gani zinazotaka kutumiwa katika uvuvi. Mimi nasema sina budi nimpongeze.

Mhe. Spika, zamani nilikuwa ni mkaidi sana kuweza kuona masuala ya uvuvi yanakuja mimi nina wavuvi lakini sioni tija yoyote, lakini nina imani huwezi ukampatisha mtu kitu kama hujampa taaluma. Mhe. Spika, mtu anatakiwa umpe taaluma halafu umpe kitu afanyie kazi. Kwa hivyo, nasema Mkurugenzi ahsante sana Mwenyezi Mungu akujaalie juhudi zako ziendelee, bado usichoke, usisite chukua majukumu yako.

Mhe. Spika, kufanikisha malengo haya kama serikali tayari imeshatoa pesa kuwaelimisha jamii ingekuwa ni vyema Mkurugenzi huyu akawezeshwa zaidi, akapangiwa bajeti inayolingana na wakati ili kuondoa kero za wavuvi. Mhe. Spika, ameshawapa taaluma, ameshawapa maelekezo wanataka nyenzo sasa, na kama ni nyenzo serikali imuwezeshe Mkurugenzi awawezeshe wavuvi ili wapate haki zao katika nchi.

Mhe. Spika, ukiangalia ukurasa wa 6 katika mavuno ya samaki ya mwaka 2009 basi wavuvi wamefanya kazi kubwa sana, na wamefanya kazi nzuri yakupewa mafanikio na kupewa hongera. Kwa hivyo, Mhe. Spika, katika pongezi hizi zisiende ovyo serikali nasema tena bajeti ya Idara ya Uvuvi bado ni ndogo kabisa. Kuna mambo ambayo huwa huwezi ukayaepuka lakini unayapunguza bajeti zake, ukayaelekeza kunakozile idara husika.

Mhe. Spika, kwa sababu malengo yetu ya mwaka 2010-2011 tunataka wavuvi wetu waachane na uvuvi huu mdogo mdogo ili idara hii ifanye kazi zake wapate kuelekea kule waziri anakokutaka kwenda kuvua bahari kuu. Kwa hivyo, kuna haja ya bajeti ya dharura kupewa Mkurugenzi wa Uvuvi ili wavuvi wetu sasa hivi wapate vifaa vya kwenda nje kuvua samaki wale ambao kuwa wanatakikana.

Mhe. Spika, cha ajabu ni kwamba rasilimali tunayo, watu tunao tunashindwa kuwafanyia kazi tunaziacha meli za kideni zikivua samaki wetu wakati tija ile ni ya Wazanzibari. Nafikiri hapa karibuni tuna mifano mengi meli moja tu iliyokamatwa miezi sita wanauza samaki. Je, kama serikali imemuwezesha Mkurugenzi na kwa sababu wavuvi wameshapata taaluma kubwa malengo yetu ni kuvua bahari kuu, tunapomuwezesha Mkurugenzi akawafanikisha wavuvi nina imani maendeleo yatakuja.

Mhe. Spika, nichukue ule msemo wenzangu waliosema baada ya kula muhogo kwa samaki tutakula samaki kwa muhogo sasa. Kwa hivyo, nafikiri Mhe. Spika, serikali imenisikia, waziri amenisikia tufanye hima ili tupate malengo tuliyoyakusudia katika jamii.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niende katika Idara ya Mifugo. Mifugo ni jamii moja ya wananchi ambayo huwa wanajitahidi kufanya maendeleo na wakajipatia kipato na rizki pamoja na kuisadia serikali. Mhe. Waziri humu ameelezea humu

namna ya mifugo alivyoichanganua lakini bado mifugo wananchi wetu hawajapata taaluma yakutosha. Mtu unaweza ukampa pesa leo akafuge ng'ombe, kafuge kuku lakini baada ya wiki ikitokea baridi basi hana tena hata kuku mmoja. Kwa hivyo, ningeliomba serikali kupitia wizara hii ikawaelimisha jamii juu ya mifugo namna ya kufuga, namna ya kuendeleza mifugo na namna ya kuhifadhi mifugo yao wakati inapotokezea majanga ili wapate tija nzuri na wapate mafanikio ya kujiendeleza katika maisha yao.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niende katika ukurasa wa 4 katika changamoto iliyopatikana kipindi hiki kilichopita, ni wizara kuvumbua mbegu tatu za mpunga ambazo ni bora, mbegu nne za mihogo. Mhe. Spika, kupitia kwako ningelimuomba Mhe. Waziri kuhusu mbegu hizi zisiwe ni kumalizia eneo moja kwa sababu ni mbegu bora zinazohimili vishindo vya ukaazi, basi zienee katika maeneo yetu yote ya nchi hii ya Zanzibar ili kupata maslahi na mafanikio tuweze kuondoa shida zetu.

Mhe. Spika, ambacho kuwa kidogo kitanitetemesha niseme sijui Mhe. Waziri wa uzee wake au binadamu amesahamu, kipindi kilichopita tuliahidiana kwamba atakuja Pemba na akija atanitafuta tuonane tukaangalie yale matatizo ambayo huwa nayazungumza kila leo, bahati nzuri hakupata kuja. Mimi nina wasi wasi huu hizi mbegu kama kweli nazo zitafika kwa wananchi. Kwa hivyo, ningemuomba achukue jitihada za makusudi na pindipo akiingia Pemba akifika jimboni kwangu anitafute popote nilipo kabla sijamaliza kipindi hiki ili tuangalie tatizo gani la kuwaokoa wakulima wetu na kupata mbegu hizi utaratibu gani utakaotumika.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo kuna neno langu sitaki nije nilisahau nataka niende katika ukurasa wa 68. Kwa kweli hapa nimekuta mambo ambayo kuwa sisemi kama yamenifurahisha au niseme pengine nimebanabana na hapa nije nipate maelezo ya kina katika maelezo yangu nitakayoyatoa.

Mhe. Spika, kuwaonea imani wanyama sijasema ni tatizo, lakini kuna wanyama wa aina ambao binadamu wanawatumia kwa faida hii na kuna wanyama wanaotumia kwa faida nyengine mbali mbali. Lakini masikitiko yangu makubwa ni kuweza kupatiwa chacho na afya bora mbwa 10,000 na paka 5000 kuweza kupatiwa kinga ya uzazi. Lakini cha ajabu ng'ombe hawajatiwa wala mbuzi kwa kweli haya yamenisikitisha.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri angeliangalia na akafanya utaratibu ng'ombe na mbuzi hata kuku basi wakaelekeza bajeti yao ikapunguzwa bajeti kwenye chanjo za mbwa na paka ikaelekezwa kwenye kuku. Mhe. Spika, chakushangaza zaidi hapa Mhe. Waziri amenichekesha kidogo maana sasa katika uzazi wa mpango wa binadamu sasa tunakuja kwenye mbwa na paka, amesema kwamba mbwa

wanataka kufungwa uzazi na paka. Hili mimi kwa kweli linanishangaza, lakini ningelimshauri waziri kama nia ni hiyo basi bora tungechukua bajeti upande mmoja tukaelekeza kwenye kondom ili mbwa nao waweze kupanga uzazi. (*Kicheko*).

Mhe. Spika, ni kwamba hilo sina ubishani kwa sababu tunataka tuwaenzi wanyama na huwezi ukamuenzi mnyama bila ya kumpa tastarehe yake na yeye. Tunataka kuwafanyia chanjo, tunataka kuwapunguzia uzazi sasa kwa nini isiwezekane kuwapatia kondom angalau kupunguza uzazi zaidi, halafu malengo yetu kwa sababu tunataka mbwa wasizae hilo ni moja katika kuzuia uzazi na maradhi ya kuambukiza.

Kwa hivyo, mimi ningemuomba Mhe. Waziri kama hili hakulifanya kwa utani maana wengi wanacheka pengine waziri amekusudia kuliboresha vyengine ikawa limeingia hili ikawa kama ni utani. Lakini kama waziri hakukusudia kama ni utani basi na mimi nasema nisingefanya utani tuangalie mazingira ya maslahi yao.

Mhe. Spika, kwa sababu bajeti hii mara hii kama nilivyosema mwanzo Mhe. Waziri amejitahidi na mzee wangu nimeshachoka kumpigia buti sana, niseme kwa hayo machache niunge mkono bajeti hii. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa na mimi kuchangia bajeti hii ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira.

Mhe. Spika, mimi kwanza naanza kwenye kilimo cha mikarafuu. Mhe. Spika, kwa masikitiko kabisa naona bado Mhe. Waziri kilimo cha mikarafuu hajakipa kipaumbele kwa sababu amesema kwamba sasa hivi kilimo hakiko mstari wa mbele tuna utalii ndio unaoshika hatamu ndio maana ikawa hakipewi uzito.

Mhe. Spika, mimi ninavyokumbuka siku za nyuma karafuu zikizaliwa tu bado hazijawa vizuri ni dalili tu ya karafuu, basi wazee wetu walikuwa wanaanza kukopa pesa kwa ajili ya kuja kutumia karafuu zitakazochumwa. Lakini sasa hivi Mhe. Spika, karafuu zinafika kuchumwa basi mtu hathubutu kukopa pesa za watu kwa sababu hiyo ni kwamba karafuu hazikupewa uzito na tumeona kama sasa hivi serikali inaona karafuu hazina maana. Mhe. Spika, nataka niungane na Waziri Kivuli kama sasa hivi umefika wakati wa zao la karafuu kubinafsisha kupewa fursa wenyewe wakauza wanapotaka.

Hasa ukizingatia wakati nilipouliza suala kuhusu masuala ya viwanda Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji aliniambia kama sasa hivi serikali imejitoa kwenye biashara. Kwa hivyo, kama wamejitoa kwenye biashara basi na hili zao la karafuu tuwape ruhusa watu kila mtu auze anapotaka. Mhe. Spika, ni

bora serikali ikusanye kodi tu lakini iwe ni hurusa mtu kuuza karafuu zake anakotaka. Mhe. Spika, naomba kwani sasa hivi wakati umefika tulione hili ili tuwape fursa watu ili wapate kujitegemea wenyewe.

Mhe. Spika, kwa sababu ukiangalia sasa kuna mpango wa miradi ambayo itatekelezwa kipindi kinachokuja. Lakini karafuu zimeingiziwa fedha kidogo zaidi kuliko ile miradi mengine, na wakati ukiangalia kama karafuu ni zao la taifa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi ninashauri namuomba Mhe. Waziri aishauri serikali ili tuharakishe iwe wakati umefika sasa tubinafsishe zao la karafuu na watu wauze karafuu zao wanapotaka.

Mhe. Spika, suala jengine nije kwenye kilimo cha maweni kwa sababu mimi ni mtu wa maweni kwa hiyo lazima na hili nilizungumze. Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo ina wataalamu wengi na kwa masikitiko mimi naona labda hawa wataaalamu sijui wanaishia wapi lakini kwa kweli kwenye kanda za maweni hasa Micheweni mimi sijawahi kuwaona wataalamu kuja kuwapa watu elimu au mafunzo ya kulima vilimo vya maweni ambavyo vinastahamili ukame sehemu za maweni.

Kwa hivyo, ninaishauri serikali pia wakati umefika sasa hivi kuboresha na kule maweni kuwapa watu utaalamu wa kilimo na walime yale mazao ambayo kuwa yanaweza kustahamili ukame. Mhe. Spika, ukiangalia sisi Micheweni watu wamezoea kulima mtama, uwele, muhogo na migomba lakini si ile ya biashara sana ni migomba ya boko.

Mhe. Spika, wakati umefika ukiangalia micheweni vitunguu vinakubali, kilimo cha mbatata nina uhakika kinakubali, viazi vitamu vinakubali kwa maana hiyo umefika wizara hii sasa iende na kule maweni iwape elimu wananchi na iwaelekeze wakati gani unafaa kulima vitunguu, wakati gani unafaa kulima mbatata.

Kwa hivyo, iwe ni vilimo vya mbadala badala ya kuwa watu wanalima muhogo na uwele serikali iwaelekeze kama jamani tulimeni na kilimo hiki. Mhe. Spika, kama wananchi watapewa maelekezo na wapatiwe mbegu nina uhakika kama watu watalima na wataweza kuuza biashara ambazo zitawasaidia.

Mhe. Spika, kila siku tunakuja huku kwenye bajeti tukiangalia kama ukanda wa Micheweni ni ukanda mmoja ambao ni masikini. Lakini kama wataelekezwa vizuri basi wataweza kujisaidia, lakini ukiachana na kuwa serikali imetulia tu haiwaelekezi ndio maana tunakuwa pale pale hatwendi mbele. Kwa hivyo, naiomba serikali kupitia Wizara ya Kilimo wale wataalamu sasa wateremke na kule maweni wende wakawaelekeze watu.

Mhe. Spika, kama walivyozungumza wenzangu waliotangulia kama jamani Zanzibar ni sehemu ya bahari na tumezungukwa na bahari na baharini kuna faida kubwa, mna rasilimali kubwa ambazo zinaweza kutusaidia ukiachana na utalii, kilimo lakini na uvuvi unaweza ukatusaidia na ukaipatia tija serikali. Lakini bado hatujawa tayari kuwaelimisha watu na kuwapatia watu zana za kisasa ili tukafaidika na bahari. Mhe. Spika, baharini mna samaki hawajawahi kuona watu hata siku moja. Kwa hivyo, naiomba serikali iangalie kuleta zana za kisasa ili tufanye kazi, sisi hapa tuna utajiri baharini lakini bado hatujataka kuutoa.

Mhe. Spika, ninaiomba serikali ione sasa wakati umefika wa kufanya kazi kwenye bahari kwa sababu wavuvi wetu unakwenda kuwapa zana ambayo haina tija, lakini kuna eneo la kwenda samaki hawajasikiapo hata kama kuna watu. Mhe. Spika, kule kwetu kuna eneo kuna bahari samaki wanacheka tu wakizungumka hao ni kwamba hawajafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, ni kwamba wakati umefika hebu zungumzeni na hao wafadhili ili watuletee vyombo vya kisasa ili tufanye kazi. Sisi tunasikitika hapa kwetu kama hatuna ajira na wakati ajira zipo za kuwaajiri ndugu zetu, hapa wanakuja watu na meli wanatuibia samaki wetu ikisha wanakwenda kufaidika wao, sisi wenyewe tuliokuwa na mali hapa tunatizamana tu. Kwa hivyo, ninaiomba serikali ibadilike ione kama sasa huku kwenye bahari kuna ajira za kuwaajiri ndugu zetu.

Mhe. Spika, zikiletwa meli tatu tu hapa basi watafaidika ndugu zetu kupata ajira katika meli hizo, lakini zinakuja meli za kigeni zinatuibia samaki sisi wenyewe tumekaa tu hapa. Mhe. Spika, naiomba serikali umefika wakati sasa ione kama na huku kuna ajira Mhe. Jadi amesema hapa kwamba baada ya kula wali ukatoelea samaki sasa utakula samaki utoelee wali. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hili nalo alifanyie kazi tunapokuja hapa tukipiga kelele hizi kelele zetu tunazopiga zizae matunda tuone kama sasa wakati umefika.

Mhe. Spika, sasa niingie katika sehemu ya mazingira ni kwamba mazingira serikali naiomba ione kama na hiyo ni moja inayochangia uharibifu wa mazingira. Mhe. Spika, kwa sababu mimi nakubali kwamba pahali popote pale unapotaka uzuri lazima uzurike na siku zote faida ina na hasara zake. Mhe. Spika, kwa maana hiyo sisi tunataka faida ya kupata barabara nzuri lakini barabara hatuwezi kuzipata mpaka fusi, mawe na tupate na mengine.

Kwa hivyo, serikali inapowapa wale kampuni kuchimba fusi lazima iwalazimishe kama baada ya kwisha kuchimba basi wafukie hata kama ile ardhi hairudi tena kama mwanzo. Lakini kama watafukia kidogo ile hali inakuwa ni ya kuridhisha, lakini ukiangalia kama kule Micheweni tusiwalaumu wananchi kama wanachimba mawe, ndio wananchi wanachimba lakini na serikali nayo inachimba.

Mhe. Spika, hebu tuangalie ile sehemu aliyochimba *COGEFAR* kule Micheweni tangu mwaka huo mpaka leo ukifika kule lile shimo linatisha. Kwa hivyo, naomba tukitia mikataba na makampuni lazima sharti hili ya kwamba wakishakuchimba warudisha japo ardhi haitorudi kama mwanzo lakini itakuwa haiwi kama inavyokuwa hilo shimo. Mhe. Spika, naiomba serikali ikianza kutia mkazo juu ya hilo ndio wananchi tutapata kuwaelimisha kwamba tusiharibu mazingira.

Mhe. Spika, sasa niingie kwenye misitu, ni moja ya faida ambayo inarutubisha nchi na inaleta faida kwa wananchi na kwa serikali wenyewe. Kwa hivyo, naomba wahusika wa Idara ya Misitu waisimamie vizuri hii misitu kwa sababu misitu kukatwa katwa ovyo ovyo ndio inakufa na kumalizika. Kwa hivyo, wasimamizi wakuu wa misitu ni Idara ya Misitu wenyewe, lakini kwenye idara hii kunakuwa na kamati ndogo ndogo za kuhifadhi misitu.

Mhe. Spika, kama kule Micheweni msitu uliokuwepo kule wale watu waliokuwepo kwenye vijiji vyenye misitu kuna kamati ambazo zinasimamia. Lakini naiomba serikali kupitia hiyo Idara ya Misitu na Mazingira zile kamati ambazo huwa tumeziunda zinazosimamia na kulinda misitu kidogo tuzipe motisha, tusiwalipe lakini tuwape motisha ili wawe na nguvu za kuihifadhi ile misitu.

Mhe. Spika, kamati zilizoko kule Micheweni mimi naamini kama zinafanya kazi kikamilifu, lakini hapa kipindi kilichopita nilichangia nikasema kwamba ili wale kuwapa nguvu na ile misitu isiharibike basi tuwape motisha, tusiwalipe mshahara lakini tuweke muda twende tukawape motisha, pia tuwapatie nguo za kuingilia mle msituni wakati wakwenda kulinda kwani mle mna miba inachoma.

Mhe. Spika, katika kipindi kilichopita msitu wa kule Micheweni nilisikia kukitoka tangazo kama kuna Jini, sasa Jini yule ikawa anakula watu lakini yule Jini alikuwa na watu kwa maneno sio kwa vitendo. Mhe. Spika, kumbe kulikuwa na watu wana habari zao wanataka kufanya, walipokwishafanikiwa Jini alihama.

Mhe. Spika, mle kwenye msitu wa Micheweni mna mivule mingi sana badala ya watu walipokwisha kuiba mivule basi Jini huyo alihama moja kwa moja. Kwa hivyo, naiomba serikali kupitia hizo kamati mzipe motisha basi majini hao watahama wote. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi kuchangia machache katika hotuba hii ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira. Mhe. Spika, wizara hii ni muhimu sana kwa sababu wale wote ambao wamekosa ajira rasmi kimbilio lao sasa hivi ni wizara hii.

Kwa kweli imechukua mahitaji ya wananchi wetu wengi wale walioajiriwa na Mhe. Dk. Mwinyi serikalini ni asilimia ndogo sana, waliobakia wote wanaingia katika wizara hii kujitafutia rizki.

Mhe. Spika, mimi nianze na uvuvi wenzangu wameanza hii na mimi naomba nianze hapa hapa. Mhe. Spika, wenzetu wa Bara wana msemo wanaita "kilimo kwanza". Mimi ningeiomba serikali hapa Zanzibar msemo wetu uwe uvuvi kwanza. Wale wanasema vile kwa sababu wana ardhi kubwa sana, sisi ardhi kubwa hatuna lakini tuna bahari kubwa sana. Kwa hivyo, tusiwaige maana tunapenda sana kuiga sisi, si kauli tu lakini hata kibajeti tuelekeze huko tuone kwamba bajeti yetu sasa imeelekeza zaidi katika suala la uvuvi.

Mhe. Spika, kupitia uvuvi tu kwa mazingira ya nchi yetu ndio ambapo uchumi wa visiwa hivi utanonoka sana. Kwa hivyo, mimi nasifu jitihada za waziri kupitia kwa Mkurugenzi wake na Idara nzima ya Uvuvi shughuli wanazofanya, lakini wanahitaji kubadilika sana kuona kwamba jitihada zao wanazofanya zinalenga kuona tunajibadilisha ili tuone kwamba shughuli za uvuvi zinaubadilisha uchumi wa Zanzibar hasa.

Mhe. Spika, mfumko wa bei Zanzibar unachangiwa sana na uagizaji wa chakula lakini zaidi mchele. Sasa tungekuwa makini na tungejipanga mapema kabla, Sekta ya Uvuvi ingesaidia sana kupunguza *inflation* hapa Zanzibar.

Wenzangu wamesema hapa na ni kweli tumezoea kula wali kwa samaki au shelisheli kwa pweza. Sasa tungeweza kubadilika tukasema sasa tuleni kweza kwa shelisheli. Wenzangu wa Donge na Gando hali hii ingewasaidia sana. lakini sasa bado tunapiga shelisheli kwa pweza ndio hilo hilo. Basi tubadili tuleni kamba kwa muhogo au tuleni kombe kwa sembe. Sasa kile ambacho tunakiagizia kitakuwa kidogo na miili yetu itajengeka kiafya, lakini leo tunakula *starch* kila mmoja ana kitambi badala ya kula *protein* ambayo tunayo imetuzunguka sana.

Sasa ushauri wangu ni kwamba hili ni jambo muhimu sana. Katika hili ningeshauri serikali ama isomeshe watu katika fani ya *home economic* sidhani kama tunao wengi. Lakini nchi makini hili somo wanalipa kipaumbele sana kwa sababu linahusiana zaidi na masuala ya *house holding community consumption.* Sisi tunapuuza hili, lakini ukisomesha wataalamu katika fani hii wanajaribu kuhakikisha kwamba zao ambalo linatoka nchini ndio linatumika na watu wengi.

Sisi hatuzalishi mchele mwingi lakini katika nafsi zetu kila mtu anapenda kula wali. Lakini tunazalisha kwa mujibu wa Mhe. Waziri humu kwenye kitabu chake tunazalisha muhogo mwingi sana. tunazalisha vitamu na vikuu vingi sana, lakini ile *mind set* yetu ni kwamba vile si vyakula vya kula, sasa kila mmoja anataka kula wali. Nafikiria tungebadilika kuona kwamba tunabadilika kuwa vyakula

vinavyozalishwa ndani ndivyo ambavyo tunavitumia vikisaidiwa na vitoweo ambayo tunavyo vingi sana. hilo ni la kwanza.

La pili, katika ukurasa wa 6 kuna takwimu za uvunaji wa samaki, mwaka 2009 ilikuwa ni tani 25,000. Sasa ukiziangalia hivi hivi tani 25 elfu ni nyingi, lakini ukizipigia mahesabu maana yake hizi ni kilogramu 25 milioni kwa mwaka. Ukigawa kwa watu milioni moja tu wa Zanzibar, maana yake ni kwamba kilogramu 25 kwa kila mtu kwa mwaka, *catch* yetu ya samaki . Ukigawa kwa miezi 12 ni kama kilogramu 2 kwa mtu kwa mwezi, sas kwa mazingira ya Zanzibar ilivyo haya kwa kweli hayajawa mafanikio ya kujivunia hata kidogo.

Ukamataji wetu wa samaki kwa mwaka ulikuwa kilo mbili kwa mtu kwa mwezi mafanikio madogo. Nchi hii imezungukwa na bahari sana, sasa ikiwa hii ndio *achievement* ambayo imekuja baada ya *investment* hii ya 1.8 bilioni ambapo Mhe. Waziri amesema vifaa vya uvuvi vimetolewa kwa kwali tuna kazi kubwa sana ya kufanya. Mimi nashauri Mhe. Spika, serikali sera tubadilishe kuona kwamba masuala yanayohusiana na mambo ya uvuvi hayawekewi *selling* na yatafutiwe fedha za kutosha kuona kuwa Mkurugenzi na watu wake utaalamu wao walionao umeweza kuisaidia nchi sana.

Mhe. Spika, eneo jingine ambalo nilizungumze ni *data* za Mhe. Waziri katika kitabu chake, ukiziangalia ni nzuri. Ukurasa wa 5-6 anatupa *data* za ongezeko la uzalishaji. Mimi nampongeza kwa hilo, lakini bahati mbaya sasa, *data* zake hazitupi kipimo cha kujitathmini. Kwa mfano, mpunga mwaka 2008 tulipata tani 20,569 na mwaka uliopita tulipata 26,962.

Mimi nahisi angetusaidia sana kama angetuambia lengo la kujitosheleza ni lipi *from there* tukajua tuna safari ndefu kiasi gani ya kuifikia. Lakini akitupa hivi anatuvungavunga kidogo hatujui sisi tuna tatizo kiasi gani. Pengine mtu anaweza akasema labda ni tani 30,000 ndio tumejitosheleza, lakini angetuambai kwamba lengo la kujitosheleza kwa wananchi wa Zanzibar kwa 1.2 milioni hivi sasa labda ni tani fulani.

Muhogo ametuambia tulitoka kutoka tani 149,000 mpaka 195,000. ni mchupo mzuri lakini pia hajatuambia lengo la kujitosheleza kwa muhogo hapa Zanzibar tukifikia tani kiasi gani tutakuwa tumevuka lengo na jengine labda tuzisarifu vipi, tuzifanye vipi, tuziuze wapi. Nafikiri hizi ni *data* ambazo sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi tungepewa zingeweza kutusaidia sana. Lakini *the way* ambavyo ametupa kwa kweli hazitusaidii kuweza kutathmini lengo letu na tufanyeje au tu-*invest* kiasi gani ili kufikia lengo. Angeweza kutuambia sisi kama Wajumbe wa Baraza tungelishauri serikali kuona kwamba malengo ambayo Mhe. Waziri tuna pengo pana viwango hujavifikia, tungeweza kusema. Lakini hivi ambavyo umeiweka umetuweka kizani.

Mhe. Spika, naomba pia nirudi tena kwenye uvuvi, kwamba wenzetu sio tu wana-*hunt* samaki, lakini wanafuga. Sisi Mhe. Waziri katika kitabu chake ametuambia kwamba kuna maeneo mawili matatu ambayo ufugaji wa samaki umeanza. Nafikiri hili ni suala la kulipa kipaumbele sana, sio tu kuwa tuende baharini lakini tukifanya jitihada tunaweza kupata samaki katika maeneo ya karibu.

Kule jimboni kwangu kuna kijiji kimoja kinaitwa Chozi Shehia ya Ukinjwi, wana eneo zuri, wamejitahidi kuomba angalau *know how* ya ufugaji wa samaki lakini bado hawajafanikiwa. Ningemuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwa Mkurugenzi wake aone kwamba hawa wananchi wa Kijiji cha Chozi wana hamu sana na taaluma ya ufugaji wa samaki. Wana eneo zuri wamelitenga kwa ajili ya kazi hiyo.

Sambamba na hilo Mhe. Spika, ni jambo la ajabu kwamba hadi leo Zanzibar inaagizia chumvi na hapa ni jambo la kujilaumu sana. Iweje bahari yote inayotuzunguka hii, maeneo yote ya uzalishaji wa chumvi tuone katika maduka kuna chumvi kutoka Mombasa na kwengine isiwe Rwanda na Burundi. Kwa sababu Rwanda na Burundi kuagizia chumvi sana hawana bahari, lakini hata sisi jamani? Nafikiri hapa serikali iangalie tutafanyaje. Kuna wananchi wamejitahidi katika hili wanahitaji kuwa *promoted* ili kuona hatimaye hatuwezi kuendelea kuagizia chumvi. Kwa kweli haya ni mambo ya aibu.

Eneo jengine ambalo naomba nilizungumza ni ukulima wa mikarafuu. Mhe. Spika, hapa na mimi ningeiomba serikali kupitia kwa waziri atafute mradi wa maana kuona kuwa mikarafuu imeimarishwa. Vijisenti vya shilingi milioni sitini anavyopata kwa mwaka kwa kweli havilengi kuona kwamba mradi huu unaimarika. Kwa kweli ni pesa ndogo haliwezi kuwa zao la nchi linatengewa pesa hizi ndogo, hizi ni pesa chache sana.

Jingine kule Pemba kitengo cha mbegu kiko dhaifu kidogo *facilities* zake ni chache na ningemuomba Mhe. Waziri akipe msukumo kidogo vitengo hivi ni muhimu sana katika nchi. Hatuwezi kuendelea kuagizaagiza mbegu kutoka nje. Mambo haya yanaturejesha nyuma sana. Sasa kwa vile kiko kitengo, vijana wako lakini hakina *facilities.* Basi ningemuomba Mhe. Waziri akisaidie kuona kwamba kinaweza kufanya kazi zake na kufanya utafiti wa namna gani kuweza kupata mbegu nzuri itayoweza kujitosheleza ndani.

Naomba pia ombi langu la mwaka jana la kwamba Chuo cha Kizimbani kiwe na tawi Pemba Mhe. Waziri alisikilize. Lakini pia mara hii nitakuwa mgumu kidogo katika bajeti ya Idara ya Mipango kuhusiana na hadhi za Karakana ya Matrekta. Hii ni mara ya nne nasimama katika Baraza hili kumuomba waziri sasa atupe *vision* ya serikali kuhusiana na *status* ya Karakana hizi. Kwa kweli kila mwaka

tunapewa ahadi lakini hatuoni mafanikio. Sasa kama Mhe. Waziri mtu mzima sana na ninamuheshimu sana na kwa kweli sipendi nimhangaishe, naomba asaidiwe kunipa majibu ya maana katika suala hili, vyenginevyo nitalazimika kupiga buti katika suala la Idara ya Mipango.

Naomba pia nizungumze suala la misitu. Mhe. Spika, misitu ni kweli inatoweka sana na kwa kweli hapa napo tunahitajika kubadilisha sera na sheria ziwe makini sana. Vyenginevyo baada ya muda Zanzibar itakuwa jangwa kama maeneo mengine. Matumizi ya kuni hatuwezi kuyadhibiti kwa sababu mtu hawezi kukaa bila ya kupika. Ni bahati mbaya sana umeme unakuwa ghali na umeme kuwa ghali mtu hawezi kutumia *cooker* lazima ata-*opt* kwenye makaa huo ndio ukweli wenyewe au kwenye kuni. Huwezi kumwambia mtu mbona unakata kuni afanyeje na watoto wanataka kula. Sasa umeme ghali na serikali haijawa na sera ya kutumia gesi.

Wenzetu wanachukua gesi *miles and miles*, kilomita kwa kilomita kutoka nchi nyengine kwenda nchi nyengine. Tunaambiwa gesi inatoka Russia inakwenda Western Europe kwa sababu watu wanataka kuchunga mazingira. Wengine hutumia meli wanachukua gesi kutoka inakozalishwa wanakuja katika nchi zao ili watu wapate nishati nzuri ya kupikia. Sisi serikali kwa kweli haijaliona hilo na kuacha hilo maana yake ni kuwaambia watu wakate kuni, hatuwezi kuwazuia.

Ningeiomba serikali hili ni la sera si la waziri *per see* lakini yeye kama waziri mhusika anaweza aka-*lobby* serikalini kwa sababu ni *part and percel* ya hili kuona kwamba sera ya matumizi ya nishati haiathiri misitu ambayo tunayo, vyenginevyo akilegalega katika hili baada ya muda wa miaka mitatu ijayo kwa kweli kila kilima cha Pemba kitakuwa kipara hakitakuwa na juu tena.

Mhe. Spika, naomba nimalizie na suala la *irrigation*. Naona unanitizama na najua unanitizama kwa sababu gani. Kwa hivyo, Mhe. Waziri Kiongozi mara nyingi huwa anazungumzia *irrigation master plan*, bila ya hii tutakwama sana. kwa hivyo, tutafuteni uwezo wa kuona mabonde yote ya *irrigation* yaliyowekwa yanatafutiwa uwezo, ukulima wa *irrigation* unapewa kipaumbele.

Kuna wataalamu wazuri wa *irrigation* nchini mwetu, wahandisi wa kila aina wapo wanafanya kazi vizuri. Wanafanya jitihada kubwa, lakini bajeti yao inakuwa fupi hatuwezi kuwalaumu. Ningemuomba Mhe. Waziri kuna mambo bila ya kuyatilia mkazo sana kwa kweli tunaweza tukakwama sana.

Wenzangu wanalaumu kwamba bajeti iko Kibokwa na Bumbwisudi, ni sawa kwa sababu hali halisi hatuwezi kwa kidogo tulichonacho kuenea kwa muda, lakini tujitahidini kidogo. Bahati nzuri Pemba sasa tumepata umeme. Kwa hivyo sasa ni wakati na *irrigation pump* kuwa *mechanized*. Kwa sababu Pemba ni nusu

irrigation nusu mvua yaani ukulima wa kutegemea mvua, bila ya mvua hakuna *irrigation* kwa sababu hatuna *pump irrigation* kule, nafikiri kwa kuwa kulikuwa na tatizo la umeme siku nyingi. Umeme tunaishukuru serikali imeleta tunaiomba kwamba katika mabonde ya *irrigation* Pemba waanze shughuli za kupeleka miundombinu ya *mechanization*.

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa sababu wakati wako ni mdogo kuna mambo mengi ya kuyazungumza, lakini namalizia kwamba kama Mhe. Waziri atanijibu majibu yanayohusiana na hadhi za Karakana ya Matrekta, basi hivi sasa naunga mkono hoja kwa asilimia tisini, asilimia kumi *pending* majibu yake. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Haji Faki Shaali: Nakushukuru na mimi kunipa fursa hii ya kumpa baraka mzee wetu wa Baraza Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira kwa kusema machache katika hotuba yake.

Kwanza Mhe. Spika, moja kwa moja mimi nitakwenda katika ukurasa wa 52 ambapo panazungumziwa takwimu za uzalishaji wa mazao kwa tani, mwaka 2008/2009. Hapa Mhe. Spika, nina maswali nataka Mhe. Waziri anielimishe. Kwanza takwimu hizi wamezipata wapi? Ni za kukisia, za uhadithia au vipi? Kwa sababu mimi kwa mfano katika Jimbo langu la Mkanyageni, wananchi wanalima mihogo, mpunga na ndizi. Nyengine zinaliwa ndani ya jimbo na nyengine zinasafirishwa lakini sijaona pahala hata pamoja penye kituo cha kupimia mazao haya.

Hata hapa Marikiti Kuu Unguja ambapo vijana wengi wa Kipemba wanakuja wakiuza ndizi, sifikirii kwamba pana mizani za kupimia mazao. Sasa hizi zinapimwa au zinakadiriwa kwa utaratibu gani? Nina wasi wasi sana na hizi takwimu kwamba ni *cooked data* kwa sababu sioni harakati zozote zile za kitaalamu au hata zisizokuwa za kitaalamu za kuona kufuatilia hizi takwimu. Sasa labda wenzetu watwambie utaalamu gani mpya uliozuka duniani wanaotumia wa kupata hizi takwimu au vigezo wanavyotumia kama wanavyo, watatwambia. Hilo lilikuwa la kwanza.

Lakini la pili, mimi nataka nimpongeze Mhe. Waziri na waliofuatia kabla yake. Wizara hii mimi nasema ina bahati tokea ilipoanzishwa mpaka leo kwa jambo moja, kuelimisha watu. Wizara hii inajitahidi sana kila mwaka kupeleka vijana nje kwenda kusoma.

Nafikiri ukiondoa Wizara ya Elimu sina uhakika yupi atamshinda mwenzake lakini kwa *average* mimi nafikiri wizara hii imeweza kuwa ni *number one* kwa wataalamu wengi. Kwa maana ya watu wenye *PhD*, wenye shahada ya pili, wenye shahada ya kwanza, basi wizara hii imesheheni.

Tatizo lao ni moja tu kwamba wengi wao ni watawala au ni warasimu ambao wamo afisini, kwenye *field* ni wachache. Ndio pale utaona kwamba ile *input* haionekani, *output* haipatikani lakini wasomi wanao. Sasa wasomi wao wote karibu *almost* ni warasimu wa dola wamo maofisini kufanya mambo ya utawala katika *field* hawako.

Mimi nadhani tungebadili huu mfumo watu wakavutika kwenda huko kwenye *field* kuliko kukaa ofisini kwenye *air condition.* Nadhani tukibadili mfumo wa utumishi kwa wizara hii watu watatoka ofisini watakimbilia, lakini sasa hivi wasomi wa kilimo wote kila mmoja anatafuta pahala penye *air condition* anajiweka anabuni mradi na yeye apate maslahi *finish*.

Halafu Mhe. Spika, jengine nataka nirudi nyuma kidogo ukurasa wa 4 ambapo waziri kazungumza mafanikio ya ilani yake ya CCM. Nampongeza kwa mafanikio aliyoyataja, kayataja mengi lakini mimi sitaki niyarudie yote. Moja katika fanikio alilolizungumza Mhe. Omar Ali Jadi ambaye anataka wanyama wapatiwe *condom*. Alizungumza kwamba kuna uvumbuzi wa mbegu za kisasa tatu za mpunga na nne za muhogo ambazo zina sifa ya kuhimili maradhi, ukame na uzalishaji mkubwa.

Mhe. Spika, na mimi suala langu mara ya pili au ya tatu leo kuuliza, mbegu hizi zinaishia wapi? Kwa sababu mimi ni mkulima, si mkulima kwa maana ya kukamata jembe sasa hivi nikenda nikachezea mraba ata, lakini mashamba ninayo. Mashamba ya mihogo ninayo, ya mpunga ninayo, sijapatapo mimi kuona wataalamu wanatuletea hizi mbegu za muhogo na mbegu tulizonazo sasa hivi huyo mwari keshachoka tena. Kila mbegu tunayotafuta siku mbili tatu maradhi tayari haifai. Sasa hizi mbegu na sisi tunasema zinaishia wapi baada ya kuzalishwa hizi mpya?

Hata mipunga naona kule kwetu bado watu wanalima mbegu zao zile zile. Sasa Mhe. Waziri hebu twambie hizi mbegu mpya ni wilaya gani zinakopelekwa hata ikawa kwenye wilaya zetu sisi wengine hazifiki? Hilo lilikuwa ni swali ambalo nilitaka kuliuliza.

Jengine hili ni pongezi, kwa sababu mimi nilikuwepo Kamati ya Fedha na Uchumi muda mrefu nilikuwa namuona mwenzangu, ndugu yangu Kassim kila siku akitushitakia habari ya huu mtambo wa *liquid nitrogen.* Sasa Mhe. Waziri kauweza kautafuta hiyo pongezi Mhe. Spika. Mtu anapofanya zuri lazima asifiwe na atapokuwa hajafanya mazuri lazima tumuulize maswali atusaidie.

Hili kwa kweli ni la kupongeza kwa sababu vijana walikuwa wanasononeka na hata wakulima walisononeka kwa sababu zile mbegu za kutoka Arusha wanasema hata wakipigwa sindano wale ndama wengi walikuwa wanakufa.

Lakini hapa nafikiri itakuwa haina muda mfupi sana, nafikiri zitakuwa mbegu zile zina usalama. Kwa hivyo, hilo ni jambo la kupongezwa. Katika mafanikio hayo mimi kwa kweli niliona lazima nikupongeze.

Mhe. Spika, jengine katika mafanikio umesema kuna ujenzi wa maabara ya usafirishaji wa mazao. Hii maabara kwanza Mhe. Waziri mimi ningependa anambie iko wapi? Imeaanza kusarifu mazao gani? Kwa sababu siku hizi Mhe. Spika, machungwa mengi Unguja, linauzwa chungwa kama kichwa shilingi 50 tena unamenyewa kabisa, najua ukija msimu wa maembe ndio hivyo hivyo, utaikuta embe ya Muyuni ya kuuzwa shilingi 500 unainunua shilingi 150.

Sasa mazao gani yanayosarifiwa hivi sasa na kiwanda hicho kiko wapi. Kwa sababu hii ni habari njema lakini ndio tunaona ukienda Marikiti mazao yanaozeana, ukipita mitaani yanaozeana na huku tunaambiwa tayari tuna mambo ya kusarifu. Sasa labda kama hapa hatukufahamu naomba Mhe. Waziri utupe ufafanuzi zaidi.

Halafu nataka nizungumzie juu ya mipango ya kilimo. Mhe. Spika, mimi naona kilimo kuna mipango mingi na mingine inanichanganya. Ukiangalia ukurasa wa kwanza kuna Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe, halafu kuna Mkakati wa Mageuzi ya Kilimo, kuna Programu ya Kuendeleza Huduma za Kilimo. Sasa haya mambo matatu ukiangalia yote malengo yake ni mamoja, yote ni kuondoa umaskini kwa kilimo na kuhakikisha tuna chakula cha kutosha.

Mimi nafikiri hizi programu na mipango mingine inatia wasiwasi. Kwa nini tuanzishe tuwe na programu nyingi zenye lengo moja kwa sababu ukiangalia huo unaoitwa mkakati wa mageuzi ya kilimo, sera ya uhakika wa chakula na lishe, programu ya kuendeleza huduma za kilimo, Wallahi *difference* ndogo sana ni usanii tu wa maneno ndio utakaokuwa unatofautiana, lakini lengo kuu ndio lile lile, malengo mahususi ndio yale yale.

Sasa mimi nasema lazima tufike pahala tuache ujanja wa kufanya programu nyingi kama hizi ambazo tija haipo. Ni bora kuwa na programu moja au mbili tukazisimamia kwa ukweli lakini hizi nyengine naona ni programu za ubababishaji. Haya ni mambo ambayo mimi hata akilini nashindwa kuyafahamu vizuri. Miradi mingine inaeleweka kwa sababu ni miradi *independent,* kila kitu kinazungumzia mambo mahususi nafahamu, lakini hii mitatu naona yote inazungumzia kitu kimoja, baba mmoja mama mmoja.

Halafu Mhe. Spika, jengine nataka niulize swali moja katika haya mambo ya chakula na matunda. Mhe. Waziri sijui wizara imefanya utafiti kiasi gani ya matunda tunayokula yanayozalishwa Zanzibar na kiasi gani yanatoka Tanzania Bara?

Nakumbuka kuna mchangiaji mmoja alipokuwa akichangia hotuba ya serikali alisema kwamba alikwenda Soko Kuu la Mwanakwerekwe, lakini muono wake wa haraka haraka alilogundua kwamba mazao mengi yanayouzwa pale hata yale yanayotangazwa asubuhi katika redio ya *Zenji FM* bei za mazao kutoka sokoni mengi yao huwa yanatoka Tanzania Bara. Sasa sijui waziri mmefanya utafiti kuona mazao yanayouzwa pale sokoni yepi mengi, ni yanayozalishwa Zanzibar, nakusudia Unguja na Pemba au ni yale yanayotoka Tanganyika? Na mmeweza kulidhibiti vipi soko la ndani.

Kwa sababu sasa hivi hakuna tena mambo ya *monopoly* katika *market* kwenye nchi yetu. Lakini kwa wenzetu yapo angalau kuna mambo mengine unaweza ukaambiwa mfanyabiashara *stop* kwa sababu sasa hivi kwa machungwa yalioko Zanzibar ukaruhusu tena watu kuingiza machungwa kutoka Muhenza unakuwa wewe unauwa kilimo chako cha michungwa. Na mambo haya hakuna pahala ambapo hayafanyiki bwana, haidhuru ni biashara huria lakini mambo haya popote yapo.

Tanganyika hapo sasa hivi ukipeleka saruji kutoka nje hawakubali wanakwambia wanalinda viwanda vyao, na kuna baadhi ya vitu ukipeleka hawakubali wanakwambia wanalinda viwanda vyao. Uyatoe hapa Zanzibar ukipeleka unaambiwa tunalinda viwanda, maji hayatakiwi ukifika unaambiwa tunalinda viwanda vyetu vya Dasani na Kilimanjaro. Wewe kayapeleke maji ya *Drop* au *Zanzibar Kool* hawana haja nayo. Sasa nafikiri na sisi kuna haja ya kuwalinda wakulima wetu unapofika msimu kama huu angalau yale mazao yao wasiuze chungwa moja shilingi 50 au mfuko mzima shilingi 500, nadhani mambo mengine mimi nafikiri yanawezekana.

Jengine nataka nizungumzie mradi wa uimarishaji karafuu ambao mwaka jana uliombewa shilingi 60 milioni. Mhe. Spika, ikiwa tunasema kilimo ndio uti wa mgongo na mimi naamini kwamba kilimo ndio uti wa mgongo kwa sababu kama utafanya utafiti wa kisayansi watu wengi bado wanaajiriwa katika sekta ya kilimo, sekta ya utalii inaajiri watu wengi kutoka Tanganyika, lakini Wazanzibari hasa kwa maana ya Muunguja na Mpemba bado wengi wanaajiriwa na sekta ya kilimo kwa njia moja au nyengine, ama kwa kulima yeye au kwa kuwa *middle man* kununua ndizi kwa wakulima akaja akauza sokoni au utamkuta kijana sokoni anauza ndizi mtu wa tatu. Sasa ukimchukua mtu anayeuza bidhaa sokoni yule *middle man* anayechukua kutoka kwa mkulima akaleta sokoni na mkulima, hawa ni *population* kubwa.

Kwa hivyo, mimi nasema bado kilimo ndio kinachomuajiri mkubwa na hasa hiki cha karafuu ndicho kinachotuletea fedha za kigeni. Lakini kweli jamani shilingi 60 milioni mradi kama huu ushindwe na mradi wa paka na mbwa? Kwa sababu mambo mengine kwa kweli inakuwa hayaoneshi kuwa kweli tumekusudia

kufanya kitu. Hizo shilingi 60 milioni wakapata shilingi 35 milioni tu sawa na asilimia 58. Kwa maana hiyo bado Mhe. Spika, mimi siridhiki kabisa na hatua zinazochukuliwa katika kuimarisha kilimo.

Tunaambiwa kwamba kuna sensa ya kilimo itafanyika, sijui sensa hii itafanyika vipi labda atusaidie. Mnakwenda kuhesabu mkarafuu mmoja mmoja mabondeni au mnawafuata wakulima kila mkulima atoe takwimu za miti aliyonayo? Maana sifikirii sasa hivi mtaalamu kumtia porini atakuja na hesabu ya uongo, kwa sababu mashamba mengine hayaingiliki kwa miti yenye miba hasa zile eka, kwa hivyo haihesabiki. Sasa sijui sensa hii mtaifanya vipi kupata takwimu sahihi za mikarafuu.

Jengine Mhe. Spika, mimi naona kama utani katika mradi huu. Naona kuna *component* ya kutoa mafunzo ya uvunaji na uanikaji wa karafuu. Hivyo mtu wa Donge na Mpemba anafundishwa kuchuma na kuanika karafuu? Hiki si kichekesho? Hizi *component* nyengine naona kama ni kichekesho.

Halafu kuna bidhaa tunaambiwa watu watafundishwa kusindika zitokanazo na karafuu, ni bidhaa gani? Pemba wanawake wanayo bidhaa wanaisindika kutokana na karafuu wanazijua mama zetu, ndio hii iliyokusudiwa au kuna bidhaa nyengine? Kwa sababu najua karafuu Pemba watu husindika na kutumia kwa dawa, kwa mababa zetu kusuguwana suguwana, ndio hii iliyokusudiwa au nyengine? *(Kicheko).*

Mhe. Spika: Hivi Mhe. Haji Faki Shaali ulidhani hatukufahamu pale mwanzo? *(Kicheko).*

Mhe. Haji Faki Shaali: Halafu Mhe. Spika, katika ripoti ya maendeleo Mhe. Waziri kazungumza kitu kimoja *very sensitive*. Kasema kwamba kuna ripoti ya kila mwaka ya mfumo wa upatikanaji na matumizi ya chakula.

Mhe. Spika, mimi naomba atupatie nakala hii na sisi humu Barazani kama itawezekana kesho tuone hivyo ilivyotayarishwa, ikiwezekana wataalamu wake Katibu Mkuu madhali yupo aagize kesho vijana watuletee tuone hii *food balance sheet report* ya mwaka 2007 tuone hasa tujiridhishe kweli ilivyofanywa imefanywa vipi?

La mwisho Mhe. Spika, kwa sababu wakati unakimbia, nakuja pale pale na kilio changu cha Kisiwapanza kinavyoathirika na mazingira. Mhe. Spika, bado nasikitika sana kwamba Kisiwapanza inamalizwa na maji ya bahari. Ninaona vibaya mimi nafsi yangu kwamba wakati wa ukoloni tatizo hili lilitokea wakalidhibiti, walijenga ukuta maji wakayazuia ile sehemu kubwa ikawa watu wanalima.

Sasa wananchi ukienda kule wanasema aah, jamaa hawa wakoloni wakorofi walitusaidia hii serikali yetu wenyewe kwa sababu walikuwa wana Afro Shirazi watu wa Kisiwapanza wote. Kisiwapanza kulikuwa na Hizbu 11 tu, lakini wanasikitika mbona hawa wakoloni wakorofi walituweza kutufanyia hivi, mbona hii serikali yetu haitufanyii hivi?

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Mhe. Haji Faki unajua takwimu za mbali kweli kweli, historia hasa. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe, tunakushukuru Mhe. Haji Faki kwa mchango wako. Sasa niahirishe kikao hiki hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mohamed Ali Salim: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya mwanzo jioni hii kuchangia Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira. Mhe. Namshukuru Allah kwa kutuwezesha saa hizi kufanya kazi hii muhimu.

Mhe. Spika, moja kwa moja kwa sababu muda ni mfupi mno naomba nianze kwa suala zima la kilimo. Mhe. Spika, labda kwanza niungane na Mhe. Haji Faki Shaali juu ya suala la upimaji wa mazao. Kwa kweli suala hili Mhe. Spika, kwetu sisi ni kitendawili kwa sababu hatujapata kuona hata siku moja sehemu zote tunazokaa na sehemu zote tunazotembea kukuta kuna pahala popote pale ambapo mazao ya kilimo yanapimwa. Lakini tukija Barazani miaka yote tunapewa takwimu za mazao yaliyozalishwa ya kilimo.

Mhe. Spika, mimi mwenyewe nina mashamba ya mpunga, muhogo, migomba, lakini hata siku moja ndizi zangu ninazovuna hazijapimwa, wala mpunga ninaovuna haujapimwa, wala muhogo ninaovuna haujapimwa. Au katika hesabu hizi vyangu mimi havimo.

Mhe. Spika, naomba tupewe ufafanuzi labda huu upimaji unafanywa namna gani, ili tuelewe na sisi siku ya pili kama Wajumbe wa Baraza hili tuweze kujua jinsi gani vipimo vinavyofanywa.

Mhe. Spika, jengine kwa kusema kweli bado kilimo chetu pamoja na kuwa bajeti ya mwaka jana ilikuwa ya miundombinu ya kilimo na utalii, lakini bado miundombinu ya kilimo na utalii haikuweza kuimarishwa mwaka jana angalau mwaka huu tukasema tumefikia pahala pazuri.

Kwa sababu miongoni mwa mambo ambayo yanatendeka ni watu kulima kwa kijembe cha mkono. Mhe. Spika, mimi ninavyojua katika jimbo langu lote watu wanalima kwa kijembe cha mkono muhogo, migomba na mambo mengine. Sasa tukija kwenye suala la mpunga wanapata trekta mara moja tena kwa kuchelewa, yaani wanachimbuliwa tu wakawekewa yale madongo makubwa basi, halirudii tena trekta hilo kuja kuvuruga. Wakati kuna sehemu nyengine kwa wenzetu wanalimiwa, wanavurugiwa.

Mhe. Spika, ukija kwenye suala la dawa ya magugu ndio kabisa haionekani. Sasa ni miundombinu gani iliyotayarishwa katika mwaka uliopita. Mhe. Spika, hili naomba tuelezwe na miundombinu hiyo imejengwa upande gani. Isijekuwa kuna sehemu imejengwa hiyo miundombinu lakini sehemu zetu sisi wengine haijafika bado.

Sasa Mhe. Spika, mimi nashukuru sana kuwa wizara ina wataalam wa kutosha. Ninaamini wataalam hawa kama wangelikuwa wanakwenda kwa wakulima wao wenyewe wakaonana na wakulima, wakawafundisha wakulima jinsi ya kulima, mimi ninaamini tungelikuwa na mazao hata pakuyaweka hatuna. Lakini bahati mbaya huambiwa kuna mabwana shamba, shambani kwangu sijamwona hata siku moja. Sasa sijui mabwana shamba hawa na mabibi shamba wanafanya kazi gani.

Lakini kiasi mabwana shamba na mabibi shamba wasiende mashamba kwa sababu hawana wakubwa wa kuwafuatilia ndani ya mashamba. Mtu yeyote aliyekuwa hafuatiliwi Mhe. Spika, hakuna mtu anayetaka kazi duniani, kila mtu anataka pesa, akishakupata pesa hana haja ya kufanya kazi. Ndio maana kama utamuajiri mtu akufanyie kazi ukampa pesa mwanzo basi hakufanyii kazi mtagombana tu mwisho wake. Hata fundi wa ushoni kama utampa pesa mwanzo kazi hakufanyii kwa sababu haja yake ni pesa sio kazi.

Kwa hivyo, hawa mabwana shamba na mabibi shamba haja yao ni pesa sio kazi. Ili wafanye kazi lazima wasimamiwe na wakubwa zao. Lakini mimi sijamwona hata mmoja katika hao na mimi ni mkulima kwa huko kwetu najulikana kidogo, Wambaa ninayo mashamba kidogo.

Mhe. Spika, kuna suala hili la umwagiliaji maji. Mhe. Spika, niliambiwa katika bonde langu la Makombeni pale kutakuwa na mradi wa umwagiliaji maji. Labda tu nielezwe leo mradi huu wa umwagiliaji maji umefikia wapi. Lakini pia Mhe. Spika, kuna suala la mbegu mpya zinazozalishwa. Kuna mpango gani wa kuzipata mbegu hizi mpya zinazozalishwa kama mtu anazitaka. Kwa sababu kwa huko ninakokaa mimi kwenye mashamba ya wakulima basi sijaziona hizo mbegu mpya. Kwa hivyo, tuelezwe hapa Barazani mtu akitaka hizo mbegu mpya afanye nini ndio atazipata, zinapatikana wapi.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi nilikuwa nataka nibadilishe hii habari ya maneno ya kutumia katika kilimo, tumeshatumia maneno mengi tu kama kilimo ni uti wa mgongo, kilimo kwanza. Mhe. Spika, mimi nafikiri sasa labda Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ingelijiandaa rasmi halafu ikatumia kauli badilisha kilimo. Lakini isiwe kauli iwe na vitendo vifuatie katika kubadilisha kilimo. Kilimo kibadilishwe, mtu kieneo kidogo alichonacho aweze kuvuna sana. Sasa hivi bado haijafikia hali hiyo.

Mhe. Spika, kazi anayoifanya mkulima na pato analolipata halilipi, pato ni dogo mno kuliko kazi anayoifanya. Mtu anaanza kulima mpunga anachukua miezi sita au zaidi, chakula anachokipata hakitimii hata mwezi mmoja. Sasa tunawafanya nini hawa wakulima.

Halafu Mhe. Spika, tunazungumzia mbolea, kuna mbole nyingi tu mbona. Mimi ninavyojua kila siku kule kwetu watu wanafyagia vibanda vya kuku mavi wanayatupa. Hivi Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira imeshawaelimisha hawa kuwa haya mavi ya kuku yakusanyeni baadae muyatumie kwa mbolea. Utakwenda katika wilaya nzima pengine kuna sehemu moja tu ndogo ndio watu wanaofundishwa pengine kulima migomba basi. Lakini ukenda sehemu nyengine zilizobaki zote zimekaa watu wanatupa mbolea bure, wakati mbolea ile wangeweza kuitumia katika kuzalisha zaidi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo labda niligusie kidogo tu suala zima la karafuu kwa sababu muda wangu naona kama unamalizika. Mhe. Spika, karafuu kwa mujibu wa kitabu cha Mhe. Waziri tunataka kufundishwa sasa kupanda mikarafuu, yaani kuchuma karafuu na kuanika karafuu. Labda niulize kuna mbinu mpya zilizogunduliwa za uchumaji na uanikaji wa karafuu. Kwa sababu kama kuna mbinu mpya basi si tatizo kuna haja ya kufundishwa, lakini kama tutakalofundishwa ni lile lile la kuweka jamvi chini ukazitawanya hili litakuwa halijawa na haja ya kufundishwa.

Mhe. Spika, nije kwenye mifugo. Mhe. Spika, mifugo nayo ina kazi kubwa. Kuna miradi hii imeanzishwa mingi tu ya mifugo ya ng'ombe, mbuzi, kuku na mambo mengine. Mhe. Spika, linalonisikitisha sana ni kupotezwa pesa ndani ya miradi hii, pesa zinapotezwa vibaya sana.

Mhe. Spika, najua Wambaa waliletwa ng'ombe, watu waliambiwa watapelekewa ng'ombe wenye mimba, watu wakaambiwa watapelekewa ng'ombe wa maziwa mengi, wamepelekewa vindama vilivyokuwa labda vimeachishwa karibuni tu hakuna mwenye mimba. Wenye mimba walikuwa wawili na wakachukua hao waliofuatana na wataalam kwenda kuchukua ng'ombe. Watu waliobaki wakapewa ng'ombe wadogo wadogo waliokonda dhaifu, hivi sasa kiasi cha wanane wameshakufa.

Mhe. Spika, la kusikitisha zaidi ni kuwa ng'ombe anaumwa wataalam wanapigiwa simu wanaambiwa kuna ng'ombe anaumwa wanajibu tutakuja. Zimepita siku mbili wakapigiwa tena simu ng'ombe jamani anaumwa, tutakuja. Zikapita siku mbili nyengine wakapigiwa simu ng'ombe ameshakufa. Sasa Mhe. Spika, hivi tunafanya nini, hivi hawa wataalam wote waliopo wanafanya nini kitu kama hicho.

Mhe. Spika, hili kwa kweli limeniuma sana na yaliyoniuma ni mambo mawili, kuwa waliokwenda kuwatafuta kule ng'ombe walikuwemo wataalam na wataalam wale ndio ambao ilikuwa wawaelekeze wananchi wanunue ng'ombe wa aina gani, lakini ng'ombe waliokuja hawafai.

Mhe. Spika, nikiacha suala hilo labda nigusie tu kidogo katika suala la uvuvi na liwe ndio jambo langu pengine litakuwa la mwisho kwa sababu ya muda. Mhe. Spika, uvuvi mpaka sasa kama walivyosema wengine bado hatujaupa stahili yake katika bajeti ya serikali na katika mipango ya nchi. Mhe. Spika, mpaka leo bado wavuvi wetu ni kama hawa wanaonekana kwenye kitabu hiki hapa nyuma. Sasa wavuvi wa aina hii watavua wapi na watavua nini, wanaokwenda kwa ngarawa hapa wamekalilia. Mitego yao ni mshipi na ndoana, kenda mbele atakuwa ana dema.

Mhe. Spika, hii itakuwa sasa jamani tunawasumbua watu bure halafu tumewazuilia yale maeneo yao waliyokuwa wakivua kwa sababu ya hifadhi. Maeneo waliyokuwa wakivua yale sasa hivi ni maeneo ya hifadhi. Kwa hivyo, lazima sasa hivi watoke kwenye maeneo yale waende katika maeneo ya mbali zaidi mbele. Watafikaje huko kwa ngarawa za aina hii, watafikaje huko waende wakavue masamaki hayo ninayoyasikia kuwa yanauzwa kwa milioni moja kama tulivyooneshwa humu kwenye kitabu. Kweli kuna mshipi wa kumvua samaki huyo wa milioni mia moja.

Mhe. Spika, mimi ninavyoona kuwa bado mpaka sasa hatujawa *serious* katika suala zima la uvuvi. Kama tutakuwa *serious* Mhe. Spika, mimi ninahakika hatuna haja ya kutafuta vianzio chungu nzima vya uchumi, uvuvi ungetosha kuwa uchumi wa kuongezea huu tulionao na tukaweza kufanya mambo yetu mbali mbali ndani ya nchi kama inavyostahiki.

Mhe. Spika, hili kwa kweli kuna haja serikali kuwawezesha wavuvi. Si kuwawezesha kuwapa vile vimashua wanavyopewa na vinyavu vile, kuwapa zile hawajenda bado kwenye maji hayo yanayotakiwa waende, zile haziwezi kuvua. Kutafutwe mambo yanayoweza kuwawezesha kufika huko kwenye samaki kama kunakotakiwa hivi sasa.

Mhe. Spika, kama haijajiandaa hivyo serikali kila siku tutakuja hapa tukipigishana kelele, mwaka huu ukija tunapigishana kelele zile zile, ukija mwaka mwengine tunapigishana kelele zile zile lakini hakuna jambo litakaloendelea. Mhe. Spika, mimi naomba wataalam waishauri vizuri serikali, wasiandae miradi kwa malengo ya kuwa kila mtu idara yake iwe na mradi, waandae miradi kwa ajili ya maendeleo ya nchi. Mhe. Spika, nakushukuru ahsante.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo kutoa mchango wangu kidogo katika bajeti hii ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira. Mhe. Spika, kwanza namshukuru *Allah* kwa kutuweka hai tukawa wazima na tukapata nafasi ya kuzungumza katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira mambo yote matatu yana uzito wa aina yake katika maisha ya binadamu, hasa maisha yetu ya Zanzibar. Kwa sababu ardhi tuliyonayo ni ndogo na ikichafuliwa hakuna marekebisho yanayoweza kufanyika kwa muda mrefu. Kwa hivyo, mambo matatu hayo kwenda sambamba ni mambo yanayohitaji uangalifu mkubwa na uwezo mkubwa.

Mhe. Spika, nikianza hapo nilikuwa napenda niseme kwamba kuna sehemu nyingi zimepiga hatua hususan katika miaka mitano hii ambayo mimi nilibahatika kuwa katika Kamati ya Fedha na Uchumi kwa hivyo tulikuwa tukitembelea wizara katika kila mwaka.

Mhe. Spika, kuweka miundombinu ya umwagiliaji, miradi ya uvuvi au ya hifadhi ya maeneo ya ukanda wa Zanzibar na Pemba *(MANCEP)*, miradi ya *PADEP*, ni moja katika mafanikio ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira katika kipindi hichi lakini ina changamoto kubwa. Kwa muda mrefu kulikuwa na kukosekana kwa mtambo huu wa *liquid nitrogen.*

Mhe. Spika, moja katika jambo ambalo napenda kuipongeza wizara yenyewe binafsi pamoja na Wizara ya Fedha ni kuweza kuona umuhimu wa mtambo huu na kutoa msukumo angalau katika kipindi hichi ukapatikana. Kwa hivyo, hii ni changamoto kwa wizara yenyewe na hasa Idara ya Mifugo kuona kwamba mtambo huu unatumika kwa uangalifu kutokana na hali ya bei yake ilivyo na unatoa tija zinazohitajika.

Lakini Mhe. Spika, changamoto ambazo wakati mwengine inakuwa zinasikitisha hasa kuonekana kwamba zinajirudia katika wizara hii la mwanzo ni suala zima la karakana tulizonazo mbili. Kwa kweli ikiwa wewe ni mwanakamati au ni mjumbe unayekwenda kutembelea kila baada ya muda utajikuta huamini kwamba mambo yale yanaweza yakatokezea na yakafanywa.

Mhe. Spika, mimi nilipata taarifa za watu wa karibu mafundi hawa wa magari walioziona zile karakana ule mwanzo wake zilipoanzishwa. Fundi ambaye anafanya kazi mpaka sasa hivi akikuelezea unaweza ukatokwa na machozi ukiziona karakana zile zilivyo sasa hivi. Kuna fani moja Mhe. Spika, inaitwa fani ya kuchonga, kwa kweli utaalam wake huu si rahisi kuupata. Hata kama Zanzibar tutasema kwamba vije vyombo vya binafsi lakini utaalam huu ni wa aina yake. Mhe. Spika, bado Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ina kigugumizi, ina kusita sita, haijulikani hasa kitu gani wanachokifanya.

Mhe. Spika, mimi naamini siku karakana zitakapokufa nakuhakikishia na kilimo kimemalizika Zanzibar hakuna trekta litakalotengenezwa kwa sababu karakana zina uwezo mkubwa wa kubuni zana ambazo zinafungwa katika matrekta. Lakini tukiziachia karakana zikamalizika kabisa basi tujue na matrekta hatuyawezi tena. Bei za kutengeneza matrekta katika gereji za binafsi zitakuwa kubwa na hazina mwelekeo.

Inasikitisha sana kuona kwamba baada ya miaka mitano sisi kuzungumza suala hili bado kuna sentensi moja tu iliyotajwa humu na malengo mengi lakini hakuna maamuzi yaliyofanywa kuhusiana na suala zima la uendeshaji wa karakana.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja kutoa maelezo yake atupe utandu na ukoko kwamba wizara ina mkakati gani wa hizi karakana na mustakbali mzima wa suala la kilimo katika nchi.

Mhe. Spika, nikiendelea naomba nizungumzie kidogo kuhusu suala la uvuvi. Mhe. Spika, sisi tumezungukwa na bahari lakini tunatafuta fedha. Mimi nasikitika sana kwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kupewa fedha hizi ndogo sana za kufanyia kazi zake. Hii ni bajeti ndogo sana kwa wizara hii. Hapa kiukweli kwa Zanzibar mimi sipendi sana kuzungumzia asilimia ya kupewa. Fungu lote la serikali ambalo Mhe. Spika, mimi shahidi nimelizungumzia katika bajeti kuu ya serikali na kasema kwamba bajeti hii ya serikali ni ndogo sana ukilinganisha na mahitaji halisi ya nchi.

Mhe. Spika, bajeti inaambiwa ndio kioo cha ile nchi namna mwelekeo wake. Kwa hivyo, ingefaa sasa kwa kupitia hizi wizara zetu tukabuni njia ambazo zitaongeza mapato ya nchi. Imeonekana wazi kwamba kutokana na kuanzishwa kwa *ZRB* wananchi wanakamuliwa katika hali ya juu kabisa. Kwa hivyo, uongezekaji wa mapato kwa njia ya kodi umefikia katika kiwango kikubwa kwa sababu *ZRB* wanaporipoti wanasema wamekusanya mapato kutokana na malengo yao kwa mfano asilimia 90. Hii inaonesha ukusanyaji wao wa mapato ni mzuri lakini bado pato la nchi ni dogo sana.

Sasa Mhe. Spika, kupitia wizara hii, kupitia mradi huu wa *MANCEP* na Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini tunaiomba sana iangalie kuleta mapato mengine ya nchi katika suala zima la uvuvi wa bahari ya kati na bahari kuu. Hii itakuwa ni changamoto kubwa kwa wizara na ingelifaa lipewe kipaumbele ili Zanzibar kama alivyosema mwenzangu mmoja hapa kwamba sasa tuweke dira yetu sisi ni kuitazama bahari na mazao yake.

Mhe. Spika, serikali inaelekeza nguvu zake nyingi katika suala zima la utalii. Lakini mimi binafsi naona kwamba sisi hatunufaiki sana na biashara ya utalii. Kwa sababu mambo mengi wanayotumia watalii katika hoteli hayazalishwi hapa Zanzibar. Ziko nchi ambazo kuanzia godoro analolalia mtalii, kitanda, shuka, rangi iliyotiwa katika hoteli na kuanzia *breakfast* mpaka *dinner*, vitu vyote vinazalishwa ndani ya nchi ile. Mhe. Spika, hawa ndio wanaoingiza utalii.

Sisi Mhe. Spika, tunaagiza kila kitu kinachotumika katika hoteli zetu. Hata haya maji yetu ya *Zanzibar Kool* na *Drop* hayatumiki katika mahoteli. Tutajigamba vipi kwamba sisi utalii unatuendesha. Kwa hivyo, sehemu yake Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ni kuhakikisha kwamba kama serikali imeupa kipaumbele utalii kwamba ndio sekta inayoongoza au inaitwa sekta kiongozi, basi tufanye kilimo chetu kiweze ku-*supply* kule mahoteli kwa viwango vyao, ili kile kilimo kichangie sasa katika ile biashara nzima ya utalii ndio tutakapovuna ile thima ya utalii. Lakini kwa hali ilivyo sasa hivi si rahisi sana.

Mhe. Spika, naendelea mbio mbio kwa sababu ya dakika ambazo tumepewa nizungumzie suala la kilimo na matunda. Mhe. Spika, embe ni tunda zuri sana. Kwa sababu miembe haitiliwi maji ikifika msimu wake huzaa huwa haina tatizo kubwa. Mhe. Spika, miti mingi hutaka kutiliwa maji kwanza, lakini miembe wakati ule wa kiangazi ndio hutoa maua. Lakini tumeingiliwa na hawa nzi wa embe inasikitisha kwamba *kilometre square* ngapi sijui za Zanzibar tunashindwa na dudu hili nzi tu mdogo.

Mhe. Spika, nimeangalia katika kitabu naona miji iliyotajwa ni minne humu, mmoja sikuufahamu kwa sababu imetajwa kwamba kumepelekwa mitego 16,800 katika maeneo ya Muyuni, Mtende, Mjini Unguja na Makunduchi. Hili moja sikulifahamu kwa sababu kule kwetu Pemba iko miji inaitwa hivi Mjini Kiuyu, lakini nilikuwa natazama Mjini Unguja kuna mji huku unaitwa Mjini Unguja au ni hapa mjini penye majumba ya ghorofa ndio kulikopelekwa mitego hiyo.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri aje anifafanulie pengine kuna mji huko shamba unaitwa Mjini Unguja mimi sikufahamu. Kama kule kwetu kuna Mjini Kiuyu, Mjini Wingwi, kwa hivyo na huku labda iko Mjini Unguja ambapo sio hapa tunapopazungumza Mjini Magharibi hapa.

Mhe. Spika, naomba nitoe rai kwamba huyu mdudu nzi hawezi kuondoshwa kwa njia za utaratibu kama hivi. Huyu ni adui na hili suala wataalam wanaliita *eradication* yaani ni kuondoa kabisa ina maana lazima avamiwe, ikiwa hakuvamiwa tusijidanganye tunamzalisha zaidi.

Kama tulivyoivamia malaria, tutafute njia za kumvamia mdudu huyu na hii lazima serikali ishiriki. Tumeshaiambia katika bajeti yake kuu na tunaiambia tena sasa hivi. Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira, katika suala utakalokuja kutujibu basi tunauza kwamba je, umepeleka maombi yako maalum serikalini ya kumvamia mdudu huyu, au bado unasitasita na keshokutwa nasikia unapitishwa tena. *(Makofi).*

Kwa hivyo, ili wananchi waone umewatumikia vizuri, basi hebu pigania huyu mdudu nzi wa embe kumuondoa, kwa sababu sisi Zanzibar ikiwa tutakosa embe, basi matunda yetu ni kidogo sana. Kwa sababu tunaona huko ma-*apple* yanavyouzwa bei zake, hatuna ma-*apple*. Sisi tunda letu ni embe, tukilikosa embe hatuna tunda jengine linaloning'inia juu ya mti, yote yaliyobaki ni haya haya tu.

Mhe. Spika: Malizia hotuba yako Mheshimiwa Mjumbe.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, suala langu la mwisho, naomba kabla sijaunga mkono hoja kuwa je, yatakapotokezea maafa ya kilimo. Kwa hali ilivyo sasa hivi wananchi wanauliza. Maafa ya kilimo ni mvua kubwa ambazo zinazoa yale mazao na watu wakakosa hata mpunga wao, au ukaja ukame. Je, wizara huwa inachukua hatua gani na ina utaratibu gani wa kuwasaidia wakulima katika hali kama hiyo. Mhe. Spika, naunga mkono hoja, naomba nimalizie hapa.

Mhe. Ashura Abeid Faraji: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba nikae kidogo.

Mhe. Spika: Kaa kitako.

Mhe. Ashura Abeid Faraji: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake na rehma zake kuweza kutufikisha hapa leo tukachangia mambo ya Serikali yetu ya Zanzibar.

Mhe.Spika, nakushukuru wewe kwa uvumilivu wako na busara zako na hekima zako, Mwenyezi Mungu atupe kila lenye heri atuondolee shari. Amin.

Mhe. Spika, pia nimpongeze Waziri wangu wa Kilimo, Mifugo na Mazingira. Mimi pia kidogo nalimalima. Nampongeza waziri wangu pamoja na Katibu Mkuu wake, Mkurugenzi wake, Afisa wake na wafanyakazi wote wa kilimo, kwa uhodari wao na utaalamu wao.

Mhe. Spika, kwanza kabisa niende moja kwa moja. Mimi nilikuwa niko katika Kamati ya Fedha na Uchumi, nilitembelea kule kwenye kiwanda cha Chuo cha Kizimbani. Katika chuo kile kuna vijana wanaume na wanawake wanasomea mambo ya utaalamu wa kilimo. Lakini narudia kusema kama mwenzangu alivyosema, sisi tuna wanawake na wanaolima sana ni wanawake Mhe. Spika. Mbona hatuwaoni hao wanawake wenzetu kuja kutufundisha mambo ya utaalamu wa kilimo. Mipunga tunajisilia tu ovyo. Leo tunasikia mpunga ukiupanda ndio mzuri. Hao wataalamu wako afisini, afisi na wao. Sasa tutajua wapi huo utaalamu wa kulima mpaka tukapata mazao ya kutosha na sasa ardhi yetu inakuwa kongwe, lazima ipate utaalamu na ipate na mbolea.

Kwa hivyo, tunawaomba na tunaiomba serikali ya Zanzibar, wale wanawake waliokwenda masomoni, basi waende vijijini wakawafundishe wanawake wenzao kulima muhogo, mananasi, mpunga, migomba, chooko na kunde. Lakini tunajilimia tu haya, tutafute kijio tule *Alhamdulillah Rabillaalamina*.

Mhe. Spika, mimi nilikwenda mpaka kwenye shamba la mtakata, hakuja takata. Mhe. Spika, shamba la mtakata zuri, kongwe lakini lina mbolea ya kutosha, hukuti hata kile kigomba cha mfano kilichowekwa pale. Jamani wanapokuja wageni basi watizame huu mgomba ni mkono wa tembo, huu mgomba kisukari, huu mgomba mlali kifupa, huu mgomba malali maua, huu mgomba mzuzu, huu mgomba kiguruwe na huu mgomba mtwike tuone. Sasa mtakata kama wataweka mifano kama ile tunapokwenda kutembelea tutaelezwa. Kisha tunauliza sisi tukifika huko, eeh! Wakati wa kupanda unafanya vipi mbona ndizi kubwa. Basi tunaambiwa unapanda hivi na hivi tunachukua.

Mhe. Spika, halafu wataalamu nawaombeni, kama alivyosema mwenzangu muende vijijini, sisi wanawake ni mahodari sana. Jinsi tunavyoyachukua mambo ya vilimo kupanda, basi hatumuoni hata mmoja kuja akatusaidia. Ombi langu ni kwamba naomba mwende vijijini kwa wanawake, hao wanawake ambao wamesomeshwa basi watoweni katika maofisi waje watuelekeze.

Mhe. Spika, siku hizi kuna hii idara wanaita Idara ya Kilimo, zamani ikiitwa *agriculture.* Mhe. Spika, ukenda katika mashamba yao, vituo vyao au afisi zao naona kama ni mashamba yao, basi utakuta kila mbegu au miche ipo.

Mhe. Spika, mimi natoa ombi moja kwamba kulikuwa kuna miche ya mifenesi haipo, mikomamanga haipo na mitufaa hakuna. Utakwenda Kongweni utakuta mkomamanga mdogo lakini una makomamanga tele na halafu makubwa, lakini siku hizi huyaoni. Kuna matunda mengi kama matomoko, mastafeli, hatuyaoni kwenye miche kama ile. Zamani kulikuwa kuna Kituo cha Wesha kule, ilikuwa mpaka makakau yanapandwa, lakini sasa huyaoni hata lile moja Mhe. Spika.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naomba miche hii iwepo ili tupande. Watoto wetu siku hizi wakitaka kitu mpaka wakanunuwe sokoni, anasubiri hicho cha sokoni tu kitoke huko Dar es Salaam hapa hakuna. Kwa hivyo tunaomba miche ipandwe tena, wana kazi gani na waoi wamekwenda kusomea, waliosoma wako wapi, basi warudi huko vijijini wakatupandie ile miche yetu.

Mhe. Spika, nikiendelea kuna mashamba ambayo yalikuwa yakipandwa minazi. Sasa hivi minazi huioni na kulikuwa kuna minazi ya kitamli mifupi tu lakini inazaa haipo. Mikarafuu utakwenda kuikuta tu matuta mawili au matatu, halafu kila siku tunapiga kelele kwa mikarafuu. Kwa hivyo, tunawaomba wenzetu wataalamu tafadhalini, mtuwekee zile mbegu zetu za asili, ili watoto wetu waje waione.

Mpaka mipera, jamani mipera mnaiona, mipera iliyokuwa tele, lakini sasa hamuioni tena, iko wapi. Zamani kulikuwa hakuna wataalamu hivi, sasa wanasoma mpaka wanasoma tena. Lakini ilivyokuwa siku hizi wanasoma basi hakuna kinachopandwa katika nchi yetu hii. Lakini utakwenda katika nchi nyengine utakuta kila aina ya matunda. Zamani walikuwa wakija kuchukua miche hapa wakiipeleka nchi za nje huko na kupanda miti mizuri pamoja na matunda, sasa hayapo.

Mhe. Spika, kulikuwa na miti ilikuwa ikiitwa nafikiri mama yangu Mhe. Zakiya Omar anaijua ilikuwa ikiitwa mikarambola. Unaijua wewe mikarambola, basi siku hizi haipo hiyo, sasa kwa nini. Mhe. Spika, mimi naomba wenzangu wamesema mengi sana, sipendi kuyarudia rudia. Wewe mwenyewe unapenda kusema tusirudie lile kwa lile halina maana. Mhe. Spika, kwa hivyo naunga mkono hoja hii mia mara tatu, ahsante sana.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi hii Mhe. Spika ya kuendeleza kikao hiki jioni hii. Vile vile nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira.

Mhe. Spika, naomba kumpongeza na kumshukuru Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira, Mhe. Burhan Saadat Haji kwa hotuba yake nzuri. Naomba vile vile kuwashukuru Katibu Mkuu pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kwa jitihada zao waliochukua hata kufikia leo kuweza kupata hotuba hii na kuichangia katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, suala la kilimo ni suala muhimu sana katika nchi yetu. Kama alivyotangulia Mhe. Ashura Abeid Faraji kusema kwamba yeye ana uzoefu kwa muda mrefu na kwa maelezo yake inaonesha kuwa kilimo kimeshuka kwa kiasi fulani.

Mimi nataka kusema kwamba suala la kilimo katika nchi yetu ni suala muhimu sana. Tunapozungumzia utalii, tunapozungumzia biashara na tunapozungumzia viwanda basi vyote hivi vinategemeana sana na kilimo. Ikiwa kilimo ni dhaifu basi faida ya utalii ni ndogo, faida ya biashara ni ndogo na faida ya viwanda ni ndogo sana. Lakini kilimo kitakapoimarika basi biashara, viwanda na utalii ndio utakapoimarika.

Mhe. Spika, utalii unahitajia sana kuwepo na kama inavyojulikana kisiwa hiki ni kisiwa cha viungo yaani *Spice Island.* Kwa hivyo, nchi yetu ina ardhi ndogo, lakini viungo maisha vinakuwa na bei kubwa. Kwa hivyo mnakuwa na ardhi ndogo lakini uzalishaji wake unakuwa na thamani kubwa.

Kwa hivyo, wakija watalii hapa basi waone viungo vinavyotoka Zanzibar, sio waje Zanzibar wakute pilipili manga zimetoka India, wakute pilipili hoho zimetoka nje, wakute mdalasini umetoka Komoro au China, wakute viungo mbali mbali vimetoka nje ya nchi yetu, kwa kweli hii ni aibu kubwa sana. Tujitahidi kuona Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira inashajihisha sana wananchi wake katika masuala ya kupatikana viungo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, katika nchi za wenzetu kama Faice Thailand na kwengine huko, basi mkifika pale katika *tour* ile ya kutembea mnapelekwa leo kwenye shamba la minanasi, kesho shamba la minazi na halafu shamba la mitufaa basi hiyo ni moja katika matembezi ya utalii tena yana gharimu pesa chungu nzima. Kwa hivyo, ningeomba masuala haya yasiachiliwe kwa sababu yanakwenda sambamba na utalii.

Vile vile mahitaji ya mahoteli na mikahawa yanahitaji vyakula vya mboga mboga, vitoweo kama kuku, mbuzi, samaki, maziwa na vile vitoweo vya magome gome na asali. Mhe. Spika, utakuta vitu vingi katika hivi tunaagiza kutoka nje. Kwa kweli hali hii hairidhishi hata kidogo. Hata lile tui la kupikia la nazi nalo linaagizwa kutoka nje, hii ni hatari.

Mhe. Spika, utalii pia unastahi sana masuala ya kimaumbile, kwa hivyo una utalii wa kimaumbile. Kwa hivyo, hifadhi ya misitu ya taifa kama Jozani, Ngezi, Huba ya Chwaka, hifadhi ya Masingini, Dole na kwenye rasi kama Rasi za Mkumbuu pamoja na wanyama pori kama Kimapunju na wengine, hawa wanaotoka hapa Zanzibar pia ni vivutio vya utalii. Kwa hivyo, mambo yote haya yamo katika sekta ya kilimo. Kwa hivyo, utali kwa kiwango kikubwa sana unahitajia kilimo.

Mhe. Spika, haiwezekana leo vitu kama mboga mboga, nyanya, pilipili boga, keroti na kila kitu kinaagizwa kutoka Bara na kinaletwa Zanzibar kwa kuwa sisi Zanzibar hatuwezi kuzalisha vitu hivi, wakati vitu hivi ardhi tunayo, na ujuzi tunao wa kuweza kuzalisha mboga mboga zote na tukalisha katika mahoteli yetu

yote. Lakini kwa bahati mbaya aslimia 80 ya vitu hivi vinatoka Tanzania Bara. Mhe. Spika, jambo hili linasikitisha sana na kwa kweli na linaturudisha nyuma sana.

Mhe. Spika, tukumbuke kwamba nchi hii ina watu ambao wanaweza kuzalisha 603,000, katika hawa 47,000 ndio walioajiriwa na serikali pamoja na sekta binafsi. Kwa hivyo, kuna watu 380,000 katika nchi hii ambao ni asilimia 70 ya wale wote ambao wanazalisha wamo katika sekta ya kilimo, kwa hivyo tukitaka tusitake sekta ya kilimo imechukua sehemu kubwa sana ya jamii katika nchi yetu. Kwa hivyo, kadiri tutakadhoweza kuimarisha kilimo ndio kadiri tutakavyoweza kuwapa nafasi wananchi wetu kupata kazi na kuweza kukimu maisha yao.

Mhe. Spika, kwa hakika hali kama hii tunayokwenda nayo, haitupi mafanikio hasa ya kuzungumza kwenye sekta ya utalii. Tukenda katika biashara. Mhe. Spika, kwa muda mrefu tunapiga kelele kwamba bandari yetu bado haina uwezo wa kuchukua makontena ambayo yana viyoyozi ili watu wetu waweze kuchukua bidhaa hapa na kupeleka nje, jambo kuwa ni kidogo. Mhe. Spika, tunaweza kuanza kidogo kidogo na halafu tunaendelea kubwa.

Mhe. Spika, tuliwahi kupeleka mananasi na viazi vitamu Sharja kwenye maonesho, na vyote vilitakiwa tena kwa bei kubwa kabisa. Lakini Bandari ya Zanzibar imeshindwa kutupatia nyenzo za kuweza kuweka makontena yenye viyoyozi vya kuweza kuweka bidhaa hizi na kupeleka katika nchi za Arabuni, vinatakiwa na vina bei nzuri kabisa.

Mhe. Spika, kwa hivyo usafirishaji wa matunda na bidhaa nyengine kupeleka nje inawezekana ikiwa tutapata msaada kama huo. Pia tukumbuke kwamba Zanzibar bado tunatumia *organic fruit, organic spice* na *organic products,* hatutumii mambolea mengi na madawa mengi. Kwa hviyo, vitu vyetu bado vina thamani kubwa na kwa hivyo ni lazima tuweze kufanya njia ya kuweza kupatikana vitu hivi.

Mhe. Spika, kwa mfano, kuna maua fulani yanaitwa maua karkadei, maua haya yalikuwa yanazalishwa JKU kule. Maua haya Dubai wanauza kilo moja *dirham* 20, ambapo hapa Zanzibar leo ni Shs. 16,000 kilo moja. Vitu kama hivi vinahitaji ardhi ndogo, lakini vinakuwa na thamani kubwa kabisa.

Mhe. Spika, viwanda katika nchi yetu hakuna, lakini viwanda vinategemea *row material* na *row material* yenyewe basi ni usindikaji wa samaki, usindikaji wa mboga mboga na vile vile usagaji wa viungo, utengenezaji wa mafuta mazuri na uzalishaji wa mbegu. Hizi mbegu zote sisi tunanunua katika vifuko, hapa tunaweza kuzalisha mbegu na kuweza kuuza katika nchi za nje pia.

Mhe. Spika, tukiangalia katika masuala ya mazingira. Kama tujuavyo kuna changamoto kubwa sana dunia nzima. Nchi yetu Tanzania ni kama nchi maskini duniani, nchi maskini duniani zimetoa mchango mdogo katika kuleta joto jingi duniani, lakini nchi tajiri ndio zinazosababisha duniani kuwa na joto kali sana mpaka ikapelekea barafu kuyayuka katika Bara la *Atlantic* na *Actic.* Hii imesababisha kutoka mafuriko katika fukwe za pwani na kuongeza mafuriko na kuongeza kiasi cha joto katika nchi zetu. Sasa sisi kama Zanzibar tumejitayarishaje kukabiliana na hali kama hii.

Mhe. Spika, ukiangalia katika ukurasa wa 8,29 na 36 utaona kwamba bado wananchi hawajapata njia mbadala ya umeme, ingawaje huku tunaona kuna jitihada za Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kwenye masuala ya *biogas*, masuala ya nishati mbadala ya kutumia jua na kutumia upepo. Bado miti inateketezwa kukatwa kwa sababu ya kuwa umeme Zanzibar ni ghali sana, ukilinganisha na nchi yoyote katika Afrika ya Mashariki. Vile vile kwa bahati mbaya hatujawa na njia ya umeme mbadala mpaka dakika hii miti inateketezwa. Ushauri wangu ni kwamba hii gesi tunayopikia basi ushuru wake ungeondoshwa ili bei yake iwe rahisi na wananchi waweze kumudu na waweze kutumia.

Mhe. Spika, kote tunakotembea nje huko, mabarabarani mpaka wanaopika mamantilie hao basi hawatumii mkaa wala kuni, bali wanatumia gesi mpaka magari ya teksi yanatumia gesi, hivyo vibajaji vinatumia gesi. Wenzetu hao walituambia kwamba makaa na kuni ni ghali kuliko gesi kutokana na jinsi ilivyokuwa bei ya chini. Lakini kwetu sisi gesi ni kitu ghali sana ambapo tajiri tu ndiye mwenye uwezo wa kutumia. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ningeomba hii gesi ikaondoshwa ushuru ili hapa Zanzibar bei ya gesi ikaweza kuteremka na wananchi wakaweza kununua gesi bila ya kulipa ushuru, ili iwasaidie katika matumizi yao, ili kuweza kuhifadhi miti kwa kutumia makaa na kuni.

Mhe. Spika, nije kwenye suala la kilimo. Suala la kilimo tumeambiwa kuna matrekta 45, sasa sisi hatujajua matrekta haya yana uwezo gani, tumeambiwa ni asilimia 84 na kidogo. Ile ardhi ambayo inataka kulimwa ni hekta ngapi na haya yana uwezo gani na kulima hekta ngapi hakuna maelezo ya kutosha. Ndio maana wajumbe hawaridhiki na suala hili la matrekta.

Jengine Mhe. Spika, kuna matrekta mengi sana China wanatumia kwa mikono tu, ambayo bei yake ni rahisi na watu wana uwezo wa kuyanunua. Mhe. Spika, naomba ifanywe kila bidii yapatikane haya matrekta ya kupandia mbegu, ya kuvunia, ya kusilia na ya kukatia mpaka yale majani ya wanyama, kuna mshine ndogo tu ya kukatia chakula cha wanyama. Ule mpunga ukishavunwa majani yale yanakatwa madogo madogo na yanakuwa ni chakula cha wanyama na inasaidia sana.

Mhe. Spika, ningeomba ipatikane kila hali mashine hizi ziletwe, ili wananchi wazijuwe na waweze kuzinunua au upatikane uwezo wa kukopeshwa ili waweze kulima kilimo cha kisasa. Mhe. Spika, wakati umefika sasa hivi kufanya mapinduzi ya kilimo, kutokana na kilimo cha kujikimu kuingia katika kilimo cha biashara. Huu ni wakati muafaka kabisa na tusipoteze wakati tuingie katika kilimo cha biashara tuweze kuwakimu watu wetu na kusafirisha nje, hata ikiwa kwa kiwango kidogo.

Mhe. Spika, tunatumia fedha nyingi za kigeni kwa kuagizia mchele, sukani na unga. Sasa hatujui mpaka sasa hivi Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira hawajatupa takwimu ni kiasi gani wanaweza kupunguza mahitaji ya chakula kuingia nchini na kuhifadhi fedha za kigeni kutokana na uzalishaji wa mchele na vitu vingine vinavyoweza kupatikana hapa nchini kwetu. Mhe. Spika, ipo haja kubwa ya kuweza kufanya thamani hiyo na kujua lipi ambalo litaweza kusaidia. Mhe. Spika, nikiingia katika Chuo chetu cha Kilimo mpaka dakika hii chuo hiki kinatoa cheti tu peke yake. Mhe. Spika, wakati umefika sasa hivi chuo hiki kiimarishwe na kiboreshwe ili kiweze kutoa angalau diploma, ili vijana wetu waweze kuwa na vyeti ambavyo vitakuwa vinatambulika.

Mhe. Spika, suala jengine ni kwamba chuo hiki kinapewa nafasi ya ku-*stand* kwenda Makurunge. Ningeomba Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira suala la Makurunge wasilipuuze, hii ni fursa ya pekee, miradi mingi sana inaweza kufanywa kule Makurunge na kwa kweli serikali imepoteza fedha nyingi huko Makurunge na bado inaendelea kupoteza fedha.

Kwa hivyo, shamba hili kuliwachia likapotea ni hasara kubwa na lisiachiwe ichukuliwe kila aina ya hatua liweze kufanyiwa kazi, kama tulivyoahidiwa hapa katika vikao mbali mbali katika Baraza la Wawakilishi tangu lilipoanza.

Mhe. Spika, ningeomba kutoa wito kwamba hili zao la karafuu lisiachwe, litiliwe mkazo. Mhe. Spika, wenzetu kama Mauritious walianza na zao la miwa. Waliweza kuzalisha miwa na waliweza kuuza sukari kwa mwaka na nchi yao ikapata mapato, karibu milioni 600 dolla kwa mwaka, walikuwa wakipata kutokana na sukari.

Wameondoka kwenye sukari wamekwenda katika utalii, viwanda vya nguo na mpaka sasa hivi wamefika katika suala la *technology*, wamemaliza masuala ya EPZ mpaka sasa hivi wamo katika *IT*. Lakini bado sukari uzalishaji wake uko pale pale na mikakati iko pale pale.

Kwa hivyo, unapokuwa katika masuala ya uchumi na unapokwenda hatua moja mbele na ukasahau na nyuma, maana yake hujapiga hatua, badala ya kwenda mbele unabaki pale pale hatua moja moja tu. Ukenda hatua moja, mbili, tatu na

nne, kwa hivyo zao la karafuu likiachwa ina maana tunabaki pale pale. Kwa hivyo, zao la karafuu liimarishwe uzalishaji uongezeke, hata kama bei imeshuka basi mazao haya iko siku bei inaweza ikapanda na bado kipato chake tutakihitajia na wananchi bado wanahitajia na inaweza ikawasaidia.

Kwa hivyo, kilimo cha karafuu kisiachwe kiendelezwe na hiyo ndio itakuwa tunapiga hatua ya pili. Tukitoka katika karafuu hatua ya kwanza, utalii hatua ya pili na tupige hatua katika mengine. Lakini tukikitupa kilimo cha karafuu basi tumetupa msingi mkubwa kabisa wa kilimo. Mhe. Spika, kwa haya naomba niishie hapa na kwa heshima na taathima kwa niaba ya jimbo langu la Ikulu nasema naunga mkono mia kwa mia, ahsante sana.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi ya kuichangia bajeti hii ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira. Kwanza nampongeza waziri mwenyewe binafsi pamoja na watendaji wake wote wa wizara hii, nawapongeza kwa utendaji wao mzuri kwenye kazi zao.

Mhe. Spika, nitaanzia katika ukurasa wa 11 kuhusu utekelezaji wa malengo mwaka 2009/2010. Mhe. Spika, kwenye hiki kitabu nimeona programu tano, huduma za kilimo, kuimarisha huduma za mifugo, chakula na lishe, uimarishaji wa mazao ya kilimo na kuhamasisha kutoa mafunzo ya UKIMWI.

Mhe. Spika, hizi programu tano ni nzuri kama tutazifuata kwa uelekevu na ufanisi, basi naona tutaelekea vizuri na tutashinda vizuri malengo yetu haya yaliyowekwa hapa ya 2009/2010. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ahakikishe tunayafuatilia vyema ili kufikia upeo.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 16 kuhusu huduma za elimu kwa wakulima. Mhe. Spika, hizi huduma humu kitabuni zimeandikwa kwa televisheni, vipeperushi, mafunzo ya wakulima, mabibi shamba na mabwana shamba. Mhe. Spika, namwambia Mhe. Waziri hii haitoshi. Hawa mabwana shamba na mabibi shamba wenyewe kwanza wangekuwa nazo hizo konde ili wakaonesha mfano, mwanzo hadi mwisho wa mavuno. Nafikiri kuonesha kwa vitendo ni bora zaidi kuliko hata kwa *theory* tukaangalia ufanisi wake utakuwaje. Haidhuru sio peke yake japo ni kundi la mabwana shamba na mabibi shamba wanne wanne kwa vile tunao wengi, wakafanya kikundi kimoja kimoja cha mpunga pamoja na mambo mengine. Halafu wale wanaofundishwa wakaona kwa vitendo yaani kwa macho yao jinsi wale viongozi wanafanya nao nafikiri watashiriki vizuri tu kwa hili.

Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 29 kuhusu idara ya mazao, biashara, matunda na misitu. Hapa nitaanzia na misitu. Mhe. Spika, Mhe. Waziri kama atakubaliana na mimi pamoja na wote wanaosikiliza sasa hivi, misitu haipo kabisa imevamiwa na imemalizwa na iliyobaki imebakia rakaa teni. Tulikuwa na msitu wa Hanyegwa

mchana haupo, tulikuwa na msitu japo tutasema tunao wa Jozani, umebaki rakaa mbili na huko kwengine kulikobakia Kiwengwa nako ndio hivyo hivyo, tunasema hamna misitu, misitu imevamiwa. Mhe. Spika, sio sisi ni viongozi ndio tunaotoa vibali vya kukatwa hiyo misitu. Kwa hivyo, hiyo adhabu tukiiweka haifikii mwisho. Wewe unaweka adhabu akikamatwa yule unakwenda kumtoa. Sijui kama tuna ubia au tunashirikiana au sijui niseme vipi.

Mhe. Spika, kwa makusudi mazima sisi viongozi, watu wanaokaa jirani na misitu pamoja na wananchi wote basi tukubaliane kwa hili, tuwache tabia ya kusema halafu tukarudi nyuma, sote tuwe pamoja kukilinda hicho kilichokuwepo halafu tukiendeleze. Kwa sababu hakuna tuipande tena hii miti ili tuipate hiyo misitu, halafu tuwaelimishe sote hao wenzetu wanaokata, waliokuwepo jirani na wengine.

Tukikosa misitu basi tutakosa mvua, kama hakuna mvua njaa tayari, sio njaa peke yake pamoja na maradhi, kwa sababu hakuna hewa joto mwisho tutakufa. *Pollution* itajaa hapa kwa tatizo la kukata misitu na hiyo misitu tujitahidi kuipanda mtu hata pembeni mwa nyumba yake azungushie miti kwa kuepusha haya. Nafikiri tukikubaliana kuyafanya haya sote kwa pamoja tutafikia kwenye hatua nzuri.

Vile vile nizungumzie kuhusu Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini nayo naipongeza kwa Hifadhi ya Minai. Kwa kweli ile ni hifadhi nzuri yenye matumbawe mazuri ambayo yanatoa samaki na baada ya muda hapa tutakuwa na samaki wengi kuliko na matajario yetu.

Lakini kuna matatizo kwa wavuvi wenye kutumia vyavu, sasa zile vyavu zinakuwa zinakatika vipande vipande, wakati vinapokatika na kuingia kwenye matumbawe samaki wadogo wadogo wanakufa na matumbawe yenyewe yanaharibika. Kwa hivyo, idadi ya samaki inapungua na hatutofikia lengo kama vile tulivyokusudia.

Mhe. Spika, naomba hawa wenye hifadhi kila baada ya muda nadhani wafanya ziara katika maeneo yale, kwa ajili ya kufanya maarifa ya kuzitoa zile nyavu kwa lengo la kulinda matumbawe yetu.

Nikiendelea na mchango wangu niende kwenye Idara ya Vyama vya Ushirika, kazi zake ni kusajili, kutoa elimu, huduma za ukaguzi pamoja na kuondoa migogoro. Lakini pamoja na haya Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kuna suala moja nadhani wamelisahau hivi kama ni vyama bila ya shaka vitakuwa na mikopo, ambayo watu au wanachama watakuwa wanakopeshwa, wakati anapokopeshwa mtu basi awe na moyo wa kulipa. Kwa hivyo, hapa ninaushauri nataka niongeze kuwe na usimamizi wa fedha, yaani fedha wanazokopeshwa

kama vile kununua maboti, vyavu, jarife pamoja na mambo mengine, basi kuwe na usimamizi mzuri kwa lengo la kurejesha, ili na wenzao waweze kukopa tena kwa ajili ya kufanikiwa kama wao.

Mhe. Spika, ukurasa wa 45 kuhusu Karakana ya Matrekta. Nadhani tunalo jengo tu na Mhe. Waziri atakubaliana na mimi, yaani hakuna karakana isipokuwa lile ni jengo tu ambalo lipo pale Mbweni. Kwa kweli karakana lazima iwe na zana za kufanyiakazi, vipuri au malighafi, hasara kwa serikali kwa sababu wafanyakazi wapo pale na kazi hakuna kutokana na ukosefu wa nyenzo za kufanyiakazi. Kwa hivyo, bajeti hii imekwisha, lakini bajeti ijayo kwa makusudi iwekewe kifungu chake kwa ajili ya kuifanya iwe bora zaidi kama karakana zilizopo duniani. Kwa mfano, watu wakiona karakana basi wajue kweli ile ni karakana na kilimo.

Mhe. Spika, Zao la Karafuu. Mimi ni mshamba naujua mkarafuu *A to Z*, zamani huko kwetu shamba maana lazima niseme kwetu. Mikarafuu hii ilikuwa inakua inazaa karafuu vizuri, karafuu zile zinapokuwa pevu basi tunaita matende sijui wengine wanaita nini, yaani zile mbegu zinaanguka chini na inatoka miche ya mikarafuu mizuri sana.

Lakini siku hizo wataalamu hawakuwepo na mikarafuu ilikuwa mingi, basi mikarafuu ile walikuwa wakiichukua na kuieneza kwenye sehemu nyengine ambazo ni *open space*, halafu wanachukua vijiti kwa ajili ya kuikinga na wanyama kama vile ng'ombe na mbuzi wasiiharibu mpaka inakua. Kwa kweli Mhe. Spika, mikarafuu ilikuwa mingi na hasa huko kwetu Ndijani na inazaa vya kutosha na wala hakuna na mtaalamu, yaani sisi wenyewe wananchi wa kawaida tulikuwa na moyo wa kufanyakazi, kwa ajili ya kuiendeleza mikarafuu yetu na ilikuwa inafanyika kazi vizuri.

Mhe. Spika, sisemi kama wasiwepo wataalamu, lakini na wale wenye mashamba tungewarejeshea hali yao ile ya kawaida na kuwahamasisha na kuweza kufanya kama zamani, kwa hiyo wataalamu wakawa ni sehemu ya ziada. Kwa hivyo, ni vyema ule ubunifu wetu wa asili tukaendelea nao, nadhani zoezi la mikarafuu lingefanikiwa katika hali nzuri na kuliko hata mwanzo, kwa sababu hivi sasa tunao wataalamu. Pamoja na hayo, zamani hatuna wataalamu lilikuwa zuri na hivi sasa tunao wataalamu, basi tungepata yale ya zamani na ya sasa. Mhe. Spika, hali hiyo ndiyo iliyokuwa ikifanyika hapo zamani na watu wengi wanajua, isipokuwa nakumbusha tu na sehemu za Pemba pia nafikiri walikuwa wakifanya hivyo.

Kuhusu Matunda ya Biashara. Kwa kweli Dubai ndimu ni ghali sana, yaani kile kikapu cha mkononi basi unaweza kurudi na dirhamu nyingi sana. Kwa hivyo, kama tumeacha ule usafirishaji wa bidhaa ndogo ndogo ni vyema tukarudia kama vile zao la ndimu na midimu imeenea na hata sehemu za maweni ni nyingi tu,

mpaka hivi sasa wakulima wanavunjika moyo, kwa sababu ndimu zimekuwa nyingi na wala hazina soko. Kutokana na hali hiyo, nafikiri ni vyema kukafungua lile soko kwa ajili ya kusafirisha nchi za Kiarabu hizi ndimu, pilipili hoho Bombay kama chumvi, yaani mtu anaponunua chakula basi lazima ananunue robo au nusu. Kwa hiyo, kama tunazisafirisha na kuzipeleka Bombay basi ni bidhaa nzuri sana.

Mhe. Spika, kama Mhe. Waziri hana soko, basi nitamsaidia kutafuta kwa hizi pilipili hoho, yaani tutapanga mpango mzuri wa kupeleka kule na kuweza kutoka, kwa sababu pilipili hizi bei yake ni nzuri Bombay kuliko chumvi tunavyonunua sisi hapa, mtu akinunua chakula lazima atie na pilipili. Mhe. Spika, kwa hayo machache na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa kwa ajili ya kuchangia Hotuba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira.

Pili nikushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kwa wakati huu.

Tatu vile vile nimshukuru pamoja na kumpongeza Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira pamoja na watendaji wake.

Nne niwashukuru wakulima kwa juhudi zao kubwa sana wakulima wa Zanzibar pamoja na ustahamilivu wao katika kilimo.

Kwanza napenda kila mtu afahamu kwamba mchango wa serikali kwa wakulima wa Zanzibar sio mkubwa sana. Lakini juhudi za wakulima wa Zanzibar ni kubwa mno.

Mhe. Spika, katika nchi zinazoendelea hivi sasa wakulima duniani hawalimi kwa vile vijembe vya kawaida, wanalimia majembe ya kileo. Lakini Zanzibar bado tuko kwenye kilimo cha zamani.

Kwa kweli wakulima wetu inapaswa kila mwaka tuwapongeze na kama wako wakulima bora basi wapewe zawadi. Mhe. Spika, kutokana na upelelezi wangu Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira imekuwa kama ni mratibu tu, ikija hapa inajisifu tumezalisha tani kadhaa, lakini ukipeleleza sana ni juhudi za wakulima wenyewe. Kwa hivyo, serikali inapaswa ilione suala hili kwamba bado mchango wa serikali kwa wakulima ni mdogo sana na wala haiwezekani hata kusifu katika Baraza hili.

Mhe. Spika, wizara inaonekana kama inaratibu, sawa na ile Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ, huwauliza hivi nyinyi mnafanyakazi gani na mkifika hapa mnajisifu kwamba mmefanya hili na lile. Lakini hamjengi, hamlimi na wala hamfanyi chochote isipokuwa mnaipamba bajeti inakuwa nzuri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilivyopeleleza sana nimeambiwa kwamba hawa ni waratibu tu ah! Sasa kama unaratibu unachukua nafasi, yaani unakwenda kwa siri na kuchukua *activities* ambazo wamefanya watu wengine na hata habari hawana wakati unapochukua. Nadhani ni vyema kwanza kuwashirikisha na baadaye kujisifu.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kwa kuiangalia kwa mbali mkulima bado hafaidiki. Kwa kweli ninashangaa wizara hii wataalam wengi na inakwenda sifa, lakini humo mabondeni mpaka waambiwe anakwenda Mhe. Waziri Kiongozi ndio wanateremka. *(Makofi)* .

Hata hivyo, nashindwa kuelewa kwamba wamesoma sana, lakini uongo hawaijui hata ile mienendo ya miongo na wakulima wanapata tabu sana. Kwa mfano, mienendo ya miongo hawasaidiwi kuelekezwa kwamba mwaka huu muongo umekwenda mbele kidogo kwa siku tano au sita, basi mnatakiwa mtayarishe mashamba tarehe fulani na muanze kupanda tarehe fulani hakuna, isipokuwa kila mkulima anabahatisha kutokana na ile miongo yake ya kurithi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ningeomba wanapowasomesha hawa basi jambo la mwanzo wasomeshwe miongo kama si hivyo tunawapoteza wakulima. Kwa kweli wakulima wanalima wakati umeshapita wakipanga wanavuna mapepe, kwani hatuwasaidii wakulima na tusipambe vitabu wakati kuna haja ya kuwasaidia wakulima.

Hata hivyo, mkulima unamsaidia kumtoa katika kilimo cha zamani na kumleta cha sasa, lakini bado tunawasifu na wako vile vile. Kwa mfano, yanapokuja matrekta unaambiwa wilaya nzima trekta moja. Katika kusubiri nafasi yako ya kulimiwa basi msimu utapita bado hujalipata na hii ni hasara kubwa sana, tuwatizame wakulima.

Mhe. Spika, kwa mfano mzuri wa wakulima wanavyokufa sana pale Kibeni Mkwajuni kwa Mhe. Juma Duni Haji tuangalie wanavyoumia. Kwa kweli wakulima wanapata tabu sana, haya masuala ya pembejeo, mbolea, futi ngapi za kupata yote wakulima hawayajui. Lakini tukifika hapa tunaoneshwa ng'ombe walivyoshiba, sijui magugu ya mpunga na mambo gani na hivi si tunadanganya. *(Makofi)*

Mimi mpaka leo naishi vijijini na ninawaona wakulima wanavyoteseka, yaani namna wanavyokula hasara. Kwa mfano, mkulima katika siku 366 karibu siku 90 anapanda gari shilingi 1200/- kutoka Mkwajuni kwenda Kibokwa na kurudi tena bila ya msaada wowote, anapofika huko analima kwa kijembe atanenepa, hanenepi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tuwageuze wakulima twende na wakati, lazima tuone Mhe. Waziri anawabadilisha wakulima kutoka kilimo cha zamani kwenda cha kileo na atakuwa mfano mzuri. Kwa kweli ardhi yetu inayo rutuba sana na inastahamili, kwa sababu muda wote tokea mimi sijazaliwa inalimwa na inatoa, lakini haina nguvu wala msaada. Kwa maana hiyo, tuwatafutie mbolea pamoja na pembejeo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kutoa ushauri katika kilimo tujaribu kupunguza mambo, ili tuone tunapata matrekta ya kutosho pamoja na wataalamu ambao wanaweza kuwasaidia wakulima na wala tusipambe mabuka, wakati tunaona wakulima wetu wanaumia.

Baada ya kuondoka kwenye kilimo sasa niende kwenye ukurasa wa 33. Mhe. Spika, juzi nilipokuwa nikichangia Hotuba ya Mpango wa Maendeleo ya Serikali, nilisema kwamba wako watu wenye juhudi tena wakarimu, rafiki yangu Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha alikaribia kukasirika.

Kwa kweli lazima tuone wako watu wenye sifa ya kusifiwa. Kwa mfano, tuingie Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini, nani ambaye hajui kuwa idara hii inafanya vizuri sana kwa nchi yetu. Lakini bado tunamuachia Mkurugenzi wa Idara hii agombane na wavuvi tu na wala sisi hatumsaidii, kwa sababu hivi sasa mataifa yote yanasema kuna uhifadhi wa mazingira na suala hili ni kubwa sana katika dunia.

Kwa hivyo, bado Mkurugenzi anao moyo wa kusimamia mazingira, lakini anayo sifa kubwa sana ya kuwasikiliza wale watu ambao wanaoharibu mazingira, pia juhudi yake ya kutafuta misaada katika Sekta ya Uvuvi yapo na yanaonekana. Kwa mfano, hivi karibuni Mkoa wa Kaskazini katika kupunguza tatizo la uharibufu wa mazingira wananchi wengi wamepokea boti na vyavu, hii ni moja miongoni mwa juhudi ambazo zinaonekana wazi wazi. Pamoja na kwamba hazitoshi, lakini huwezi kufanya jambo kwa mara moja, lazima upate muda ukasaidia pamoja na kuwapa matumaini watu.

Mhe. Spika, katika hayo hivi karibuni tumetengeneza ile Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu, kwa sababu shida yetu Zanzibar zaidi ni kitoweo na chakula kama hatutotengeneza mazingira mazuri, basi siku zote tutapambana na mfumko wa

bei. Kwa kweli mfumo wa bei Zanzibar hautabiriki, Watanganyika wakilima sana mfumko unapungua, wakishindwa kulima sana basi mfumko unapanda. Kwa mfano, hivi sasa mchele wa Mbeya uko chini ya shilingi 1,000/- kwa kilo moja ule wa chenga chenga na ule mzuri ni shilingi 1,000/-, yaani kutoka shilingi 1,400/- mpaka 1,000/-, lakini mtegemea cha ndugu hufa masikini.

Kwa hivyo, tujitahidini kuona kwamba tunalima pamoja na kufanya mipango mizuri ya uvuvi, ili tuone tunapiga hatua nzuri katika kuzuia mfumko wa bei. Mhe. Spika, mfumko wa bei unapopanda unachafua kila kitu, lakini mfumko wa bei unapokuwa wastani, basi hali ya maisha inakuwa nzuri. Vile vile tunayo maeneo mazuri ya kupunguza sana mfumko wa bei.

Kwa mfano, kama tutalima na kuvishughulikia Viwanda vya Sukari pamoja na mambo mengine, basi tunaweza kupungukiwa na tatizo kubwa. Lakini tunapopanga mipango kama vile tumekikodisha kiwanda karibu hivi sasa miaka siijui tunasubiri uzalishaji, kwa ajili ya kupunguza bei za sukari kutoka nje.

Mhe. Spika, nadhani mwekezaji hakiwezi, hatupewi jawabu wala maelezo na bado amezuia tu. Kutokana na hali hiyo, hatuwezi kupungukiwa na matatizo, kwa sababu tumejipanga kabisa kuweka miundombinu ya mambo yale, lakini waendelezaji hakuna.

Kwa kweli ninashangaa sana kwa mujibu wa utaratibu kama umempa mwekezaji kiwanda au mradi wowote kwa ajili ya kuwekeza basi akizidi miaka miwili unatakiwa utoe taarifa amefika hatua gani. Kwa hivyo, kama ameshindwa basi ni vyema akarejesha ule mradi, kwa lengo la kutafutwa mtu mwengine na kuwekeza. Kutokana na hali hiyo, bado nahoji kwamba Kiwanda cha Sukari hakijaonesha maendeleo yake katika nchi yetu. Kwa hiyo, naomba sana ifanyiwe marekebisho ama kirejeshwe kwetu au tumtafute mwekezaji ambaye ni madhubuti.

Mhe. Spika, nilikuwa kwenye ile Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini, isipokuwa nilikuwa nikitia vinyama. Idara hii hivi sasa kwa mujibu ilivyo inatakiwa ifanyiwe mageuzi tena, sio mageuzi ya sheria au vipi, isipokuwa lazima tuipe nguvu. Vile vile inaonekana Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira inao mzigo mkubwa kama vile mazingira, kilimo, mifugo na kadhalika. Sasa kwa hatua ambayo imefika Idara hii ya Mazingira ipo haja ionekane kwamba igeuzwe angalau Wizara katika Nchi (AR), kwa ajili ya kupata mafanikio makubwa zaidi au vyenginevyo. Kwa kweli tunapogeuza vile jambo moja moja na yakifika mambo manne au matano, basi tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana.

Mhe. Spika, inavyoonekana katika Idara za Serikali ambazo ziko mbele katika kukimbia ni Idara ya Uvuvi pamoja na Shirika la Bandari, lakini nitakuja kulisifu siku hiyo. Pamoja na hayo, nikisifu wengine wananuna, kwa sababu juzi nilisema hawa watoto wa Mzee wetu Rais Mstaafu wa Zanzibar Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi mahodari, basi watu wengine wananuna, mtu unamsifu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha juzi alikasirika bure na kusema niende wizarani kwa ajili ya kula *chips* kwa rosti. Lakini nilikuwa nikisifu hali halisi ilivyo, kwa sababu wakati mwengine tunakwenda wizarani au idarani angalau kupima kuona unapokelewa vipi, ukifika kule karibu. Kwa kweli watoto hawa sifa wanazo sisi na sijui huko.

Kwa mfano, tunapokwenda kwenye idara zao tunaonaje, kama vile Bandari au Uvuvi *Alhamdulillah*, lakini wengine unaambiwa huyu bwana hayupo amesafiri na mlango haufunguki kumbe yumo ndani na hili ni tatizo. Mhe. Spika, zile idara zinatutuma na kufanyakazi mule na wala hatuna sehemu nyengine za kufanyiakazi, basi lazima tukubali na atakayekata kusifiwa basi tutamsifu tu.

Vile vile tukimuona anaboronga tutamwambia tu, kwa sababu hivi sasa ule muda wa kununiana upo, kwa sababu hivi sasa tumo kwenye mikondo hii mipya ya siasa na kila mtu anayo kambi. Mhe. Spika, nilimbaini rafiki yangu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk wakati alipokuwa akichangia, basi alimsifu rafiki yangu na sijui leo kama hakugawa miswala. *(Makofi)*

Kwa kweli tunatakiwa tusifu, lakini mimi sisifu kwa hilo na siku zote hawa watu wapo na kukiwa na tatizo tunakwenda na hali tunaiona. Lakini ziko idara nyengine hata kama uwe na shida ya kiwembe basi si rahisi, yaani hupati.

Kwa mfano, Shirika la Meli sijui kama bovu au vipi, sasa hali hii itakuwa vipi, kwa sababu shirika ni kubwa ambalo ni la muda mrefu, tena lina karibu idara mbili kama utazipeleleza zimo, maana yake humo ndani kuna uwakala pamoja na meli yenyewe.

Lakini hata pale mlangoni unaogopa kwenda kuuliza mtu kwamba jamaa mtu wangu anasafiri mfanyie punguzo la tiketi, unaambiwa loo! Hasara kubwa haiwezekani, kwa sababu tiketi unafanya punguzo tu kutoka shilingi 20,000/- na kuwa shilingi 10,000/-, basi analalamika, hivi kweli ndio tunakwenda lazima tusaidiane. Kwa kweli nasifu na bado naseme kwamba Idara ya Uvuvi itengenezewe mazingira, ili ionekane inapiga hatua. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende kwenye Idara ya Maendeleo ya Mifugo. Kwa kweli hii ni idara muhimu sana, kwa sababu vitoweo vyetu vitatu katika nchi, samaki habarini, wanyama na mboga mboga. Kwa hivyo, lazima tuone kwamba hizi ni sehemu zetu tatu ambazo zinatosheleza kwa kitoweo.

Pamoja na juhudi zote idara hii bado iko nyuma kidogo, iko nyuma kwa nini, kwa sababu wafugaji hawa wanaofuga wanyama wa kienyeji, kama vile mbuzi, ng'ombe na kuku hawapigi hatua, maana ile hatua si kama iwe ndani ya kitabu. Kwa mfano, kwenye mazingira yenyewe tu ukitembelea utaona hakuna ongezeko la mifugo hii ya kawaida kama vile ng'ombe, mbuzi na kuku.

Mhe. Spika, mnamo miaka ya 2005 kama sikosei au nyuma kidogo wafugaji walikumbwa na tatizo kubwa sana la wanyama kuna maradhi yanayoitwa chambavu, yaliwaumiza wafugaji sana na tulifikiria kwamba nchi yetu itafanya kama nchi za kigeni. Kwa kweli nchi za wenzetu kama kunatokea janga kubwa, basi wafugaji au wakulima wanafidiwa, lakini hapa kwetu haipo hiyo.

Mhe. Spika, nilitegemea yale matibabu, dawa na mambo mengine yatakuwa bure. Lakini inaonekana bado tatizo la kusaidia wafugaji lipo, yaani wafugaji wajitegemee wenyewe. Pamoja na hayo, tunashukuru kwa upande mwengine hawa wafugaji wa kuku wa kileo wamepiga hatua sana, nafikiri si muda mrefu mayai yatatosheleza katika soko letu, kitakacholeta upungufu labda miezi miwili ya Fungo Mosi na Tatu. Kwa kweli siku nyengine zote zinazobaki wafugaji wanatosheleza soko la ndani hasa kuku hawa wa kienyeji.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri, idara hii ijitahidi sana kuona kwamba katika maradhi ya wanyama hasa kuku wajitahjidi mahepe na ndui. Hivi sasa ndui inawavunja moyo sana wafugaji. Kutokana na hali hiyo, ipo haja ya makusudi kuona kwamba wanapiga vita ndui pamoja na mahepe kwa njia zozote, ili yaondoke kabisa, kama si hivyo Mhe. Spika wafugaji hawatopiga hatua.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kulizungumza ni Idara ya Mazingira.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, muda umemalizika nakupa dakika mbili.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu naunga mkono wizara hii pamoja na maelezo yote kwa asilimia mia moja. *(Makofi)* Ahsante sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia kwa kifupi tu Wizara hii ya Kilimo, Mifugo na Mazingira.

Mhe. Spika, kabla sijachangia chochote naomba nitoe pongezi kwa wote waliochangia wamechangia kwa utaalamu na kwa sababu Kanuni hairuhusu kurejea yale kwa yale. Kwa hivyo, mchango wangu leo utakuwa zaidi kwa masuala ya kuelimishwa kwa lengo la kuona hiyo safari tunayokwenda ndio au sio, natarajia haitokuwa kama mwaka jana na safari hii nitapata majibu.

Tunafahamu nchi yetu ni masikini na wananchi ajira yao kubwa ni kilimo na uvuvi, kwa sababu ardhi yetu ni ndogo na bahari *Alhamdulillah* tunayo kubwa sana. Kwa hivyo, kama tunataka kuondokana na umasikini kwa mazingira ya nchi yetu ilivyo, basi hatuna budi tuzalishe mazao ya kilimo kwa wingi pamoja na kuitumia vyema bahari yetu.

Mhe. Spika, katika kukitizama hiki kitabu kimeeleza kuwa shughuli za kilimo na uvuvi zimeongezeka sana, vile vile tusisahau kuwa idadi ya watu inaongezeka katika visiwa vyetu bila ya mpangilio.

Hata hivyo, ninalo swali hapa tunasema kilimo kimeongezeka, maana yake ni kuwa tunacho chakula cha kutosha na pengine cha ziada kuuza katika nchi za nje, kwa ajili ya kuingiza fedha katika serikali na kuwa na chakula cha kutosha kwa kupunguza kuagiza chakula kutoka nje.

Mhe. Spika, ikiwa kilimo kimekua swali la mwanzo.

(a) Je, wizara imeingia kiasi gani kwa bidhaa za kilimo kutokana na kuziuza kupeleka nchi za nje?

(b) Kwa nini mambo mengi ambayo yanaota hapa huwa tunaagizia kutoka kwa wenzetu pamoja na sisi kilimo chetu kinakua?

Kwa mfano, Wazanzibari chakula chetu kikubwa ni mchele, lakini tunaagiza mchele kwa wingi wanatokea nje ya Tanzania mpaka upande wa pili wa muungano, wakati humu tunaambia kilimo cha mpunga kimeongezeka mara dufu.

Vile vile katika uvuvi nimeona kwamba malengo ya wizara kwa mwaka wa fedha 2010/2011 ni kuongezeka kwa matumizi ya zana za kisasa za uvuvi. Maana yake zana za kisasa tunazo na hivi sasa tunao mpango wa kuziongeza.

Mhe. Spika, kwa bahati mbaya ikiwa zana za kisasa tulizonazo ni hizi mashua, nyavu, mashine zilizotolewa katika vikundi mbali mbali. Swali langu lipo hapa kwa vile mimi nafikiri kuwa uvuvi wa kisasa ni kutumia zana za kisasa. Kwa mfano, kama ile meli iliyokamatwa inaiba samaki kwa wingi sana. Sasa ikiwa huu wetu ni wa kisasa ule ni wa aina gani?

Pamoja na hayo, nimeongeza hapa mimi ninaomba wizara ifanye kama inavyowezekana itumie hii bahari ipasavyo. Kwa kweli wavuvi wetu wanavua ovyo, yaani kuna uchafuzi mkubwa wa mazingira, mazalio ya samaki yanaharibiwa.

Kutokana na uvuvi wetu hata ile hali halisi ya maumbile ya samaki mazingira yao walivyoumbwa na Mwenyezi Mungu inachafuka, hivyo tunakuwa na upungufu mkubwa wa samaki hasa kwenye hii bahari yenye maji kidogo.

Kwa maana hiyo, kitabu kinaeleza kuwa kuna haja ya kupiga vita uharibifu wa mazingira katika zile sehemu maalum zilizotengwa, kwa ajili ya watalii kuja kuangalia na kuingiza fedha kwenye serikali. Sasa zile sehemu ambazo hazimo katika mpango huo ndio kubwa. Je, kuna utaratibu gani au inatolewa ruhusa ili hizi shughuli ziendelee. Halafu kwa wenzetu wanapovua samaki wanachangua wale ambao wameshapewa, sisi uvuvi wetu pamoja na hizo zana za kisasa tunazozizungumza ni kuwa kinakamatwa kitakachopita tu je uvuvi huu tunaouita wa kisasa ni kweli baada ya miaka mingi hizi mashua na nyavu hizi zinazotolewa zikiongezeka si vilevile tunarudi nyuma.

Halafu jengine ni uharibifu wa mazingira, Mhe. Spika, wananchi wetu ni masikini na wanajiendeshea maisha yao kwa kujitegemea kuna wengine wanaharibu mazingira ya bahari kwa uvuvi ambao ni haramu kama tunavyosema, kuna wengine wanaharibu mazingira katika ardhi kwa ukataji wa miti ovyo, ukataji wa miti ambao unaleta umasikini uliokuwa unaelezwa kwa sababu katika misitu kunakuwa na miti mingi ya matunda mwitu ambayo tunatumia, kuna mibungo, mizambarau na miti mingine chungu nzima inakatwa ovyo wala hakuna mkakati wa kuendelea kupanda miti mingine baada ya ile kukatwa.

Lakini kitabu kilivyoeleza ni kuwa Wizara hii kazi ni ya kila mmoja wetu kushiriki na kitabu kimeeleza kuwa wizara itashirikinana na masheha, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa na wananchi kukemea jambo hilo la uharibifu wa mazingira. Sasa kwa mimi ninavyoona kukemea ni kitu kukipigia makelele tu lakini hakuna hatua ya kuchukua.

Kwa hivyo kwa ushauri wangu ili tuweze kuyamudu mazingira yetu mimi nadhani kungaliwekwa sheria maalum inayomfanya mtu hata kama akikata mti lakini kuna mpango maalum wa kurudisha miti mingine japo kuwa ni michanga,

ili kuona mazingira yetu yanaendelea kama kawaida, vyenginevyo itafika pahala hapa tunapojidai kwa kulima kuwa tuna ardhi yenye rutba katika hali ya hewa nzuri nayo ikakauka tukazidi kuingia katika hali ngumu ya maisha.

Kwa hivyo nasisitiza kutafutwe mpango wa kuwekwa sheria ambayo itamfanya masikini ya Mungu aendeshe maisha yake lakini pia mazingira yasiharibiwe kwa maana ya kuwa kukemea kuwa ndio adabu ya mwenye kuharibu mazingira, wakati tunajua hivi sasa hali ya kiutaalam imeongezeka minazi inakatwa ovyo, miti inakatwa ovyo kwa kutumia njia rahisi ya msumeno wa moto kama wanavyoita watu.

Mhe. Spika, ningerudi kidogo kutaka kujua ufafanuzi wa mambo kama nilivyoeleza, tunaingia katika kuzalisha mbegu bora na Mwenyezi Mungu alipoumba nchi hii aliumba na mambo yake ya baharini na nchi kavu, kama matunda, wanyama na viumbe vya baharini, sisi tunaingia katika maendeleo ya kukuza kipato.

Tunajikita sana katika suala zima hili la kuleta wanyama kama ng'ombe na mbuzi ambao katika utoaji wa maziwa na wengine kwa nyama, kwa upande wa kuku ni hivyo hivyo kuna mbegu ya asili kutoka nchi fulani tunaleta, lakini pia tufanye kwa utaalam wetu, tunafanya kitu kinaitwa *selective birdling* yaani mbegu za kuchagua kwa sifa unazozitaka.

Lakini Mhe. Spika, hivi viumbe vimeshaunmbwa na Mwenyezi Mungu katika hali yake na ardhi hii haikuanza leo wale ambao tunao wa asili ikiwa ni miti ikiwa ni wanyama ndio Mwenyezi Mungu aliowajaalia kwamba hawa ndio wenye sifa ya kuweza kuishi hapa na kuzaa kwa wingi n.k. Hicho kizazi walichonacho sisi tunabadilisha maumbile kwa kutaka kupata faida bora, lakini ng'ombe anayeishi hapa na ng'ombe anayeishi nchi nyengine ana mazingira mengine ya kuishi.

Kwa hivyo suala langu la mwanzo sisi tunapofanya hii *selective birdling* tunao hapa mtambo wa *liquidnitrogen* na humu kuna maelezo ya utengenezaji wa mbegu bora, lakini twende kwenye hawa wanyama kwanza hii *selective bridling* hizi mbegu mpya tunazoingiza katika nchi yetu kweli mbegu hizi kutokana na hali ya maumbile ya nchi hii Mwenyezi Mungu alivyoiumba wanaweza wakazaliwa, wakazaa wazaa na hiki kizazi kikaendelea na kuweza kupata zile sifa.

Nauliza suala hili kwa sababu hili suala halikuanza mwanzo lilianza zamani sana tokea kopa ng'ombe ulipe ng'ombe, lakini sioni mabadiliko makubwa kutokana na hii kazi tunayoifanya, sasa kama hapana utaalam wa kutosha ningeliomba kwa sababu ndio tumeua mbegu ya zamani kwa kuingiza mambo ya maumbile

yanayotoka katika mbegu mpya, isijekuwa huko usoni na hichi tulichokuwa nacho cha asili alichotujaalia Mwenyezi Mungu nacho kikapotea, ni lazima kuwa na *research* halafu ndio tufanye hiyo kazi, tusiwe tumeshapata mbegu zetu tunapiga tu kila kitu kina mazingira yake.

Halafu la pili hapo hapo Mhe. Spika, ninaloomba kueleza ni kuwa unapofanya *selective bridling* tuseme ng'ombe huyu maziwa yake ni kidogo lakini hivi ninavyopandisha ni kuwa huyu dume asili yake ni maziwa mengi, au vyenginevyo lakini hizi sehemu za binaadamu ambazo zinachukua ule urathi siku zote zinakuwa mbili mbili katika kizazi chochote.

Sasa inatokezea wakati mwengine mimi nafanya shughuli hii nipate ng'ombe mkubwa mwenye nyama lakini ile nyama yenyewe inaweza kuwa na matatizo yule ng'ombe akabakia vile vile, sasa hatujui vizazi vinavyoendelea pengine inawezekana mambo yakawa mchanganyiko, ikawa vile vunavyofikiria kuwa *first* ile *generation* ya pili na ya tatu ikawa kumbe sisi tunakwenda kunyume chake.

Kwa hivyo suala langu ni kuwa kweli Wizara ya Kilimo ina watalaam wakubwa sana na vifaa vya kisasa vya kufanyia utafiti, wanayaangalia haya vilivyo kwa sababu mkulima anayepewa hawa ng'ombe au mbuzi kuchunga kwa makusudi ya kupata hayo maziwa mengi haelewi chochote isipokuwa kile unachomueleza wewe.

Karibuni hivi zilipoingia hizi *SACOs* kuliletwa ng'ombe wengi sana hapa kutoka Tanga na mbuzi wengi sana kutoka Tanga kwa madhumuni ya kuwa tuwe na ng'ombe bora watakaotoa maziwa kwa wingi na watakaozaa wenziwao wenye sifa hizo ili tuondokane na tatizo hilo la ukosefu wa maziwa. Lakini kwa bahati mbaya kwa yale maeneo niliyopitia mimi wengi walikufa na wengine walizaa hawakuwa na sifa hiyo iliyokusudiwa. Je, nasema utafiti wa kweli unafanywa?

Halafu la mwisho pamoja na kuwa mambo yote tunayoyafanya tunapata misaada kutoka nchi za nje lakini tuone kuwa ile fedha inayotumika inaleta tija, tusije tukaonekana kwamba utaalam wetu ni mdogo siku zote au mpaka wenzetu wakaja tukorofisha.

Mhe. Spika, nimesoma ukurasa wa nne napongeza kuwa tumefanya uvumbuzi wa mbegu bora hizi za kisasa ambazo tatu ni za mpunga na nne za muhogo, nikitaka kujua mbegu hizi za kisasa kwa sababu mtu anavyofanya kitu kipya huwa anakipa jina lake, na kwenye kuvumbuliwa kitu kipya kuna sehemu maalum tunakwenda kinafanyiwa uchunguzi halafu kinapewa jina kamili, hizi mbegu hasa ni mpya kwa kuwa tunazitumia sisi tu au ziko zinafanya kazi tunasema ni mpya kwa hivyo nataka nielewe.

Halafu jengine hizi mbegu mpya hasa hizi za mpunga na muhogo ni utaalam gani tulionao hapa Zanzibar wa kuweza kuzalisha kitu kipya kabisa bila ya kuwa na kikongwe tukafanya kama hivyo nilivyoeleza.

Mhe. Spika. Mheshimiwa dakika mbili.

Halafu Mhe. Spika, nikushukuru kwa kupata muda wako lakini kidogo tu kwa huku ukurasa wa kumi na tisa kuna hii taarifa ya hawa mbwa, hii tu. Hapa nimeona kuwa bajeti ya mwaka huu wa Fedha itatumia mambo mengi kwa mambo kazaa hapa lakini yanahusika na mbwa, kwanza ni kudhibiti maradhi ya kichaa cha mbwa kwa kuimarisha afya za mbwa elfu kumi na paka elfu tano kwa kuwapatia huduma na matibabu ya kinga dhidi ya maradhi mbali mbali.

Lakini chini yake kumeandikwa kuwa kufunga uzazi kwa elfu moja, sasa haya matibabu ya mbwa chungu nzima yaliyofanywa na hawa mbwa waliofungwa uzazi tuseme ni mbwa tofauti, kuna wengine walionekana kwa umuhimu wafungwe uzazi tu kwa sababu ataathari huko anakokwenda.

Sasa kuna wengine walifanyiwa matibau ili waendelee kuishi nataka kujua hapo, halafu zamani tuliona kuwa kuna majibwa mengi yanazagaa ovyo na yalikuwa hayana wenyewe, yakipigwa risasi na kuuliwa kama kitabu kilivyoelezwa katika kunguru wameangamizwa wengi mpaka ndege wengine wameingia, sasa kwa nini hawa mbwa wakabembelezwa kwa kupewa dawa kama hizo na wengine kufanyiwa mambo wasizae.

Sasa nauliza wana umuhimu gani kiasi hicho na pia kwa kuendelea ni kuwa kuna watu mia tatu na sitini wafugaji na wasiokuwa wafugaji wanapewa sehemu gani, nikitaka kujua hawa mbwa tulionao pamoja na kuwatetea haki zao.

La mwisho sasa kwa ruhusa yako ni kuwa wafugaji wenye magari ya ng'ombe wanataka kukatishwa leseni ni kwa sababu ya Wizara kukusanya mapato au kuna sababu nyengine za kitaalam katika suala hili.

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi jioni hii kupata nafasi ya kuchangia mawili matatu. Sina mapya ni yale yale yaliyokuwemo ndani ya kitabu na yale yale yanayotuzunguruka katika maisha ya kila siku.

Mimi nitaanza kama walivyoanza wenzangu kwa sababu Zanzibar ni visiwa vilivyozungukwa na bahari tulivu na yenye mali nyingi, watu wengi wa Zanzibar ni wavuvi lakini uvuvi uliopo ni ule ule waliosema wenzangu wakienyeji mno, hatujawa na uvuvi ule wa kibiashara. Kwa kweli bado Mhe. Spika, wizara

inafanya juhudi lakini haijafanya juhudi kubwa za kuona kwamba wavuvi wetu wanakwenda mbali na wanapata mazao ya samaki na mazao mengine ya bahari kama inavyostahiki, badala yake sisi tumekuwa wachumi mndu, tunazungurukwa na bahari lakini watu wengine ndio wanakuja kutumia bahari yetu kwa kupata utajiri sisi tumebakia na kulia umasikini na vianzio hivyo hivyo vya kukusanya mapato tunamkamua ng'ombe mpaka anatoka damu.

Lakini mgodi huu aliotupa mwenyezi Mungu bado hatujautumia inavyopasa ni wajibu wa wizara hii ikishirikiana na serikali kuu kuona namna gani watatumia uvuvi kuimarisha uchumi wa Zanzibar na Wazanzibari wenyewe. Na vile vile kwa sababu ya uchafuzi wa mazingira baharini Mhe. Spika, samaki wengi wameanza kupotea wale maarufu ambao tunawapenda kwa hivyo sijui kama kuna utaalam wowote unaotumika kurejesha hali ile na kuwarejesha samaki wetu waliopotea.

Nyuma huku nimeona katika kitabu hiki kuna mikandaa wengine hawajui kwa nini wizara ikaweka mikandaa, nchi yetu ni visiwa bahari siku hizi inapanda sana kutokana na uchafuzi wa hali ya hewa huko duniani. Sasa mikandaa ikiwa haipo katika pembezoni ya pwani yetu maji yatakuja kwa wingi zaidi, mimi ninachokiomba Mhe. Spika, idara ya Mazingira iwaelimishe sana watu wanaoishi pwani pwani kupanda miti au mikoko na mikandaa.

Kwa sababu huku juu utasikia ukikata mti panda mti lakini huku pwani je ambako wakati mwengine watu wanaingia kiwizi wizi kuikata hii mikandaa hapo tena bahari haina kizuizi inakwenda tu, sasa na huko baharini watu waambiwe kukata mkandaa au mkoko kwa jina jengine basi aupande na kuwe na ushindani na kiwe kilima kama ulivyo mwani, basi na hiki sasa tukifanye ni kilimo kwa sababu ni biashara miti yake ni muhimu inatumiwa sana kwa kujengea na madhubuti. Basi watu waanze kuelimishwa wawe na mashamba ya mikandaa tusiwe na mashamba ya mivinje tu na miti mingine.

Mhe. Spika, hivi sasa kwa jinsi bahari inavyokula ardhi ni muhimu sana hasa zile sehemu ambazo hazina kandaa, basi ni muhimu hivi sasa Idara ya Mazingira ikachukua jukumu kuwaelimisha watu kwamba wapande kandaa, kwa mfano ukienda nafikiri Nungwi sina hakika vizuri ardhi utaiona hasa inavyoliwa zile sehemu hazina kandaa lakini ardhi inaliwa na maji sana kwa sababu hakuna hii mikoko, kwa hivyo idara inayoshughulika na mambo ya mazingira ifanye juhudi kuwaelimisha watu wanaoishi pwani pwani waipande makusudi hii mikoko kwa ajili ya kuzuia uharibifu wa ardhi. Au kuliwa na maji ardhi yetu.

Vile vile kitabu kinatuonyesha Ng'ombe au matrekta ya kulimia kwa mkono na materekta makubwa, mwaka jana kitabu hiki kilikuja kikatuonyesha ukulima wa mabilinganyi na mabo mengine, tukasema yale mabiringanyi yana umuhimu

mkubwa kuliko mkarafuu nadhani walisikia. Safari hii mkarafuu japo haukuwekwa ng'ombe na mkarafuu humo ndani haukupewa asilimia kubwa ya pesa, nikuonyeshe labda mkarafuu hivi sasa kwa Serikali ya Zanzibar labda ni mzigo, sasa kwa sababu ni mzigo lakini wenyewe wenye mikarafuu wanajua faida ya mkarafuu basi waachiwe wenyewe washughulikie mikarafuu yao na karafuu wauze wanapotaka, lakini serikali ishughulikie ili wananchi wasidhulumiwe hizo karafuu zao na serikali ichukue kodi yake kuliko kujitwisha mzigo huu mzito hivi sasa. Serikali bado inadhibiti zao la karafuu lakini kulishughulikia bado ni mzigo mzito.

Jambo jengine Mhe. Spika, ni vituo vya karantini Unguja nzima ina karantini Kisakasaka sasa kweli mtu yuko Kaskazini Unguja atoe ng'ombe kwenda karantini huku Kisakasaka ni ngumu, maeneo haya ndio maeneo yanayoingia ng'ombe kwa wingi kutoka Tanzania Bara kwa sababu hakuna karantini na wananchi wenyewe wa maeneo haya wanataka iwepo karantini na wako tayari kuchangia.

Kwa hivyo ni kazi ya Idara inayohusika na mambo haya ifuatilie jambo hili ili upande wa Kaskazini Unguja na upande wa Kusini sana ya Unguja wawe na sehemu za karantini za mifugo, kulikoni kuacha hivi sasa kama ilivyo ni vigumu na tabu mtu hawezi kutoka na ng'ombe wake Kaskazini ya Unguja akawapeleka Kisakasaka haiwezekani Mhe. Spika, hii tunajidanganya.

Pemba nako inafikiriwa labda kutawekwa karantini hili ni jambo muhimu sana kuweka sehemu hizi za kufikia mifugo, ndio maana maradhi mengi sasa hivi yameingia katika visiwa vyetu vya Zanzibar kwa sababu tumedharau au tumeacha ule utaratibu mzuri uliowekwa na serikali tokea za kikoloni mpaka hii ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwamba lazima unapoingiza wanyama katika nchi waekwe kwanza na wachnguzwe wana matatizo gani.

Mhe. Spika, hata matunda vile vile yanaachwa tu kuingia ovyo katika nchi hii hayawekwi kwanza yakaangaliwa hawa wadudu wa matunda hawa picha inatuonyesha tulikuwa tunasema nzi wa embe funza hili linatoka, sasa hivi sio nzi wa embe tena maana hapa anaonyesha wanaingia katika balungi, kuingia katika tungule na matufaa hata kwenye watu nzi hawa wakikutafuna basi wanakuachia funza na ikiwa ni mtoto mdogo basi mafunza haya yanaendelea na hatimae yanaleta athari mpaka kwa watu.

Mhe. Spika, sasa mambo kama haya ni mambo ya kutizama sana tutakuja kujikuta Wazanzibari tuna matatizo mengi ya wanyama pamoja na mazao ya miti na matunda baadae yatatushinda kuja kuondosha kwa wakati mmoja, sasa hivi tunashindwa kupeleka embe na matunda mengine nchi za nje wakati hapo kati kati ilikuwa ni biashara kidogo iliyokwenda.

Lakini sasa kwa sababu ya matatizo haya ya mafunza na mitego iliyowekwa bado ni kidogo mno haitoshelezi na hizo dawa za kienyeji hazitawanya na hazijafanyiwa utafiti wa kina kwamba kweli zinaua au zinalevya tu. Bado wananchi wa Zanzibar tutakuwa na hilaki ya matunda na hatimae matunda yetu mengi yatakuwa na athari na yatapotea.

Mimi naomba Wizara ya Fedha na Uchumi hizi fedha ulizoitengea hii Wizara mama ya kilimo ni fedha ndogo mno na hazikizi haja, kwa hivyo katika bajeti zinazokuja itizamwe basi Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kupewa pesa nyingi hapa tutapiga kelele tutamwambia mzee wetu lakini ukitizama na fedha anazopewa ni chache mno za kuweza kukidhi mahitaji ya wananchi, mahitaji ya wananchi ya ukulima sasa hivi ni mengi hawalimi mpunga tu kunalimwa mambo mengi wananchi wanataka kulima mazao ya matunda. Lakini wakitizama kuna huyu mdudu wa embe kama tulivyomuita mwanzo lakini sasa hivi ni mdudu wa matunda wanashindwa kujiendeleza katika kulima miti ya matunda.

Mhe. Spika, nikija katika kilimo cha mpunga cha kutegemea mvua tu hakitufikishi pahali Mhe. Spika, sisi Zanzibar tunachukulia Unguja na Pemba tuna mabonde ya kutosha mazuri na makubwa ukiacha ardhi yetu kuwa ni ndogo, lakini kwa sisi wenyewe ni kubwa sana tukitizama tukilinganisha na wenzetu ni ndogo, lakini kwa sisi kile alichotupa Mwenyezi Mungu tunakiona ni kikubwa.

Sasa tukitegemea kilimo cha mpunga kwa kutegemea mvua tu hatufiki pahali niliiomba Wizara ya Fedha na Uchumi nilipokuwa nachangia bajeti kuu iitilie fedha hii wizara ili iweze kumwagilia maji na kumwagilia maji kwenyewe wapate mifereji mpaka katika mashamba au visima kuchimba chini na watu waweze kumwagilia waachane na huu mpunga wa kutegemea mvua. Hii mvua inayonyesha kama safari hii Alhamdullillahi hayakuwa madogo.

Lakini Mhe. Spika, maji ya mvua yote yamepotea sisemi kuvuna kwa sababu maji hayavunwi si mpunga huo, hatuna utaratibu wa kuyakinga haya maji tukayajengea mabwawa na baadae yakatufaa, sisi kila kitu tumekuwa aa haidhuru tutapata hakuna tena mambo hayo duniani sasa kwa sababu hali ya hewa yenyewe huko juu umebadilika.

Sasa tukikinga haya maji ya mvua yataweza kutusaidia katika umwagiliaji wa mpunga, umwagiliaji wa mboga mboga kila siku namwambia Mhe. Ame Mati Wadi hapa kwamba ukulima wa tungule katika eneo lake la Matemwe umeachwa tumeshasahau zamani. Hawa wanangu waliozaliwa juzi niliowazaa mimi hawajui tena kwamba sisi Unguja na Pemba tukinunua tungule kwa visusu hapo sokoni Darajani kutoka Matemwe na nzuri zinapendeza tena zina ladha kwa sababu hazitumii mbolea ya chumvi chumvi mbolea zake ni za kawaida za maumbile.

Lakini sasa kwa sababu wananchi wa Zanzibar hawalimi tena tungule hizi zetu za kienyeji inabidi sasa tungule tuchukue kutoka Tanzania Bara, kabichi na *carote* ambazo juzi juzi hizi kabichi nasema tena ziliua huko kwa sababu zinatiwa madawa mengi na wengine wakachukua dawa ya ngao kutia katika mboga mboga, masikini kajichukulia maji yenyewe huko bara ya shida anapika watoto wakafa wengine wako hospitali ili mradi matatizo.

Lakini tungelikuwa na maji ya kutosha basi wakulima wetu hawa hawa wangelifundishwa kilimo cha utaalam wa mboga mboga, lakini hata hivyo bado Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira inayoshughulika na wakulima wa mboga mboga wachukue jukumu lao la kuwafundisha wakulima, kwa sababu wenzetu wengine huko bara hata hawalimi sehemu kubwa wanalima sehemu ndogo tu ya nyumbani kwake pale basi analima anatoa mboga mboga za kutosha lakini analima kitaalam.

Sisi tusiwaambie wananchi wetu watie mbole ya chumvi chumvi kwa sababu tutapata kile chakula ambacho hakina ladha kwa mbolea za chumvi chumvi, tuwafundisha kutumia hii hii mbolea ya kinyesi cha ng'ombe, kinyesi cha kuku. Vile vile wakati umefika wa kuwaambia akinamama majumbani mtu karibu na nyumba yake achimbe shimo, takataka za chakula sio mifuko ya plastiki na chumba na mabati lakini takataka za chakula kama chichi, mbatata, tungule kitunguu anachomenya, bilinganyi na mambo mengine kama vile wali unaobakia atie mle ndani ya shimo baada likishajaa alifukie lile baada ya muda ile inageuka mbolea atatumia kutilia katika shambani kwake ikiwa ukulima wa mboga mboga au ukulima mwengine.

Lakini sasa hivi taka zote zinakwenda jaani hapo pa kutupa hapana na hapa mjini tuna taka nyingi kweli kweli kwa hivyo sisi wa Mjini pia tuelimishwe, jamani takataka za chakula ziwekeni mbali na taka taka za mabati na makopo zitieni mbali hizi hizi taka taka itakuwa ni mradi mkubwa watu wa kilimo wauandikie kwa sababu huu ni mradi, taka taka hizi za chakula wazichukue waende wakawafundishe wakulima huko mashambani namna ya kuzitumia, pengine wa mashamba wao wanazo takataka lakini hazitokuwa nyingi kama sisi wa mjini tunavyozitumia hivi vyakula.

Basi ni mradi huu kama hamjaubuni ndani ya vichwa nakupeni huu uchukueni, mradi huu uandikieni mpate pesa ili muweze kuwatengenezea wakulima mbolea hii ya kawaida ya maumbile sio ya chumvi chumvi. Sisi vyakula vyetu vitakuwa vizuri na vitakuwa vina soko nchi za nje kwa sababu tujitahidi sisi kugombania soko la nchi za nje, lakini kwa kumuondoa huyu nzi wa matunda na mazao tutapata sisi vyakula vyetu vinasifiwa havitumii mbolea ya chumvi chumvi Mhe. Spika.

Halafu kuna tatizo jengine la ardhi sisi ardhi yetu ni ndogo lakini kuchukua shamba la serikali lililo kubwa sana ukampa mtu mmoja ipo hii Mhe. Waziri, shamba kubwa sana lilikuwa na mifugo zamani mmempa mtu mmoja tu analitumia na anatoa maziwa mengi tunashukuru, lakini sasa hawa wakulima wengine je au hili basi lingelifanywa shamba la maonyesho au sehemu akapewa na sehemu nyengine ikaachwa likafanywa ni shamba la maonyesho kwa ajili ya wafugaji, sasa wafugaji waliko wakatoka wakenda kutizama pale wanatakiwa wafuge vipi kwa njia za kisasa.

Lakini ardhi kubwa sana kapewa mtu mmoja hawa wengine mnawategemeza nini au serikali maonyesho yake ya mifugo ifanye wapi haina ardhi kwa sababu ardhi yote mmempa mtu mmoja kwa matumizi yake binafsi, ichunguzeni wenyewe huko mtaiona.

Jambo jengine Mhe. Spika, ni miti ya matunda imeelezwa humu kwamba imepandwa lakini haitoshelezi ni michache kwa sababu katika kipindi hiki cha mvua zilizopita, minazi kule kwetu Pemba ilikuwa inatafutwa kwa uvumba na udi unatoka kusini mpaka unakwenda Kaskazini Msuka minazi haitoshi, kwa hivyo bado minazi inayopandwa ni midogo na miti mingine ya matunda Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira waipande maana imepotea haipo imetoweka kwa sababu inajenga sana majumba lakini hakuna ule utamaduni Wazanzibari tunaacha utamaduni wa kwamba mtu kwenye nyumba yake apande japo mtofaa, mtomoko, mstafeli miba, mastafeli yale madogo maana hayo yote yana tofauti mwalimu Abdalla Mwinyi anayajua ndio maana ananitizama.

Yote haya ukiyatizama ni mastafeli lakini yote yana jina lake na kila stafeli lina ladha yake, tomoko lina ladha yake kwa sisi Wapemba tunaita tomoko sijui kwa Unguja wanaliita vipi yapo madogo hivi yana nchi, halafu kuna makubwa kidogo mastafeli miba, halafu kuna maduchu sijui yamekaa vipi mastafeli tu tunaita. Yote haya yanaanza kutoweka hayapo hasa yanatoweka toweka sana kwa hivyo watu wanaoshughulika na nasari hizi wazitafute hizi mbegu zilipo popote hapa Unguja na Pemba warudishe tena kwenye nursery, ili watu wafanye kulazimishwa akenda akichukua michungwa pale mia au mia mbili aambiwe na mtonoko mmoja huo kapande.

Mhe. Spika, pale kwetu Mkanjuni palikuwa na mtomoko na mijoko ambayo inafanana na mi-*apples* lakini yana manyoya inapotea haipo, inapotea kuna miti pale kwetu Mkanjuni tukiita mabungo ya kizungu lakini mzungu hajaja na bungo makali sana lakini mazuri sana kwa juice ulibakia mmoja au miwili pale kwetu huo mmoja umeshakatwa, sasa hii ifuatiliwe na ipandwe mama Ashura Abeid Faraji kasema kituo cha Wesha kulikuwa na makarambora, wasiojua makarambora huko nje ni yale mabirimbi makubwa tunaita ya kizungu yenye pembe ukenda marikiti hapo mwezi wa Ramadhan hulinunui ni mazuri sana kwa

juice lakini sasa hivi vinatoka viduchu kwa sababu imeachwa inapotea, mbirimbi vitumbo nazo zinapotea zinabakia hizi za jamaa zanagu za kuungia mchuzi.

Miti mingi ambayo ina asili ya Zanzibar na ambayo tulikuwa tuihuwishe na tuitumie kwa matumizi ya kisasa inapotea, kuna haya mambo ya kutengeneza matunda tukatia ndani ya chupa na vikopo kuna achari zinauzwa humu mijini kwenye maduka, *mango ketchup*, sijui *mango* nini? Zinatengenezwa hapa Zanzibar na watoto wanawake wa Kizanzibari hapa na zinaingia katika soko la kimataifa. Lakini hawasomi hapa hawa watoto wetu wanakwenda wakisoma *VETA* Bara.

Je, Wizara ya Kilimo haina mpango wa kuwasomesha hawa watoto wa hapa Zanzibar na wao wakaweza kufanya mambo kama haya waliokuwa na uwezo wanawapeleka watoto Bara kuja kusoma, wasio na uwezo, ingekuwa kuna chuo na hapa? Japo kidogo cha kuwafundisha kina mama na vijana wetu wa kiume namna ya kusindika vyakula ndani ya chupa au ndani ya makopo. Hawa *VETA* wanafundisha mpaka kufanya *juice*, vijana wetu wanakwenda wanasoma wanafanya hizi *juice*, ukizikuta katika maduka huwezi kutafautisha kwamba hii inatoka nje au inatoka ndani, ni nzuri sana.

Kwa hivyo Wizara ya Kilimo ichukue juhudi hii, ikitangaze hiki chuo kama ipo maana naweza kuambiwa aa ipo jambo hilo. Je, imejitangaza kibiashara kuchukua wanafunzi. Tunatoa watoto wetu wa kike hapa tunawapeleka Tanzania Bara, wiki tatu tu wanasomeshwa pale *VETA* kwa shilingi laki moja na nusu, kula yake mwenyewe na usafiri wake mwenyewe, pale chuoni tu alipe laki moja na nusu. Wanafunzi wetu au watoto wetu wa Zanzibar wangejua kama kipo kitu kama hichi hapa Zanzibar wala tusifanye laki moja na nusu, laki moja, moja tu, ungepata laki moja ngapi. Watoto wangepata ujuzi , wangeingia katika soko la Kimataifa, wangeingia katika soko la kutengeneza hivi vitu wakapata kujiajiri.

Mhe. Spika, leo utakuta kila kitu tunaagiza Tanzania Bara sisi watu wetu watajiondoa lini katika huu umasikini au ufukari uliokolea katika Visiwa hivi vya Zanzibar wakati kazi zipo lakini ndio hivyo tena tunaziacha zinapita Unguja hakuna kazi, Zanzibar hakuna Kazi, kumbe kazi Mhe. Spika, zimejaa tele, nikuwafundisha tu watoto hawa wafanye vipi, basi watafanya. Ni jambo la kulitangaza tu kama hiki chuo kipo au kama hili jambo lipo Zanzibar, basi liingie mtaani kibiashara ili watoto wapate kujiajiri.

Nashukuru kwa kunipa muda huu kwa kuchagia ingawa nna mengi humu lakini leo muda mfupi mfupi. Lakini haya niyokwambia nadhani yanaweza kufanyiwa kazi. Naunga mkono hoja. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Nakushukuru sana Mhe. Spika, na mimi jioni hii kupata nafasi ya kutoa mchango wangu naamini mengi sana yameshasemwa na mimi bado nnamengi na nadhani mengine nitayaacha kutokana na muda ambao tunapangiwa lakini nitajitahidi kuzungumza machache.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi nina masikitiko makubwa, masikitiko yangu kwa sababu mtaa huu wa kilimo niliwahi kupita na mifugo kwa kweli nina huzuni sana kwa upande wangu mimi binafsi naona kama tumerudi nyuma. Inawezekana kama tumesonga mbele kwa kuwa na wataalamu wengi zaidi lakini kwa kweli tumerudi nyuma kwa hali halisi.

Miaka ambayo miye nimeanza kazi kilimo kilikuwa kilimo kweli, mifugo hali kadhalika na mambo mengine. Wakati huo kulikuwa na mashamba ya serikali ambayo wengi hapa wanapiga kelele wanataka wataalamu basi waoneshe zile kazi zao za mifano wakati huo mifano ilikuwepo. Kulikuwa kuna mashamba Mtoni, Pangeni, Bambi, Pemba huko Mtakata na kadhalika lakini *experience* yangu kubwa ilikuwepo hapa Unguja.

Mhe. Spika, jambo linalonizidisha homa na linazidi kunikondesha ni pale Mtoni. Pale ilikuwa ukipita lazima uache safari zao kwanza ukae ushangae, unashangaa nini? Unashangaa wale ng'ombe wakubwa waliokuwepo, leo kila kitu kama ndoto. Ukenda shamba la kuku Mtoni basi ile karibu karibu kama aliyoisema Mhe. Ame Mati hapa, basi hata kisupu kilikuwa kinapatikana, mayai yalikuwa mengi, kila kitu kilikuwa kinafurahisha ndani ya macho.

Mnakwenda kufanya kazi mashambani mnarudi vitu ambavyo vilikuwepo hasa hizi mbomboga. Pale Mtoni licha ya mifugo na kulikuwa na mazao mengi ya mboga mboga kwa kweli ilikuwa inatia moyo sana kwa ilivyo na kwa akili yangu mimi nilikuwa nadhani tungekuwa tumekwenda mbele zaidi ya pale matokeo yake tupo nyuma. Haya yaliyotokezea huku mengine nitakuwa siwezi kuyasemea sana, hiyo ndio hali halisi ilivyokuwa.

Mhe. Spika, kwa upande wangu mimi mchango wangu sitaki nende sana kwenye kitabu lakini nitagusa hapa na pale. Nilikuwa naona kuhaja sasa ya kubadilika. Maanayake haya mazungumzo au maelezo yalikuwemo kwenye kitabu pamoja na michango yetu ni mambo ya zamani, sasa tunakwenda na wakati na huu ni ulimwengu wa sayansi na teknolojia na hata hali halisi ya kiuchumi duniani imebadilika basi na sisi hatuna budi kufuata vile ambavyo watu duniani wanakwenda.

Mhe. Spika, katika kitabu hiki imewekwa hiyo dhana katika ukurasa wa 8 pale wanapozungumzia habati ya mkakati wa mageuzi ya sekta ya kilimo, anasema kwamba ipo haja ya kufanya mageuzi ya kilimo. Hili neno mimi nadhani Mhe.

Waziri na sio yeye tu lakini serikali nzima iyone kama kuna haja hiyo na sio kuiyona tu lakini ni kuifanyia kazi. Katika kuifanyia kazi suala zima linarudi kuja kwenye bajeti ya serikali kwa upande wa wizara hii ilivyopangwa, kwa kweli bajeti ni ndogo sana. Mbali ya udogo wa hiyo bajeti ukitizama lile fungu ambalo serikali linachangia na wahisani wanachangia ndio hapo shuhuli imelala. Kinachotakiwa kwenye maendeleo ni kama bilioni 19.7 kwa wastani. Serikali inatoa bilioni 2 bilioni 17 tunasubiri kupewa. Hivi hapa patafanyika jambo kweli Mhe. Spika.

Haya ndio masikitiko yangu ambayo nayaona na hii dhana nzima iliyoandikwa hapa ya kuwa na mkakati. Mimi hili neno mkakati silipendi. Silipendi kwa sababu imekuwa ni uzoefu, mtu ukimsikia anasema mkakati basi ni kama hadithi ya alinacha hakuna kinachokuwa.

Mhe. Waziri asubuhi alisema hapa mambo ya viwanda, sisi hatuna haja ya kufanya viwanda vikubwa lakini tufanye viwanda vya kati na viwanda vidogo. Vitu vya kufanyia shughuli hizo vipo. Zanzibar kama Kisiwa tumezungukwa na bahati kama ndio shamba letu kuu, hatuhitaji sisi fedha ya kigeni kwenda baharini. Wala sioni kama samaki atahitaji kufanyiwa *paper* ya kuwenda kuomba kumvua na kuna wengine wanazungumzia suala ya baharini kama kwamba wengine wanasema wanakwenda kuwinda samaki, wengine wanasema wanafuga samaki maana yake wanalea mpaka wakuwe.

Mhe. Spika, sisi bahati Mwenyezi Mungu aliyotupa ni kwenda tu tukawachukua kiasi tunachoweza wenyewe. Sasa sijui hapa serikali inashindwa nini, hii fedha ndogo iliyokuwepo tungeanzia hapo. Japan inaendelea katika maendeleo yake makubwa ni baharini na masuala mazima ya samaki. Sasa tukifanya hili tutaweza kujikwamua.

Mhe. Spika, zao kuu la karafuu tumelipa mgongo, mimi nimajaribu kutizama huku nimeona uimarisha wa zao katika ukurasa wa 72. Kama kwamba na sio kama kwamba ndivyo ilivyo haikupewa ule umuhimu mkubwa pengine labda inaonekana kwamba sasa hivi zao hili halikupewa kipaumbele au halituletei tija ya kutosha kiasi kwamba kama ilivyokuwa zamani asilimia 90 ya uchumi tunategemea zao la karafuu.

Mhe. Spika, mwenzangu hapa kidogo amenifilisi Bi Najma lakini ni vizuri kwamba ameshalisema. Muelekeo na jinsi inavyoonekana sasa serikali inashindwa kwenda na hili zao, basi ni bora libinafsishwe. Waachiwe wenyewe wananchi walishuhulikie wauze wanapotaka na serikali iwe inaandaa utaratibu wa jinsi ya wananchi kuweza kupata urahisi wa kuuza mazao yao na kupata lakini na serikali bila shaka itakuwa ina Kamisheni yake, kulikotwika mzigo huu mzito waliyokuwa hawauwezi.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nimekusudia kulizungumza ni suala zima la hali ya kilimo. Labda niseme hali halisi kama ilivyozungumzwa katika kitabu humu nimesema nitagusia gusia ukurasa wa 5 Hali ya Kilimo na Uzalishaji Nchini. Mhe. Waziri ametueleza hapa kuna tani ambazo zimeandikwa humu kwamba kuna ongezeko.

Sisi tunafurahi tukiona hivyo, lakini unapozungumzia ongezeko katika mazao basi moja kwa moja *influence* yake ni kuona kiasi ambacho kunapatikana unafuu kwa mlaji. Mimi bado sijaona mantiki ya kwamba tani za mchele zimeongezeka kutoka kiwango hicho kilichowekwa kwa tani 20,000 kwa mwaka 2008 hadi tani 26,000 kwa mwaka 2009. Najiuliza hivi tumefaidika nini katika hili. Uwagizaji wa mchele umepungua kwa kiasi gani, bei ya mchele imepungua kwa kiasi gani.

Mhe. Spika, takwimu za wataalamu zinasema kwamba mchele mwaka 2005 ulikuwa ukiuzwa kilo moja shilingi 450/= mpaka 500/= tujiulize sasa hivi hayo mapembe tu hata hujatafuta na mbeya ukachanganya ukaweza angalau kuwahami watoto ni kiasi gani?

Saa sijaona bado faida ya kwamba tumepata ongezeko la mchele kitani kwa kuvuna lakini ikawa bado ikawa inapandisha pia bei ya mchele. Ikiwa hivyo ndivyo itabidi basi bora tuvune kidogo ili na bei iwe ndogo. Kwa sababu inaonekana hapa kumbe kuongezeka kwa kuvunwa kwa mpunga ndio kunaongeza bei.

Hapa nataka akija Mhe. Waziri atueleze wanautaratibu upi au wana mkakati gani wa kuona kwamba basi huyu mlaji mwananchi wa kawaida anapata nafuu kwa hichi kinachoambiwa kimeongezeka wakati wa mavuno.

Mhe. Spika, katika suala zima la kilimo nimesema nitasema kijumla jumla kutokana na muda. Mimi binafsi nilikuwa naona tuondokane na utaratibu wa kutumia mbolea za chumvi chumvi. Mimi sijafanya utafiti lakini kwa fikra tu miaka ya nyumba 20, 25 iliyopita na hapa tulipo sasa hivi unaona ile tofauti hata ya afya za watu wetu katika nchi, maradhi ya *pressure*, sukari, yameongezeka sana. inawezekana ni mabadiliko ya hali ya hewa.

Ingawa Mhe. Ame Mati nafikiri alizungumzia kwamba ardhi zimechoka hata mama angu bi Ashura. Lakini ardhi kuchoka kwake baada ya mavuno unatakiwa uipumzishe katika kuipumzisha unakuwa unaiacha inarutubika. Sasa tukiacha kutumia haya machumvi chumvi tungejaribu basi tukaona kama chumvi chumvi na hizi mbolea zetu za asili sinatupa unafuu wa afya kiasi gani. Mashamba yapo yangefanyiwa utafiti, tuseme mashamba ya Mtwango, yatalimiwa kwa mbolea hizi zetu za kienyeji.

Bi. Najma hapa amezungumza kwa vizuri sana kwamba tunataka nyingi sana mitaani humu zinaleta uharibifu tu wa mazingira zingefanyiwa utaratibu vikakusanywa, kuna wanyama hawa yote yakachanganywa tukavumbikwa mambolea yale. Sasa hivi Mhe. Spika, yale maeneo yaliyokuwa majaa zamani watu wanapeleka magari yao wananunua mbolea kwenda kutia katika maeneo yao. Sasa tusichukulie tu kwamba mbolea ya chumvi chumvi unapata kuvuna labda ndizi kubwa au muhogo mkubwa lakini. tutizame hata ile *quality* basi, maanaake *quantity* in kubwa lakini je, *quality* vitu vyetu vingi vinapungua ladha.

Mhe. Spika, hata sisi wenyewe hamu ya chakula imepungua, tofauti ulivyokuwa unakula wali wa nazi na sasa hivi. Mimi zamani nilipokuwa mdogo katika jambo ambalo nilikuwa nalipenda sana na nilikuwa asubuhi nakwenda kwa bibi yangu kwa sababu ya kufata mwiku (uporo wa wali wa nazi) napiga kwa chai aaah! Burdani kabisa sina haja ya kitu kingine. Lakini naukumbuka wale ule na huu wali tunaokula sasa hivi ni tofauti, pamona na kwamba tunatumia nazi vile vile na mchele. Pia najiuliza michele ile wakati ule mimi nilipokuwa mdogo gunia lile sijui lilikuwa la Vietnam au sijui wa Pakistan, gunia la mraba wa kijani ulikuwa ukifanya mafunza unakamatana.

Mhe. Spika, lakini leo unaweza ukapata kigunia au kipakti cha mchele ushakatika katika kwa ubovu lakini humkuti funza. Sasa hii peke yake ni matatizo, nilikuwa naona tuone jinsi gani haya mambolea ya chumvi chumvi yanatuathiri sio tu kwenye mazao na sio tu kwenye ardhi lakini mpaka kwenye miili yetu. Utafiti pia ufanywe katika kuona hebu tujaribu, mbolea ya kawaida na hizi mbolea za kimaendeleo na ukuaji wake na athari zake zinavyokuja ili tuweze kuona chaguo ni lipi kwa sababu Mhe. Spika, mambo ya kufatafata tu sana yanakuwa mara nyingi kuiga iga si kuzuri.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda wako mimi nataka nimalizie kwa masuala yangu mawili.

Katika kitabu hiki kuna maelezo na wameandikwa hapa wanyama wengi wametajwa majina yao katika ukurasa wa 26 kumetajwa jumla ya mifugo laki moja ishirini na mbili elfu, ng'ombe kumi na nne elfu, mbuzi, kondoo, kuna na wanyama kazi. Nadhani kwa Kiswahili ninachojua miye tangu nizaliwe sijui wanyama kazi ni wepi. Kwa sababu mbwa keshaandikwa, kuku, keshaandikwa, najiuliza huyu mnyama kazi ndio yupi?

Kwenye mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi na kiambatisho chake kimewekwa kiambatisho Nam. 2. Kinasema aina ya mafunzo tuna Shahada yaani *Masters degree* watu 13, kuna shahada ya *BA* watu 33, kuna. Stashahada (*PhD*) *Prost Graduate* Stashahada ya Diploma, cheti na kadhalika.

Mhe. Spika, mimi haijanitosha kuandikwa hivi, hivi hii Shahada ya pili ni ya kitu gani. Diploma ya nini, kuna diploma nyingi hasa katika hii fani ya mifugo, kuna mambo mengi sitaki niyataje hapa kwa sababu naweza nikapoteza sana muda. Ingekuwa vizuri basi tukaambiwa ni *degree* za aina gani, masters za aina gani tukaelezwa ili tukaweza kufahamu.

Mhe. Spika, mwisho kabisa ni suala zima la chuo waliposema kwamba wao wanatoa cheti mpaka sasa hivi. Lakini katika ukurasa wa 21 imeandikwa kwamba kuongeza wigo na ubora chuo kinalenga kutekeleza yafuatayo. Kusajili wanafunzi 35 wa ngazi ya cheti na wanafunzi wa stashahada 15. Kidogo nilikuwe napenda nipate ufafanuzi. Mhe. Spika, nakushukuru ingawa muda ni mdogo sana. Ahsante.

Mhe. Ame Ussi Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa jioni hii kupata fursa ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kusimama hapa. Pili niwashukuru wenzangu wote kwa kuwa wale waliochangia Wizara hii.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo ukiitizama ni ndogo lakini ni kubwa mno, kwa sababu ni wizara ambayo tunategemea sisi wananchi wa Zanzibar, ndiyo itatuelekeza na kutupa maarifa katika kilimo au vilimo mbali mbali. Kwa hivyo hii wizara ni vizuri ikasimama na kuona yale malengo iliyojipangia kutekeleza basi yakatekelezwa kwa ufanisi.

Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano na Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nimshukuru Waziri wa Kilimo kwa jitihada zake, pia nimpongeze na pia nimpongeze Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi, Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa zile kazi ambazo tayari wanazifanya na kuzisimamia wao wenyewe.

Mhe. Spika, pia niwashukuru watendaji na pia niwapongeze watendaji, wote hawa wanafanya kazi zao kwa taratibu ambazo wamejipangia wao wenyewe pamoja na kwamba huzifanya zile za taifa zima. Jitihada tunaiyona kwa upande wa Idara ya Uvuvi kwa miradi ambayo inasimamia. Lakini pia tumeona katika kitabu hiki miradi au jitihada ambazo zinafanywa na Wizara ya Kilimo kupitia sera ambayo tayari inatekelezwa 2009/2010.

Mhe. Spika, sasa hivi nakwenda katika lengo la mwaka 2010/2011, hasa kilimo kwa ujumla. Kilimo ni uti wa mgongo kwa nchi yetu au kwa jamii bila ya kilimo nafikiri hatutofika popote itakuwa ni ile ile tu kwenda kwenye maduka na kutizama mfuko kuanza kununua. Jitihada zinatakiwa zaidi zitilie mkazo katika kilimo. Kuna maelezo humu ambayo kuna maeneo tayari Wizara yenyewe imejipanga kuyatekeleza hayo.

Mhe. Spika, hayo hayatoshi kutekeleza kwamba tumeanza, lakini tutatekeleza, sasa tunataka tunatekeleza, ile miradi ambayo tayari imejipangia, mradi mmoja mmoja inayogusa vikundi, wananchi mmoja mmoja. Lazima hii nayo ingesimamiwa na mabwana shamba kwa uangalifu kabisa na umakini. Wakatupa mda wao wakaelekea kule vijijini ambako wananchi zaidi ndio wanakojikita na ukulima wa mpunga, mahindi, mbaazi, viazi kama vilivyoainishwa katika kitabu hiki.

Mhe. Spika, lakini sasa tungewaangalia zaidi wale wanaolima kijembe kongoroka kama maneno ya Mhe. Najma huwa anasema sana kijembe kongoroka. Ukulima wa maweni hakuna trekta kule Mheshimiwa hebu tuwape na wao maarifa ya kuweza kulima. Wanajua wenyewe lakini sasa kwa kuwa Wizara imesema inaipa kipaumbele suala la kulima basi na madhali mabwana shamba wapo basi waelimishwe.

Mhe. Spika, wenzangu wengi wamesema Mhe. Mati kasema hapa miongo au zile season za kilimo sasa wafahamishwe na wale ili wajue kwa sababu kule watu wanajilimia tu wanajua mimi asubuhi nakwenda shambani matokeo yake kilimo chenyewe kinakuwa duni, hakina rutba yoyote kwa sababu na ile ardhi yenyewe ni ya mawe. Sasa hebu kama kweli wapo mabwana shamba waelekee kule nako kwenye ardhi ya mawe waanze kuonesha mfano kwamba ardhi hii inatakiwa ilimwe hivi.

Mhe. Spika, nikija kwenye miradi hii ya *PADEP* mimi nashukuru, niipongeze idara hii. Miradi ya *PADEP* tunayo lakini kuwa na mradi au kupata mradi sio mafanikio. Nakusudia kuzungumza hivyo kwa sababu miradi iliyopo ya *PADEP* baada ya kwisha kupewa mradi au kwisha kumsomesha mtu mara moja bila ya kwenda kumkagua na kumpa maelekezo mimi nafikiri gado hujamuwezesha zaidi. Kwa sababu tunao sisi mradi wa *PADEP* watu wamejikusanya jamii wamekaa, wamepanda minazi, wamewahi kuuza lakini hawajaja kukaguliwa.

Mhe. Spika, halafu kuna minazi ipatayo kama mia nane, sasa hivi minazi ile inakufa. Wale wamefikia pale kulima tu. Binafsi mimi mwenyewe niliwahi kuzungumza na Mheshimiwa kwamba twende ukaone miradi ile kule kunabiashara nzuri sana hebu tusaidiane kwa sababu wahusika wameshaandika barua wenyewe jamii. Jamani tusaidieni tupate soko, lakini hadi leo.

Sasa hiyo *PADEP* ipo lakini sasa wale wanachokifanya hawakijui. Ile minazi waipeleke wapi ina maana wametumia nguvu zao bure sasa hivi inakufa. Pale kuna kisima cha maji lakini hakina pampu. Sasa basi kama tunataka miradi hii iwe endelevu basi hebu tuone na Shirika ama Idara inatusaidia kupata ile miradi ambayo tunaweza kubadilisha miradi mengine pamoja na ile ya mboga mboga na ile ya minazi ili tutumie tupate mafanikio.

Mhe. Spika, nikwenda kwenye Ukanda wa Pwani kwenye Bahari Kuu kwenye hiyo *MACEMP* mimi nashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi ni mtu ambaye yeye anashuhulikia masuala haya na ni mtu ambaye fuatilia kile kitu ambacho ni dhamana yake amepewa kwamba kitu hiki tumia kwa masuala haya anatumia, anapita anaangalia. Nashukuru katika maeneo ya miradi hii *MACEMP* takriban tumefanikiwa. Mimi ningeomba Mkurugenzi asichoke bado kwa sababu kilimo cha watu wa Kaskazini ni bahari zaidi, kwa hivyo akatupia macho kule zaidi.

Pamoja na jitihada zake zote kwa kweli tunamshukuru sana lakini basi aone kwamba bado miye nipo na awe karibu zaidi kama alivyokuwa karibu basi azidi kusogea ili hawa watu nao kwa sababu Nungwi wameshajua faida ya hii miradi hasa *MACEMP*, mwani na mambo mengine kuna kitabu hapa kimeonesha jinsi ya wale samaki ambao wanaovuliwa Nungwi na waliowakamata wamewashika kwenye mikono ni watu wa Nungwi hakika. Kwa hivyo, asitushoke azidi kutusaidia bado kuna wengine wana hamu kama vile ambavyo wenzao wameshafanikiwa.

Mhe. Spika, nikija katika mazingira ni kwamba mazingira Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha alizungumza kwamba mazingira ina upana wake na mimi nasema hivyo hivyo nakubaliana nae kwa hilo. Mhe. Spika, kuna mazingira ya kupanda mikoko, mazingira ya usafi, mazingira ya kuona kwamba nini tunakiimarisha katika upandaji ikiwa miti au ujenzi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, idara hii nayo mimi nashauri ikae na zile sekta za idara nyengine ambazo zinakutana, kwa sababu mazingira yanagusa ardhi. Mhe. Spika, walione hili suala ili wapate kulisimamia.

Mhe. Spika, maana yangu ni kwamba unapotokezea ujenzi hii Idara ya Mazingira ni vyema ihusishwe ili ijue kwamba tukijenga hivi hapa patakuwa hivi, kuwe na ushauri uwe unatolewa sio kwa sababu *ZRB* anataka kukusanya pesa iwe anajenga tu au Wizara ya Biashara inajenga tu umeshapewa kibali. Mhe. Spika, ni vyema tuangalie na mazingira ya bahari yetu hasa ukizingatia kule baharini kuna vyombo.

Mhe. Spika, kamati yetu ilipotembelea katika Shirika la Bandari tulipata hili tatizo kwamba mnara itabidi uongezwe juu kwa hivyo na haya yaonekane kwamba ni matatizo, tusitafute uchumi wakati uchumi huo unaingia mahali sipo, tutafute maeneo ambayo tutapata uchumi ambao hautaathiri kitu.

Mhe. Spika, wengi wanafurahia kwamba sawa *jetty* tunapata pesa lakini je, kwa athari za meli Mhe. Spika, kimazingira hilo linakubalika. Meli kama haijaona ule mnara mpaka ikaja kwenye mwambao wa juu si itagonga, hili suala ndio nalisema hapa. Mhe. Spika, ndio nikasema kwamba Idara ya Mazingira au Idara ya Uvuvi ihusishwe na masuala haya hasa yanayohusiana na mambo ya ukanda

wa pwani. Mhe. Spika, hapa kumetajwa vyama vya ushirika je, hivi vyama vipo na vinafanya kazi gani na kama vipo ni vingapi. Mhe. Spika, kwa sababu kuna chama cha ushirika pale kina nyumba yake kule Tanga wala hatujui inafanya nini. Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja mia juu ya mia.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipatia nafasi kidogo yakuzungumza angalau machache kuhusiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira. Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwamba sisi watu ambao tunaishi katika visiwa hivi, kisiwa cha Unguja na kisiwa cha Pemba tunahitilafiana kwa maumbile ya visiwa hivi. Yaani ukiangalia kisiwa cha Pemba kina maumbile tofauti na kisiwa cha Unguja. Kisiwa cha Pemba maumbile yake kina milima pamoja na mabonde na sehemu ya tambarare iliyobakia ipo lakini si kwa shughuli nzito za kilimo, kutakuwa na shughuli nyengine za kilimo ambazo ni nyepesi nyepesi. Lakini tukiingia sehemu ya Unguja tutakuta kama sehemu kubwa ni tambarare ambayo kuna uwezekano wa kuweza kutumilia matrekta kwa wingi kwa sababu ya uzalishaji wa kilimo.

Kwa hivyo, mimi nataka niseme tu pamoja na maumbile ya visiwa vyetu lakini bado kama ni visiwa tutakuwa tumezungukwa na bahari. Kwa hivyo, sisi tunaoishi katika nchi hii tutakuwa tuna mambo ambayo sisi tunayategemea, moja katika hilo ni hicho kilimo chenyewe, tunategemea uvuvi uliokuwepo hapa na tunategemea mifugo ndio amali ya watu wa nchi hii.

Mhe. Spika, hizo ndizo sababu muhimu pamoja na kilimo cha mboga mboga. Lakini nia na madhumuni ya wizara hii ni kutaka kuhakikisha kwamba yote haya kilimo, mifugo pamoja na ufugaji dhamira yake kubwa ni kutaka kuwapunguzia watu umasikini kwa sababu hizi ni amali ambazo zitapunguza umasikini. Pia katika hili ni kwamba wizara inategemea kuwa itaweza katika shughuli hizi kuwaongezea watu kipato chao cha maisha.

Mhe. Spika, nasema yote haya kwa wizara zetu bado hazijaweza kuwajengea uwezo wote hawa ikiwa ni kilimo, mifugo au kilimo cha mboga mboga na uvuvi bado hatujaweza kufikia *standard* ya kuhakikisha kwamba haya mambo tunaweza tukayafanikisha vizuri. Kwa hivyo, kama tutapitia katika sehemu ndogo ndogo za majimbo yetu tunaona kwamba katika suala la mifugo bado hatujafikia ile hali ya kuhakikisha kuwatoa watu katika mifugo ambayo ni *traditional type* kwa sababu mifugo yao mingi haina uwezo wa kutoa maziwa ya kutosha.

Mhe. Spika, ng'ombe zetu bado uwezo wao ni mdogo. Kwa hivyo, je, wizara hii ina lengo gani la kuwasaidia wananchi kuondokana na mfumo ule wa ufugaji wa ng'ombe zile *traditional* na kuwapeleka katika ng'ombe za kisasa. Je, ni kiasi gani tunaweza kumudu suala hili?

Mhe. Spika, hapa kama tumefikia kweli tunaweza kuwafanya watu wetu kwa kila majimbo ambayo kwa kiasi fulani tunaweza kuyapunguzia haya nafikiri hapo itakuwa tunaondosha katika mifugo ya zamani na tunawapeleka katika mifugo ya sasa. Mhe. Spika, lakini hayo ni matatizo makubwa.

Mhe. Spika, kitu ambacho nikaona ambacho kinaendelea vizuri ni ufugaji wa kuku. Mhe. Spika, ufugaji wa kuku umeshamiri na watu wameupokea vizuri na unaendelea vizuri. Lakini katika mifugo bado wizara ina kazi kubwa yakuweza kuwasaidia wananchi. Mhe. Spika, sehemu nyengine watu wanafuga mbuzi, wengine hawafugi mifugo iko upande mmoja sehemu ambazo zile za tambarare.

Mhe. Spika, nikiingia katika sehemu nyengine ambayo ni muhimu zaidi, nikiingia katika sehemu ya kilimo hapa mimi nasema hakuna haja ya kuilamu wizara kwamba inashindwa kutekeleza majukumu yake au kuwawezesha watu. Mhe. Spika, hapa sisi tunazungumza kama ni wawakilishi, lakini mimi ninalolizungumza hapa ni kwamba kitu kikubwa ambacho nakitegemea hapa ni kiasi gani bajeti ya kilimo inatolewa.

Mhe. Spika, ugavi wake unakwenda vipi na inaonesha kwamba ugavi katika kilimo ni mdogo sana kiasi ambacho asilimia inayotolewa ni 6 tu ambayo hiyo ya makubalianao ni asilimia 10 tu. Kwa hivyo, hatujafikia katika kiwango kikubwa hali hii inavyoonesha kuwa Wizara ya Kilimo bado itakuwa na bajeti tegemezi.

Kwa mfano, ambao ninaouona hapa katika kitabu cha Mhe. Waziri kutokana na miradi kumi na saba ambayo iliyokuwepo hapa miradi hii imetengewa fedha upande wa serikali na imetengewa fedha katika upande wa wafadhili. Utaona katika pesa ambazo zipo hapa kumi na tisa bilioni utakuta ni bilioni mbili tu ambazo SMZ au wizara yake ndio inaweza kutoa bilioni yaani bilioni 17 zilizobakia inabidi zitolewe na wahisani.

Mhe. Spika, tuangalie sisi tunataka kuuhisha maisha ya watu, tunataka tukuze kilimo, tuuze ndani na vyengine tukauze nje lakii wizara yenyewe uwezo wake ni mdogo. Mimi nasema hapa tumlaumu nani, tumlaumu waziri hawakumpa pesa za kutosha, yeye waziri anataka awe na pesa nyingi afanye yote haya lakini bajeti yetu ni bajeti tegemezi hatuna namna hivi sasa ya kumlaumu waziri kwamba hili hakulifanya na hili hakulifanya, hapa tunazungumza kama kawaida lakini hiyo ndio hali halisi.

Mhe. Spika, kinachobakia sasa hivi kwa hali hii tunayoendelea ni lazima tuseme kwamba wizara yako inategemea zaidi kuweka uhakika wa chakula, sasa uhakika wa chakula tumeuona kutokana na bajeti yenyewe. Mhe. Spika, chakula chenyewe kinachozalishwa ni kidogo. Vile vile tunataka kujua usambazaji wa hizi mbegu ukoje, hapa pana visiwa viwili je, kweli katika mbegu ambazo za

kisasa ni mbegu bora ambao uzalishaji wake ni mkubwa umeenezwa kiasi gani kwa Unguja na kwa Pemba. Mhe. Spika, mimi ninavyofikiria mpaka hivi sasa ni kwamba maeneo ambayo Wizara ya Kilimo yanayotumia ni yale yale bado kuna maeneo hapa hapa Unguja mengi sana ambayo wizara hii inaweza kuyaendeleza, lakini kwa sababu ya mfuko wake ni mdogo anashindwa kununua matrekta ya kutosha, anashindwa kuwaendeleza watu katika suala la kilimo.

Mhe. Spika, pia mimi nataka niseme kwamba mpaka lini wizara hii itawategemea watu ambao umri wao ni mkubwa katika uzalishaji. Je, katika nchi hii wanaozalisha ni nani na waliobakia ni nani. Mimi kwa mawazo yangu ninavyofikiria kwamba uzalishaji mkubwa unazalishwa na watu wazima walioko katika vijiji vyao, lakini vijana asilimia kubwa katika suala la kilimo hawataki kwenda kulima. Je, wizara ina mpango gani kuhakikisha nao inawashirikisha vijana au inawatoa vijana katika suala zima la kilimo.

Mhe. Spika, bado tuna kazi nguvu ya kwenda kulima fedha tunaitaka, watu tunawahitajia, na vijana tunawahitajia katika suala hili lakini bado vijana hatunao katika shughuli za kilimo wanachokitaka ni mazungumzo, makundi na shughuli zao nyengine ndogo ndogo za biashara. Mimi niseme kwa uhakika Mhe. Spika, ni kwamba kama tunachukua mambo mawili tukayalinganisha baina ya kilimo na biashara sidhani kama tunaweza kupata wawekezaji wakaweza kuekeza fedha zao katika kilimo, ni kwamba watu hawataki yaani wanaingia katika hasara hawaingii katika faida. Lakini akiwa anataka kuwekeza kwenye biashara ana uhakika akiwekeza kwenye biashara atapata faida, lakini anaona kama akiingia katika kilimo pesa hizo zitapotea. Kwa hivyo, hapa namna gani wizara itaweza kushajihisha suala hili kwenye kilimo.

Mhe. Spika, kuhusu suala la umwagiliaji maji inaonekana kwamba kuna maeneo maalum ambayo sasa hivi yanaendelea, lakini halikadhalika mimi nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba si hapa tu Unguja hata kule Pemba mimi nimeshamwita mara nyingi waziri kuja katika tambarare nina tambarare kubwa sana na nimeshamwita. Mimi Konde ninayo maji ya kutosha yakuweza kufanya umwagiliaji wa maji, tuondokane na mvua ambazo ni *natural rain* tuingie katika maji haya ya uzalishaji kwa wingi. Lakini bado mpaka sasa hivi suala hilo mimi kwangu waziri hajaja akaniona na mimi nikamuonesha tukazungumza na mimi nikapata kilimo cha umwagiliaji maeneo ninayo, maji ninayo lakini bado sijapata kitu.

Mhe. Spika, katika suala jengine ambalo ni zito katika suala la kilimo ni lazima tuhakikishe watu wetu wote wakulima tunaweza kusambaza mbolea kila pale ambapo panahitajika. Je, mbolea zinapelekwa kwa wakati na je, kilimo kinalimwa kwa wakati au watu wanalima kwa wakati wao wenyewe wanaotaka. Hili ni suala muhimu ambalo wizara inazidi kuangalia.

Mhe. Spika, suala la madawa ni muhimu sana na lazima lipelekwe kwa wakati. Lakini zaidi mimi naona wizara hii inahitaji kujiingiza katika suala takwimu, takwimu ni kitu muhimu. Nafikiri serikali kama haina *data information* basi haiwezi kupanga mambo yake sawa sawa, sijui hii Wizara ya Kilimo takwimu zake zikoje. Sisi hatujaziona hapa takwimu za kilimo kutuonesha kama iko hivi hivi, watu wako hivi hivi, kilimo kinakwenda hivi na bado hivi, maeneo yaliyolimwa ni haya, yasiyolimwa ni haya, sababu ni zipi. Kwa hivyo, takwimu ni kitu muhimu tunataka tupate takwimu za kutosha kwa wakulima na maeneo yao.

Mhe. Spika, zaidi niingie katika suala la uvuvi na mazao ya baharini. Waheshimiwa Wajumbe hili suala bado tumeshindwa kuwapata wawekezaji wakaja kwenye maeneo haya. Maana ameshaonesha kwamba kwa miaka kupita bado tunaendelea na uvuvi ule ule wa mshipi na uvuvi wa nyavu. Ahsante sana Mhe. Spika.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 30/06/2010 saa 3:00 asubuhi)